ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe.Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu

	na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake

39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
55.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
57.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
58. Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini
59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
62.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
63.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
65.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
66.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
67.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
68.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
69.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
72.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim — **Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Ishirini na Tano – Tarehe 22 Julai, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti, (Mohmoud Mahammed Mussa) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Moh'd Ali (Makamu Mwenyekiti Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Nam. 174

Utaratibu wa Kushusha Mizigo Bandarini

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Siku za nyuma kidogo Bandari ya Malindi Unguja ilikuwa na utaratibu wa kuruhusu meli za mizigo kushusha mizigo usiku, ili kupunguza msongamano wa meli mchana na kuharakisha kazi za upakuaji mizigo. Mambo sasa yamebadilika, meli haziruhusiwe kushusha mizigo baada ya saa 3 mchana, ambapo wakati wa asubuhi meli za mizigo mara nyengine zinakosa nafasi ya kushusha mizigo.

(a) Mhe. Waziri huoni kuwa amri ya kutoshusha mizigo usiku inasababisha usumbufu mkubwa kwa wenye meli na wafanyabiashara.

(b) Je, Mhe. Waziri una mpango gani wa kuondosha tatizo la msongamano wa meli za mizigo unaosababishwa na kuzuia meli kushusha mizigo usiku.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 174 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa hapo nyuma Bandari ya Malindi Unguja ilikuwa ina utaratibu wa kuruhusu meli za mizigo kushusha mizigo usiku, lakini kwa sasa utaratibu huo umesitishwa kutokana na Ushauri wa Kiulinzi na Usalama, kwani mizigo inayoletwa na meli hizo ni mchanganyiko kwa hivyo ni vigumu kuweza kuikagua vizuri wakati wa usiku.

Hata hivyo, pindipo meli ikileta bidhaa za aina moja kunakuwa na utaratibu wa kuomba ruhusa *TRA* na Vyombo vya Ulinzi Bandarini, ili kazi hiyo iweze kufanyika usiku.

(a) Amri ya kutoshusha mizigo usiku inapaswa kutekelezwa kwa sababu za kiusalama wa nchi na raia wake.

(b) Ili kuondosha usumbufu unaotokea kwa wafanyabiashara, wenye meli wanashauriwa waanze safari zao mapema, ili wafike mapema jioni na kazi za ushushaji zifanywe kwa wakati uliopangwa hadi kufika saa 1:00 usiku na wala si zaidi ya hapo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka ku-*declare interest* kwenye suala hili.

(a) Wakati mizigo inatolewa usiku kuna tatizo gani la kiusalama lililojitokeza ambalo lilipelekea mizigo kushushwa usiku na huu ni karibu mwaka wa kumi?

(b) Ni hatari gani za kiusalama zinazoathiri meli za ndani na ikawa hakuna athari za meli za nje ambazo zinaruhusiwa kushusha na meli zile ni hatari wakati zinapopiga Somali huchukua hata silaha kwa ajili ya kuweza kujihami? *(Makofi)*

(c) Unasema mpaka uombe *TRA* na ulinzi kwa vyombo vya usalama. Sasa *TRA* ipo Bandari masaa 24 pamoja na ulinzi upo masaa 24 isipokuwa huwa wanapokezana? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti,

(a) Bandari haifanyi kazi peke yake na tunapopata ushauri kwa wenzetu kuhusu usalama na ulinzi wa nchi hii na raia wake, basi hakuna

compromise katika suala la ulinzi na usalama wa raia hawa. Kwa hivyo, awali kulikuwa na utaratibu huo, lakini mpaka utaratibu huo ulipoonekana kwamba kuna tatizo la usalama na ulinzi katika Bandari ndipo yalipofanywa maamuzi haya.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niende mbali zaidi kwamba bandari yetu inatumiwa na meli nyingi sana za kimataifa na kuna wakati tulipewa *ultimatum* kwamba hali ya usalama bandarini si nzuri na ifikapo tarehe fulani kama Bandari ya Zanzibar haijafanya moja, mbili, tatu, nne, basi bandari hii itafungwa.

Kwa hivyo, itafungwa kwa maana gani meli zote za nje ya Kimarekani hazitaruhusiwa kuja hapa na kama watachukua mizigo kutoka hapa basi mizigo haitokubaliwa kupakuliwa bandari yoyote ile nje ya nchi hii. Sasa inapofika hali hiyo wakati asilimia 70 za meli ni za Kimarekani sisi tungekuwa na bandari tena. Kwa hivyo, katika suala la ulinzi na usalama wa bandari yetu na nchi yetu hili halina *compromise*. *(Makofi)*

(b) Meli za nje ni kweli zinakuja, lakini tumesema hata hizi za ndani kama kuna mizigo ya namna moja basi hatukatai. Kwa kweli meli zote za nje zinazokuja hapa mizigo inateremshwa na inahifadhiwa pale bandarini na kila mwenye mzigo wake anakuja kuchukua mizigo ile kutokana na taratibu.

Kwa hivyo, si suala kwamba meli za nje zinaruhusiwa na hata hizi za ndani kama mizigo si ya mchanganyiko, kwa sababu mizigo ya mchanganyiko inamatatizo Waheshimiwa Wajumbe. Kwa mfano, watu wamekamatwa wameingiza mito, kumbe vile ndani ya mito ile kuna Bangui, vile vile kuna magunia ya mahindi na maharage kumekutwa bunduki zimefungwa ndani ya magunia. Sasa watu wanaingia na bunduki na bastola kuna usalama hapo. *(Makofi)*
Kwa hivyo, suala hili kwa serikali nasema ni utaratibu ambao tunaona unasaidia zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, alisema Mhe. Mjumbe kwamba *TRA* wanafanyakazi masaa 24 pamoja na ulinzi upo masaaa 24. Lakini pamoja na yote kufanyakazi usiku ni kufanyakazi usiku. Hivyo, suala la ulinzi halina *compromise* katika bandari yetu na wala hatukubali hata siku moja bandari hii kwa sababu yoyote ile ikaja ikafungwa au meli zikawa haziji kwa sababu tu, watu wengine wafanyabiashara au wapi kuna usumbufu.

Kwa hivyo, wache wasumbuke na bandari yetu ni salama pamoja na raia wetu wako salama, kwani biashara ni kusumbuka. *(Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali la nyongeza amesema kwamba kuliwekwa masharti ya kimataifa na kama hayakukamilika masharti hayo, basi bandari yetu ingefungwa na meli za kigeni zingekuwa haziji.

(a) Je, masharti yote yaliyowekwa ya kimataifa kwenye bandari yetu yamekamilika?

(b) Kwa sababu amesema kwenye mizigo inayopelekwa pale na mimi nakumbuka siku za nyuma kulikamatwa silaha ambazo kuwa zilikuwa zinaingizwa na watu kwa ajili ya kuja kufanya hujuma Zanzibar. Je, kulingana na kadhia hiyo sasa haoni kwamba kuna haja ya kuweka chombo maalum ambacho kitakuwa kinaona ama silaha au mambo mazito mabaya yanayoletwa kuingizwa katika nchi yetu, ili kuwapunguzia kazi ngumu walinzi wetu waliopo bandarini?

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa masharti ambayo tusingeyatekeleza basi bandari yetu ingesusiwa ni haya yafuatayo:-

- Wakaguzi kutoka *IMO* waliona kwamba bandari yetu ni soko, yaani wanaosindikiza ni wengi zaidi kuliko wanaopokelewa hakuna utaratibu maalum. Katika dunia hii ya ujangili na uharamia suala la kila mtu kuingia bandarini halikubaliki.
  Kwa hivyo, kwanza tunaona kwa yeyote atakayeingia bandarini kuwe na utaratibu maalum tena awe na kitambulisho maalum, ili bandari ijue kwamba huyu aliyeingia humu anajulikana. Hivyo, hilo tayari tumeanza kulifanyiakazi na hivi sasa bandari yetu inao watu wale wanaostahiki kuingia. *(Makofi)*

- Pili ni kutenganisha Bandari Kubwa na Bandari ya Majahazi na tumetakiwa tujenge ukuta. Kwa hivyo, bandari imejenga ukuta madhubuti, hivyo watu wa Bandari ya Majahazi hawaonani kabisa na watu wa Bandari Kubwa ambayo inashughulikia meli kubwa na kati kati yake kuna haya *boom. (Makofi)*

- Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni usalama wa bandari yenyewe. Kwa kweli baadhi ya wafanyakazi wetu hawakuwa na elimu ya kutosha katika suala la ulinzi. Kwa hivyo, tume-*organize* semina nzuri tu na

tayari zimeshafanyika mara tatu na semina hizo *Alhamdulilllah Rabillalamina* zimeweza kuwafanya wafanyakazi wetu wa bandarini kuwa na *awareness* ya ulinzi.

- Suala jengine ni taa za usiku na hili tunalishughulikia. Mhe. Mwenyekiti, minara yetu kama nilivyosema juzi ni kwamba mifupi kwa sababu hatukuwa na utaratibu wa kuweka makontena yetu mpaka ghorofa tano na mwisho ilikuwa ni ghorofa mbili au tatu. Sasa kwa sababu ya ufinyu wa bandari yetu imebidi sasa makontena ni mengi basi tuyaweke mpaka daraja tano. Kwa hivyo, daraja tano ni urefu mkubwa kiasi ambacho zile taa za bandarini zinakuwa hazioneshi upande wa pili na hilo tunalifanyiakazi. *(Makofi)*

  Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na taarifa ya Baraza hili pamoja na wananchi kwa jumla, hivi sasa bandari yetu iko *safe* na *Alhamdulilah Rabillalamina* hakuna tena uwezekano au ubishi kama itafungwa au haitofungwa, hivyo, bandari yetu haina tatizo. *(Makofi)*

Vile vile kuhusu chombo maalum cha ukaguzi. Mhe. Mwenyekiti, tumewasiliana na *TRA*, kwa sababu kwanza si suala la silaha au vipi, lakini hata vitu vyenyewe vinavyoletwa kwenye makontena. Kwa hiyo, utaratibu unatengenezwa kuweka *scanner* ambayo itaweza ku-*scan* mizigo yeto iliomo ndani ya kontena bila ya kontena kufunguliwa. Kwa hivyo, kama uli-*declare* kwenye *manifesto* yako kwamba umeleta mchele, lakini kumbe mna *electronics* itabaina pale. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kuhusu vitu vidogo kama vile silaha, bangi pamoja na vitu vyengine tunalikalia pamoja na wenzetu, yaani sisi kama bandari na wenzetu, ili kuona ni vifaa gani ambavyo ni *portable* vinaweza kutumika kuhakikisha kwamba si Bandarini wala Uwanja wa Ndege vitu hivi havipiti bila ya kujulikana. *(Makofi)*

Nam. 224

Kuanzishwa kwa Skuli Banafsi

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa – Aliuliza:-
Baada ya Mabadiliko ya kiuchumi na kimaendeleo, serikali imewaruhusu wananchi wazalendo na wawekezaji wa nje kuekeza katika sekta mbali mbali ikiwemo elimu. Kufuatia fursa hiyo skuli mbali mbali za binafsi zimefunguliwa na zimekuwa zikisaidia sana katika kukuza na kuendeleza Sekta ya Elimu hapa nchini. Hata hivyo, baadhi ya skuli hizo zinadhaniwa kwamba uwezo wao ni wa kutia mashaka hasa zile zinazojiita za Kimataifa (*International Schools*).

(a) Ni hatua gani ambazo muwekezaji anatakiwa kuzifuata hadi aruhusiwe kuanzisha skuli binafsi?

(b) Vigezo gani vinavyoifanya skuli iitwe *International School*?

(c) Je, hizo skuli zinazojiita *International School* hapa Zanzibar zimefikia vigezo hivyo. Kama hazikufikia kwa nini ziruhusiwe kuitwa *International School*?

(d) Kwa vile ada za masomo kwa skuli binafsi zinapishana sana baina ya skuli na skuli. Je, serikali haioni kwamba wakati umefika kwa serikali kuweka alau mwelekeo wa ada kwa skuli zote za binafsi?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 224 lenye vifungu (a), (b), (c) na (d).

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliruhusu kuanzishwa kwa Skuli Binafsi kwa madhumuni ya kuchangia katika kukuza na kuendeleza Sekta ya Elimu. Pia ni kweli kuwa baadhi ya skuli zilizoanzishwa zimepewa majina ya aina mbali mbali yakiwemo majina ya "*International School*".

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kujibu kama ifuatavyo:-

(a) Kabla ya Mwekezaji mzalendo kuanzisha skuli anapaswa kuwasilishwa ombi lake Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na kama ni Mwekezaji wa nje, ombi la kuanzisha skuli huwasilishwa kwa Mamlaka ya Vitega Uchumi, Zanzibar (*ZIPA*). Ombi hilo huambatana na taarifa zote za aina ya skuli itakayoanzishwa, ngazi ya elimu, ukubwa wa skuli na idadi ya walimu na wanafunzi inayotarajia kuandikisha. Majengo yanayotarajiwa kutumiwa hufanyiwa ukaguzi, ili kuhakikisha kuwa yanakidhi mahitaji ya skuli na pindipo yanaridhisha kibali cha kuanzisha skuli hutolewa.

(b) Mwekezaji anaruhusiwa kuiita skuli yake jina lolote ilimradi halikiuki maadili ya nchi. Wizara haina kigezo maalum kwa skuli kupewa jina la *International.* Baadhi ya Skuli zinaitwa *International School* kumaanisha kuwa zinapokea wanafunzi

wenyeji na wageni. Hata hivyo, zipo skuli chache zilizoanzishwa kwa madhumuni ya kuhudumia watoto wa wataalamu wa nje wanaofanya kazi zao hapa Zanzibar. Skuli hizo pia hupokea wanafunzi wa kizalendo.

(c) Hivi sasa, wizara hairuhusu skuli binafsi kutumia jina la *International School* kwa vile inaonekana wengi wa wawekezaji wanatumia jina hilo bila ya malengo mahsusi. Skuli ambayo itakubaliwa kuitwa *International* itakuwa ni skuli inayoanzishwa kwa dhamira ya kuhudumia watoto wa raia wa kigeni wanaoishi hapa na wameruhusiwa kutumia Mitaala ya Kimataifa.

(d) Wizara imeweka vigezo vya kuzingatia gharama za uendeshaji wa skuli kabla ya mwenye skuli binafsi kuruhusiwa kutoza au kuongeza ada. Mwekezaji anapaswa kuomba kwa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kiwango cha ada ya masomo kwa ajili ya Skuli yake.

Ada za masomo za skuli binafsi zinatofautiana baina ya skuli binafsi kutokana na aina ya skuli, ubora wa walimu wake, aina ya majengo na huduma nyengine muhimu zinazotolewa. Vigezo hivyo, ndio vinavyovutia wazazi kuchagua skuli bora ya kupeleka watoto wao.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

(a) Kutokana na wimbi kumbwa la skuli nyingi kuitwa *International* bado hamjaona kwamba kuna haja ya kuweka vigezo na utaratibu mzuri?

(b) Hivi Mhe. Waziri unaweza kulieleza Baraza ni skuli ngapi za Zanzibar ambazo tunaweza kuziita *International*?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mwenyekiti, tumeiona hiyo haja na Mhe. Waziri katika majumuisho yake kutokana na maelezo mengi ambayo walitoa Wajumbe wako wa Baraza lako tukufu. Sambamba na hilo, maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ambayo Mhe. Mwakilishi yeye ni mjumbe wa kamati hiyo, tuliona kuna umuhimu wa kuweka vigezo hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni tutatoa utaratibu wa vigezo hivi utakavyokuwa. Lakini miongoni mwa vigezo hivi ni kwanza skuli yenyewe itakayoanzishwa basi angalau iwe na asilimia 40 ya watoto wa kigeni.

Vile vile kama nilivyoeleza katika jibu langu mama, skuli hiyo iwe inafuata Mitaala ya Kimataifa. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mussa Khamis Silima: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Je, skuli hizo za watu binafsi wizara yake inaandaa utaratibu gani wa kuzifanyia ukaguzi kila baada ya muda?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mwenyekiti, skuli hizi za binafsi tunazifanyia ukaguzi na kama nilivyoeleza kwenye majibu yangu huwa tunazifanyia ukaguzi kabla kwenda kuangalia hali halisi, majengo yote yalivyo kama yanaridhisha. Lakini baada ya hapo huwa tunazifanyia ukaguzi kila baada ya mwaka kama vile kutizama walimu, leseni za walimu, ubora wa majengo pamoja na mambo mengine Mhe. Mwenyekiti kama hayo. *(Makofi)*

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa wizara yako ina wajibu mkubwa wa kuzitambua skuli ambazo zinaitwa *International*. Je, mpaka sasa kuna skuli ngapi ambazo zipo Zanzibar zinaitwa *International*?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mwenyekiti, mpaka hivi sasa kwa Zanzibar skuli ambazo zina sifa ya kuitwa *International School* ni skuli mbili tu. Skuli moja inaitwa *International School of Zanzibar* ipo hapa *Zanzibar Beach Resort* na skuli ya pili inaitwa *British School of Zanzibar* iko Maisara. *(Makofi)*

Nam. 214

Mafundi wa TUKUZA Kudai Fedha

Mhe. Nassor Salim Ali – Aliuliza:-

Kumekuwa na malalamiko ya wananchi ya kuwalalamikia Mafundi wa Shirika la Umeme wanaotengeneza Mita za TUKUZA kwa kudai pesa za matengenezo ya mita hizo pale zinapoharibika. Vile vile kumekuwa na malalamiko ya kuwepo vituo vichache vinavyotoa huduma ya umeme wa TUKUZA na kusababisha msongamano mkubwa wa wananchi wanaohitaji huduma hiyo.

(a) Je, ni sahihi mafundi hao kudai pesa kwa wananchi. Kama sio sahihi Wizara itawachukulia hatua mafundi hao, ili kukomesha tabia hiyo?

(b) Je, wizara ina mpango gani wa kuweka vituo vingi vya TUKUZA, ili kuondosha msongamano kwa wananchi wanapohitaji huduma hiyo?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Aliijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 214 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli sio sahihi kwa fundi yoyote kudai pesa kwa wananchi, lakini tunaomba ifahamike kwamba siku hizi kumefumka aina ya mafundi wanaodai kuwa ni mafundi wa *ZECO* na wanafanyakazi shirika na hawa ndio wanaodai fedha kwa kazi hizo. Iwapo itajitokeza kwa wale mafundi wetu wataojulikana kufanya hivyo watachukuliwa hatua za kinidhamu.

(b) Wizara yangu imeweka mpango madhubuti wa kutanua vituo vya ununuzi wa umeme Unguja na Pemba. Kwa upande wa Unguja tayari tumefungua kituo Mkokotoni na katika mwaka huu wa fedha tunaoendelea nao tumeweka Kituo Makunduchi, Bububu na Gamba. Kwa upande wa Pemba vituo vitavyoongezwa ni Konde na Mtambile.

Hata hivyo shirika lina mpango wa kuzungumza na Kampuni ya *ZANTEL*, kwa ajili ya kuanzisha huduma za ununuzi wa umeme kupitia simu za mkononi, huduma ambayo itaondoa tatizo la kutegemea vituo kwa asilimia kubwa. *(Makofi)*

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza kwa Mhe. Naibu Waziri pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri.

Ni vituo vingapi vinavyouza umeme huu wa TUKUZA kwa Unguja na Pemba?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kwa hivi sasa kwa upande wa Pemba ni Mkoani, Chakechake pamoja na Wete na vituo vyengine vinatendelea baada ya muda mdogo baada ya kwisha kumaliza mambo yetu ya bajeti. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti,

UTARATIBU

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nilisikiliza kwa makini swali alitaka kujua vituo vinavyouzwa umeme wa TUKUZA kwa Unguja na Pemba na sio Pemba peke yake na jibu lilikuja kwa Pemba tu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Naibu Waziri swali alilouliza Mhe. Mjumbe aliuliza kuhusu vituo vinavyouza umeme kwa Unguja na Pemba na wewe umejibu kwa upande wa Pemba tu na Unguja tumalizie.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Unguja ni ofisi yetu ya shirika, Michenzani, Mkokotoni na Gamba kama nilivyoeleza.

Mhe. Rashid Seif Suleimna: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri napenda nimuulize swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Kwa kuwa wateja wa *ZECO* wanalipa ile *service charge* kwa hivyo hakuna wasi wasi wowote kwamba matengenezo yameshalipiwa.

(a) Sasa je hawa wafanyakazi wanaokwenda katika nyumba wanavyo vitambulisho vyovyote, ili wananchi wawajue hawa ndio mafundi waliokusudiwa au ni mapateli?

(b) Kwa kuwa TUKUZA ni umeme ambao unatakiwa ununue baada ya muda ukimaliza na Chakechake kama alivyosema kuna kituo kimoja tu ambacho kiko mjini kwenye ofisi yao. Lakini eneo la Machomanne ni eneo kubwa sana linalounganisha karibu njia nyingi pale, kama vile njia inayokwenda Vitongoji, Wete, na kwengineko. Ni sababu zipi za msingi zilizopelekea mpaka leo ikawa pale Machomanne hakuna kituo cha kununulia umeme wa TUKUZA, ambacho kina *potential* kubwa ya watu?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Mwenyekiti,

a) kuhusu mafundi wetu kuwa na vitambulisho hili lipo na mafundi wetu wote au wafanyakazi wetu wote wa Shirika la Umeme wana vitambulisho, na yule atakayeonekana hana kitambulisho basi fundi huyo usimuamini na yuko nje ya shirika letu.

b) Kuhusu vituo vya ununuzi wa umeme ni vichache sio kwa upande wa Chake Chake tu ni Zanzibar nzima vituo hivyo ni vichache,

kwa kuliona hilo Wizara yangu ndio maana nikasema kwamba tayari tumeshafanya mazungumzo na Kampuni ya Zantel ili tupate kununua umeme kwa kupitia njia ya Mtandao.

Nam. 235

Umilikishwaji wa Nyumba za Maendeleo Kikwajuni

Mhe. Abdalla Mohammed Ali (Kny:Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa) - Aliuliza:

Miongoni mwa matunda ya Mapinduzi matukufu ya 1964 ni nyumba za Maendeleo za Kikwajuni. Watu au wakaazi waliohamia au waliolipwa nyumba hizo tokea utawala wa Rais wa Kwanza wa Zanzibar walitakiwa kupatiwa hati miliki za nyumba wanazoishi na hadi hivi sasa hawajapatiwa hati hizo.

Je, Mhe. Waziri katika hali tunayokwenda nayo hivi sasa ya utawala wa sheria ni lini wakaazi wa nyumba hizo watapatiwa hati hizo kwa kutilia maanani baadhi yao tayari wamefika mbele ya haki na huku nyuma kuna tatizo la mirathi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 235 kama ifuatavyo:-

Miongoni mwa matunda ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 ni ujenzi wa nyumba za Maendeleo Kikwajuni na sehemu nyengine mbalimbali Mijini na Vijijini Unguja na Pemba. Wananchi wengi wamebahatika kupata nafasi ya kuishi katika nyumba hizo ambapo baadhi ya wanaoishi wanadai wamepewa na marehemu Mzee Abeid Amani Karume na kuwa waishi humo na ziwe zao.

Serikali kwa kutambua kilio cha wananchi hao imeamua kuunda Kamati ya Kuwatambua wale wote wenye madai kama hayo. Kamati hiyo imeendelea na kazi ya kuyashughulikia madai hayo na iliwaita wahusika mbele ya Kamati kwa kuhojiwa na hivi sasa Kamati imo katika hatua za mwisho za kukamilisha ripoti yake. Itakapokamilika ripoti hiyo itakabidhiwa Wizarani na wale wote watakaobainika kuwa ni sahihi basi watakabidhiwa hati za Umiliki wa nyumba wanazoishi na wale ambao watabainika kuwa madai yao sio sahihi basi watatakiwa kuendelea kulipa kodi kwa mujibu wa Sheria.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza suala moja la nyongeza.

Pamoja na majibu ya Mhe. Naibu waziri tutakumbuka kuwa kamati hii imeundwa sasa huu ni zaidi ya mwaka wa tatu tangu kuundwa kweke na sesturi ya kamati inapoindwa huwa inapewa muda maalum.

a) Je, kamati hii ilipewa muda gani wa kufanya kazi.

b) Ni kiasi gani hadi sasa imetumia katika kuikamilisha kazi hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ni kweli kamati hii imeundwa kipindi kirefu, lakini nafikiri tujue kwamba huwezi kumhukumu mtu yoyote bila ya kufanya uchunguzi na kukamilisha uchunguzi, kwa hivyo utakapofanya uchunguzi na ukakamilika ni rahisi kumtolea hukumu mtu huyo. Kwa hivyo ni kweli kamati hii imechukua muda mrefu lakini bado iko katika uchunguzi na utakapomalizika uchunguzi huo basi italeta ripoti wizarani na tutachukua hatua zinazostahiki.

Kuhusu tathmini ya fedha ambayo imetumia kamati hii nitakujibu kwa maandishi.

UTARATIBU

Mhe. Omar Ali Shehe: Kwa mujibu wa kanuni zetu Waziri anatakiwa kujibu suala kwa kikamilifu, juzi nilipouliza suala kuwa ni kiasi gani walitumia kwa ajili a majanareta Mhe. Waziri aliniambia atanijibu kwa maandishi na hadi sasa hajanijibu, na sasa hivi ananambia atanijibu kwa maandishi.

Mhe. Mwenyekiti: Kipo kifungu kinachoelekeza hivyo.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti nashkuru na mimi kunipatia nafasi hii kuuliza suali moja la nyongea.

Kama alivyoeleza kwamba kamati hii imeundwa kuchunguza na kwa kuwa si nyumba hizo tu ni nyumba nyingi ambazo zinadai hivyo na kwa kuwa zina baadhi ya majengo ambayo Wizara yenyewe ilisema kwamba kutokana na sheria iliyopitishwa hapa wauziwe wananchi.

Je, suala la Mazizini mabanda ya magari yaliyokuwa ya tokea enzi na wananchi wa Mazizini waliomba kwa utaratibu na sheria na wakaambiwa wajitayarishe kuuziwa mpaka bei, kuenzia jana wamekwenda watu kuwaambia kwamba

wajitayarishe kuhama. Je, suala hili Wizara yako inalijua na kama inalijua ni taratibu zipi za kisheria kwa sababu wameshatoa muongozo wizara yako.

Mhe. Naibu Waziri, Ardhi, Makaazi, Maji na NIshata: Kwanza nathubutu kusema wizara yangu taarifa hiyo haina na utaratibu wa kuwauzia nyumba wananchi huo bado tunao na unaendelea. Lakini taarifa za kuhamishwa wananchi wa Mazizini hiyo taarifa wizara yangu haina.

Nam. 220

Udhalilishaji na Ukosefu Mashine ya Dna:

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa – Aliuliza:-

Kumekuwa na wimbi la vitendo vya ubakaji sambamba na tabia ya baadhi ya akinababa kuwanyanyasa wakuu wenzao na kuwakataa watoto kwa mdai ya kwamba hawahusiki na ujauzito wanaowapa. Jitihada kubwa zimekuwa zikichukuliwa na Taasisi mbali mbali ili kukabiliana na tatizo hilo; lakini juhudi zao zimekuwa zikikwama kutokana na kukosekana kwa mashine ya kuchunguza viasili (*DNA*).

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kununua mashine ya *DNA* hapa Zanzibar.

(b) Katika kipindi hiki ambacho mashine hiyo haipo ni utaratibu gani unaotumika kuyapatia ufumbuzi matatizo hayo ya ubakaji na utelekezaji wa watoto.

(c) Kuna madai kwamba kuna baadhi ya askari wa kike wa jeshi la Polisi wasiowaaminifu wameanzisha mbinu za kupoteza fomu za *PF3* ili kuharibu ushahidi kwa watuhumiwa wa ubakaji, Je, kuna ukweli gani katika madai hayo. Kama ni kweli Wizara ya Afya imejipanga vipi kukabiliana na mbinu hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako ninaomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suali lake Nam. 220 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika,

(a) Kama tulivyojibu suala Nam. 133 kwamba Serikali ina mpango wa kuinunua mashine hiyo. Hatua za awali za

kufanya uchambuzi yakinifu umeshafanyika, pia serikali imeshatafuta majengo hapo Maruhubi na sasa hivi matengenezo yanaendelea

(b) ili kuyapatia mfumbuzi matatizo ya ubakaji, kituo cha *one stop center* kimefunguliwa katika hospitali ya Mnazi mmoja na huduma ya Daktari, polisi na Mwanasheria zinapatikana hapo kwa wakati mmoja. Pindipo jambo kama hilo likatokea na likathibitishwa, na mtuhumiwa akakamatwa, sheria inaachukua mkondo wake.

(c) Tabia hiyo ilikuwepo kwa askari wote wa kike na wa kiume. Kama askari akiripoti amepoteza *PF3*, inabidi Mkuu wa Polisi aandike barua yenye muhuri wa kituo na kuomba *copy PF3* kwa Mkurugenzi wa hospitali ya Mnazi mmoja. Baada ya hatua hiyo kuchukuliwa tatizo hilo hivi sasa limeonekana kupungua.

Mhe. Jaku Khashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri huoni kwamba kukosekana kwa umeme katika hospitali yako kunaendelea mpaka muda huu na huwezi kuona kwamba kutokuwepo kwa umeme kunaweza kupoteza ushahidi wa kesi hizo.

Je, Wizara yako imejipangaje kwa suala hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Naomba kukataa suala hili kwa sababu halina mahusiano na masuala ya jibu mama.

Mhe. Amina Iddi Mbarouk: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri nayomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri tunakujua katika baraza hili tukufu kuwa unaumia sana jinsi gani ya udhalilishaji wa watoto wetu. Je, Mhe. Waziri hebu twambie hasa katika baraza letu hili tukufu ni lini kifaa hichi kitakuwa kimefika hapa Zanzibar ili kiweze kuwashughulikia na kuwasaidia watoto wetu wale ambao wanadhalilishwa.

Mhe. Naibu Waziri Maendeleo ya Wanawake Vijana na Watoto: Mhe. Mwenyekiti kwanza nashukuru kwa kunipatia nafasi hii lakini pia Mhe. Mwenyekiti naomba kuongeza majibu baada ya yale aliyotoa Mhe. Naibu Waziri wa Afya, naomba niongezee kwamba kifaa hichi cha DNA naomba

niwaambie wajumbe kwamba ghali sana si rahisi.

Lakini jengine ni kwamba serikali tumeshaiarifu kuhusu suala hili la kuona umuhimu wa kupata chombo hichi na imekubali, lakini pia hata hawa wahisani wetu pia wanaonyesha kwamba wapo tayari kushirikiana na sisi katika kukipata chombo hiki, kwa hivyo nawaomba wajumbe wawe wastahamilifu kidogo tutafute pesa tubembeleze kwa watu wetu ili chombo hichi kipatikane na tuwaadhirishe watu. Maana ikibidi mtu ameshakataa mimba hii sio yangu kumbe ni yake anajua lakini anamdhalilisha yule mtoto, kwa hivyo kikipatikana chombo hiki hana pa kujikimbiza naomba niongezee hilo Mhe. Mwenyekiti.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kifungu Nam. 37 Kanuni Waziri au mjumbe yoyote anayeulizwa suali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu suali hilo kwa ukamilifu isipokuwa kwamba suali aliloulizwa Waziri moja linaweza kujibiwa na mawaziri au Mwanasheria Mkuu.

Nilichouliza mimi Mhe. Mwenyekiti, kukosekana kwa umeme katika hospitali ile hakutopoteza ushahidi wa watoto

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe kifungu Namba 37 ngapi umesoma.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kifungu namba 37(1) nilichouliza mimi kukosekana kwa umeme katika hospitali ya Mnazi Mmoja hakutoweza kupoteza ushahidi katika kesi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Tunapozungumzia *One Stop Center* tunazungumzia watu sio mimi kama daktari atakuwepo, kama polisi yupo, kama mwanasheria yupo hao ndio wanaothibitisha hilo tatizo na kama umeme unazimika, sijawahi kuona Mnazi Mmoja kucha nzima ikazimika umeme sana itakuwa kwa dakika na tangu siku hiyo uliposema kwamba umeme umezimika watu wapo. Kwa hivyo umeme unapozimika sio lazima uwake hapo hapo hatuna *Automatic generator* pale fundi anakwenda anawasha umeme.

Labda kwa bahati mbaya hapo kila siku unapokwenda wewe umeme unazimika, siku nyengine umeme hauzimiki, lakini pia napenda niongeze kama mimi nilivyosema na Waziri wetu alivyosema suala la *DNA* ni suala ambalo linazungumzwa na linafanyiwa kazi na wizara zetu hizi, kwa sababu tunaohusika ni wengi wanawake na watoto, sisi afya, polisi na *UNICEF* wametukubalia kwamba hili watashirikiana na sisi. Kwa hivyo tuna uhakika

kwamba mashine ya *DNA* itakuja.

Lakini kabla haijaja lazima maandalizi yawepo na ndio maana sasa hivi ikawa kunatayarishwa nyumba hiyo ambayo Mkemia Mkuu atakuja kuifanyia kazi, itakapokamilika ndio utaratibu wa kuiweka hiyio mashine itakapoletwa, kwa hivyo ni vitu ambavyo vinahitaji maandalizi, sote tunaumwa mimi sipendi, nyie mliopo hapa hampendi mtu yoyote kudhalilishwa, kwa hivyo tustahamili maandalizi yaje tutakapokuwa tayari mashine itawekwa katika sehemu inayohusika na kazi itafanya.

HOJA SA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumzi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012

Wizara ya Mifugo na Uvuvi

(*Majadiliano yanaendelea)*

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujaalia kukutana hapa katika baraza tukufu tukiwa tuko ndani ya hali ya afya njema, lakini pia nikushukuru na wewe Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii asubuhi hii kuchangia na mimi machache katika hotuba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Waziri kwa kutuletea kitabu chake hichi cha bajeti ambachokuwa kimejaa matumaini na mafanikio ya Wazanzibari kwa ujumle. Mimi nikianza niende kwenye sekta hii ya uvuvi ambayo kuwa kuna mafanikio mengi aliyoeleza Mhe. Waziri ambalo moja ambalokuwa na pasa nilizungumze hapa ni ujenzi wa soko hili la Tumbe, kwanza niishukuru serikali ya Mapinduzi kwa ujumla lakini pia nimshukuru Mhe. Waziri na Wizara yake kwa uamuzi huu aliouchukua kwa kutujengea soko hili la samaki lililoko Tumbe, natoa shukurani sana na nikijua kwamba soko hili litawapa faraja wavuvi wengi wanaokuja kuvua maeneo ya Tumbe.

Mhe. Mwenyekiti, wavuvu wengi wanakuja kuvua maeneo ya Tumbe na wala sio watu wa Tumbe peke yao wanakuja kutoka vijiji mbali mbali kuja kuvua pale, vikiwemo vijiji vya Kojani, watu wa msuka kuweka madago katika kijiji kile cha Tumbe katika kutafuta rizki, kwa kiasi fulani wavuvi wale wanafanikiwa kukamata samaki wengi sana katika bahari ile, lakini hufikia pahali wanapokuja kuvua samaki wao kwa wingi basi huja wakawauza pale au wakawachukua kwenye magari na kuwapeleka kwenye masoko ya mjini kama Chake na Wete kwa kuwauza kwa bei iliyokuwa haikidhi haja, kutokana na kuwa hakuna maeneo ya kuhifadhi samaki wale.

Sasa naamini kwamba ujenzi huu wa soko utajumuisha pia isiwe ni soko tu lililokuwa ni banda lakini liwe ni soko ambalokuwa litakuwa na maghala ya kuhifadhia samaki wale watu wanapocherewa kurudi baharini ili wenyewe waweze kuuza siku ya pili kwa bei iliyokuwa ina tija nzuri. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti nitamuomba Mhe. Waziri atakapokuja kwenye majumuisho yake anieleze kuwa soko hili linalojengwa litakidhi haja hii au ni soko tu ambalo kuwa halitoleta maslahi kwa wavuvi hao wanaovua maeneo hayo.

Jengine Mhe. Mwenyekiti nije katika ukulima wa mwani, wakulima wa mwani katika Wilaya ya Micheweni ni wengi tu na hususan akina mama kama atunavyojua Mhe. Mwenyekiti, wananchi wetu wanapenda sana mambo ya kujiajiri wenyewe kwa sababu hakuna ajira ndani ya serikali lakini hufikia pahali wakati mwengine ikawa ajira zao hazina maana kutokana na kuwa hawapati masoko. Kwa mfano wakulima hawa wa mwani siku nyingi zinazopita wamekuwa na kilio cha bei hafifu iliyoko kwa ununuzi huu wa mwani na katika Wilaya ya Micheweni walipelekea mpaka kufika kugoma kuuza mwani wao kutokana na kuwa bei inayonunuliwa haikidhi, lakini nashukuru Mhe. Waziri juzi hapa alipokuwa akijibu suala lake alisema kumetokea mnunuaji mmoja wa mwani ambae kuwa aliyekuwa akinunua mwani huo kwa shs. 250 na yeye kuununua kwa Shs. 400 kwa kilo, nashukuru kwa hilo na naomba Mwenyezi Mungu atujaalie mnunuzi huyo ampe maisha marefu ili kunufaisha wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini wavuvi hao hao wa mwani serikali pia nayo ipo haja ya kuwasaidia ya kuwaonea huruma kutokana na kazi nzito wanayoifanya juu ya kuwa wameshaongezewa kilo Shs. 400, lakini serikali nayo ina haja ya kuwaongezea maslahi zaidi wakulima wale kwa kuwapatia vifaa, kama vile kamba, taitai, na bodi za kuchukulia mwani. Kwa sababu kuna mwanamke mmoja katika kijiji chetu cha Tumbe alifika hadi kutaka kufa maji kwa kuvuka kwenye kidau, kwa sababu maeneo watu wanayolima mwani wanakuwa wanavuka visiwa. KIwa hivyo naomba Mhe. Waziri alione hilo ili kuwasaidia wananchi kupata kamba na tai tai kwa ajili ya kuendeleza kazi yao.

Lakini jengine Mhe. waziri kwenye mifugo nataka nimhakikishie Mhe. Waziri kuwa katika ufugaji wa mbuzi Wilaya ya Micheweni inaongoza na niwafugaji wenye uwezo hasa wa kufuga mbuzi, sasa Mhe. Waziri alisema jana hapa kwamba kuna mbuzi ambao kuwa wanazaa watoto watatu watatu na kutoa maziwa lita sita mpaka nane, mimi naona bado katika ufugaji wa mbuzi suala la mbuzi kuzaa watoto watatu halijafika katika wilaya yangu kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri kupitia Wilaya ya Micheweni aje kufanya utafiti huu na kuunda vikundi kule. Naamini atakapokuja kuwawezesha wafugaji wa mbuzi wilaya ya Micheweni basi nadhani hawatotaka ajira nyengine, kwa hivyo namuomba sana na hili nalo alizingatie.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache mimi sina mengi nampongeza sana Mhe. Waziri, kwa niaba yangu na wanawake wa Wilaya ya Micheweni naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa wajumbe orodha yetu tuliyokuwa nayo ni kubwa sana kuna watu 19 ambao wanataka kuchangia, kwa hivyo ningeomba basi tugawani kila mmoja japo dakika kumi kumi ili wengi tuweze kuchangia, lakini pia yale mambo ambayo yameshazungumziwa tuzungumze mbadala wake.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba ya Mhe. waziri wangu wa Uvuvi na Mifugo, pia nawapongeza wafanyakazi wa wizara yake kwa juhudi kubwa na wakakitunga kitabu hiki kwa upole na maarifa makubwa.

Mhe. Mwenyekiti kwa kuchunga wakati wetu huu mimi nitaanza hii sekta ya uvuvi kwa sababu mimi ni mtu wa pwani, sasa nitazungumza kwa vile na mimi ni mvuvi. Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu ya Zanzibar imezungurukwa na bahari pande zote na Zanzibar wavuvi asilimia thamanini au tisini ni wavuvi na jimbo langu la Matemwe ni asilimia tisini ni wavuvi na wakulima. Kwa hivyo tegemeo lao kuba ni uvuvi, sasa uvuvi wetu tunaovua kule ni uvuvi wa kimasikini uende pale ukaweke wavu upate samaki watano sita saba mpaka kumi ukauze shilingi elfu moja hazikidhi haja na uvuvi wenyewe ni huo huo unaoitwa haramu, kwa sababu uvuvi wote tuliozoea sisi ni uvuvi haramu na hivi sasa unapigwa vita ili kuhifadhi mazingira.

Sasa mimi naiomba serikali kwa kushirikiana na wizara yetu hii kwamba wananchi wawezeshwe vifaa vile ambavyo vinafaa katika kuvua, wananchi wetu hawana vifaa uvuvi wenyewe ndio huo huo wa kwenda kutwa upate samaki watatu Kwa hivyo, naiomba serikali pamoja na Wizara yetu ya Mifugo na Uvuvi iwaletee wananchi zana za kuvua za halali. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu tatizo kubwa ni kwamba wananchi hawana zana hivyo serikali ijiimarishe ili wananchi wapatiwe zana, wakipatiwa zana basi uvuvi haramu utaondoka.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende katika mifugo ni kwamba wananchi wetu hivi sasa wengi wao sasa hivi wanakwenda katika sekta ya mifugo, lakini mifugo inayoletwa haikidhi haja. Mhe. Mwenyekiti, Jimbo langu la Matemwe lina mifugo, lakini watu 20 wanaletewa mbuzi 3. Kwa hivyo, watu hawa 20 watafuga miaka mingapi hata waondokane na huo umasikini. Kwa hivyo, naiomba wizara ifanye jitihada iwaletee wananchi mbuzi wa kukidhi haja, basi angalau waletewe mbuzi 10 wa maziwa ikifika miaka 3 watu wale watajihisi

kwamba wamefuga. Kwa hivyo, naiomba serikali iongeze mifugo kwa wananchi, wananchi 20 angalau waletewe mbuzi 10 au mbuzi 20 ndio wataweza kujijua kama wamefuga. Mhe. Mwenyekiti, mimi naiomba serikali pamoja na wizara iongeze mifugo, tena mifugo hii waidhinishwe na iletwe mifugo bora.

Mhe. Mwenyekiti, watu wetu bado hawajakuwa na elimu ya mifugo kwa hiyo wakiletewa mifugo waidhinishiwe na madawa kwani wakati mwengine mbuzi wanakufa kwa kuwa hawana madawa, na pia watu wetu hawana elimu nzuri ya kuchunga. Mhe. Mwenyekiti, utamkuta mbuzi hakogeshwi, hapakwi dawa huyo kweli atakuwa mbuzi mzuri. Mhe. Mwenyekiti, naiomba serikali pamoja na wizara yetu iwahudumie wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika sekta ya mwani naipongeza serikali kuwaongezea wananchi kipato cha mwani kutoka shilingi 200 kwenda hadi shilingi 400, naipongeza serikali. Mhe. Mwenyekiti, tatizo kubwa la wananchi wanaolima mwani huwa uanikaji wa mwani hawana kwani ardi ya pwani yote imeshajengwa mahoteli mpaka fukweni hivyo wataanikia wapi mwani huu? Mhe. Mwenyekiti, wananchi wanahimizwa wafunge mwani lakini ardhi imeshauzwa na mwani unaanikiwa sehemu za pembezoni mwa bahari, na mle pembezoni mwa bahari mmeshajengwa hivyo mwani huu utaanikwa wapi? Mhe. Mwenyekiti, naiomba serikali iangalie vizuri wawekezaji wanajenga mahoteli mpaka fukweni, mle fukweni mlimoambiwa kwamba watu wapite mita 30 hizo mita 30 haziwekwi zinajengwa, hivyo mwani huu utaanikiwa wapi.

Kwa hivyo, naiomba serikali pamoja na Wizara ya Ardhi waliangalie hili kwani wizara hii inawapimia wawekezaji mpaka fukweni bila ya uangalifu wowote. Mhe. Mwenyekiti, matatizo makubwa sasa hivi yanatupata katika ardhi kwa kuwa wawekezaji wanaruhusika kujenga katika fukwe. Kwa hivyo, mimi naomba hili liangaliwe kwa makini sana kwani mwani hauna sehemu ya kuanikwa utakuwa unawekwa baharini, lakini sehemu ya kuanikwa hamna. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mwananchi akitoka pale baharini hawezi kuuchukua mwani mpaka nyumbani kwake hasa kama kule kwetu Matemwe ardhi yake ni mawe. Kwa hivyo, serikali iangalie wakati inapouza ardhi yake ihakikishe kuna wananchi watapata tabu sana.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kwamba kule kwetu kuna sehemu inaitwa Hifadhi ya Mnemba ijapokuwa kwenye kitabu hiki hamna lakini iko kule na nitaielezea. Mhe. Mwenyekiti, Mnemba kuna sehemu moja ya hifadhi na hifadhi hii huko nyuma iliambiwa kwamba mapato ya pale watapata wananchi, lakini lalamiko kwa wananchi ambao ni wavuvi wa Matemwe kwa muda wa miaka 15 mapato ya hifadhi ile hawajapata.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri alishughulikie jambo hili kuhusu hifadhi ya Mnemba kwa wananchi wa Matemwe kwa sababu pale tegemeo lao kubwa na wao wapate hisa ili wapate kuendesha maendeleo yao, lakini kwa muda wa miaka 15 walipewa milioni moja moja ambayo ni sehemu inayotumia shehia nne. Shehia ya Nungwi, Pwani Mchangani, Kijini na Matemwe yenyewe lakini mapato haya hayajapatikana, hivyo wananchi wa Matemwe wana kilio cha Hifadhi ya Mnemba. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri hili jambo alifuatilie ili lipate uamuzi kutokana na wale wananchi wa Matemwe ili wapate mapato waweze kuendeleza maendeleo yao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa ilivyokuwa mimi ni mvuvi na natokana na wavuvi kwa hivyo wavuvi wanapata shida ya vifaa vya kuvulia uvuvi halali hakuna. Kwa hivyo, serikali ikishirikiana na wizara iwatafutie wananchi wanaovua uvuvi wa halali vile vifaa ambavyo vinatakikana kwani wanapata shinda. Mhe. Mwenyekiti, matatizo makubwa sasa hivi ni ugomvi mkubwa baina ya serikali na wavuvi ni kwamba vifaa vya halali hakuna, wanatumia mshale, mangu, wavu ule wa macho madogo na madema yao.

Kwa hivyo, sasa serikali iamue kuwawezesha kwa kuwapatia maboti, nakumbuka maboti huwa yanaletwa lakini huwa wanayakumba wenyewe wakubwa. Nakumbuka mwaka jana niliona maboti yameletwa kule Pwani Mchangani mengi sana, sisi tukizania yale maboti ni ya wananchi lakini maboti yale kule Matemwe hatuyaoni tena hata sijui yamekwenda wapi. Kwa hivyo, wananchi wapatiwe vifaa vya uhakika wawe wanavua vizuri na wawe wanapata mapato angalau ya kukidhi haja zao.

Mhe. Mwenyekiti, ikiwa ndio wananchi wanaambiwa msivuo uvuvi na huku hakuna zana ambayo ya kuvulia mwananchi huyo atafanya nini na watu wa Unguja sisi tunazaa sana. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba mtu mmoja ana watoto kumi, wanne ndio analalamika huyu Mungu hakunipa watoto mimi. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hili tulitizame sana kwani wananchi wetu ni masikini, wananchi wetu kazi yao ni bahari na ukulima. Kwa hivyo, tuwawezeshe halafu ndio tuwatungie sheria, bila ya kuwawezesha sheria itakuwa haisimami, hebu tujaribu sisi Waheshimiwa wa Baraza la Wawakilishi tuambiwe fanyeni imani miezi minne mishahara yetu muitie katika mfuko wa walemavu, msipewe nyinyi wawakilishi, kweli tutakubali, ni kwamba hatukubali. Kwa hivyo, na wananchi nao kama hawakuwezeshwa wakapewa vifaa basi tutapata tabu, hivyo naomba tuwawezeshe wananchi sheria itungwe na wananchi wawezeshwe, bila ya kuwezeshwa wananchi sheria itakuwa haisimamia.

Mhe. Mwenyekiti, mwananchi wa Matemwe hana kiwanda hakuna hata ile ofisi ya serikali, ofisi yao ya serikali asubuhi wakiamka wao wanakimbilia

pwani. Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano ukimkamata mwananchi wa Matemwe asiende pwani basi hatakubali atakwambia labda ukanipe chakula na watoto wangu, na wewe mwenyewe huna.

Kwa hivyo, Mhe, Mwenyekiti, kwa kuchunga wakati mimi naipongeza hotuba ya Mhe. Waziri na naunga mkono hotuba hii mia kwa mia, ahsante sana.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Vile vile naomba nimpongeze Mhe Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa hotuba yake jinsi alivyoisoma.

Mhe. Mwenyekiti, wafugaji wa nchi yetu wana matatizo mengi na nayasema haya kwa sababu mimi mwenyewe ni mfugaji kwa muda wa miaka 16. Matatizo ya wafugaji moja ni kuhusu ughali wa chakula na madawa kwa hiyo naiomba Wizara ya Mifugo na Uvuvi iandae utaratibu maalum wa kutoa fidia kwa chakula cha mifugo na madawa.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo jengine ni wafugaji kukosa huduma ya kitaalamu mara kwa mara na hii sababu tunayopewa ni uhaba wa vyombo vya usafiri kwa wataalamu na pia uhaba wa hao wataalamu wenyewe. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri anipe maelezo ni lini atawapatia usafiri wataalamu waliopo na lini atawapa mafunzo wataalamu hao na vile vile ni lini ataajiri wataalamu wapya kwa wizara hiyo?

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu maabara iliyop Wilaya ya Chake Chake ni muhimu kwa wafugaji wa Chake Chake, hivyo basi nampongeza sana Mhe. Waziri kwa kuifanyia matengenezo maabara hiyo. Mhe. Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Mhe. Waziri ni kwamba maabara hiyo itakapokamilika matengenezo yake ahakikishe kuwe na vifaa vya maabara na pia awapatie nafasi za kujiendeleza wafanyakazi waliopo katika maabara hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile wizara hii ilijenga soko kubwa na zuri na la kileo katika kijiji cha Mvumoni, lakini jambo la kusikitisha ni kwamba licha ya uzuri wa soko hilo linaonekana halitumiwi ipasavyo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri anieleze ni kwa nini soko hilo halitumiki na vile vile je haoni kutotumika kwa soko hilo ni kupoteza fedha za umma bure.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi awasaidia sana wananchi walioko katika vikundi vya mifugo kwa sababu wafugaji ni watu wanaopenda kujituma. Kwa hivyo, bila shaka wakiwawezesha wafugaji hawa serikali itapata mafanikio makubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huo kwa niaba ya wanawake wa Wilaya ya Chake Chake naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi hii kuweza kuchangia Bajeti hii ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kwa leo sina mchango mkubwa sana kwa sababu wenzangu wengi wameshazungumzia tatizo hilo hilo kila wakati kwamba tuna matatizo ya kupata vyombo vya uvuvi. Lakini hata hivyo niongezee kuzungumzia kuwa tatizo la vyombo vya uvuvi lipo kwa sababu hivi sasa nchi yetu ina matatizo sana kwani wavuvi wetu vyombo vyao ni vidogo sana.

Mhe. Mwenyekiti, zaidi nimpongeze Mhe. Waziri hivi juzi tulikuwa na semina alituzungumzia sana kuhusu masuala ya uvuvi vipi ataokoa suala la uvuvi ili vyombo viweze kupatikana na kuweza kufika bahari kuu. Kwa hivyo, nimpongeze sana Mhe. Waziri kama hilo suala amezungumza kwa dhati kwamba mwaka huu atawezesha angalau kila Wilaya moja kupata boti moja ya kisasa ambayo ina uwezo wa kuchukua 200 kwenda bahari kuu, mimi nafikiri tatizo hili la wavuvi litaondoka kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimpongeze zaidi Mhe. Waziri kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Kati Jimbo la Koani tulipokwenda Uzi alizungumzia tena hili suala la kuwa atapeleka chombo kikubwa huko Uzi Ng'ambwa kwa ajili ya suala hili hili la uvuvi. Kwa hivyo, nampa hongera sana kwamba hili suala ameliweka mbele na nategemea atalizingatia na atalichukulia hatua suala hili la uvuvi. Kwa vile wenzangu wameshazungumza sana suala hili na muhimu ni kupata vyombo ili kuweza kufika bahari kuu, mimi suala hili sitolizungumzia sana isipokuwa nitazungumzia suala la ufugaji.

Mhe. Mwenyekiti, suala la ufugaji wananchi wetu wanataka kufuga kama inavyotaka serikali, lakini tatizo ni kwamba uwezo wao ni mdogo sana wa kuweza kupata ng'ombe wa kisasa. Kama ng'ombe wa kisasa hawawezi kupata basi hawataweza kufuga wananchi wetu, isipokuwa serikali ijidhatiti kuweza kuwapatia wananchi mkopo mkubwa sio wa fedha, lakini ipate angalau mkopo wa ng'ombe wenyewe wa kisasa kwa kila Wilaya wahakikishe wanakwenda japo ng'ombe 100 wa kisasa wapewe wananchi ili wajiwezeshe kimaisha.

Mhe. Mwenyekiti, kama sio hivyo itakuwa ni ndoto kusema kuwa tunataka ufugaji wa kisasa au tunataka ng'ombe wa maziwa wa lita 20 kwa ng'ombe au mbuzi wa lita 6 itakuwa ni ndoto kama wananchi hawakuwezeshwa. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri awawezeshe wafugaji kwa kuwapatia mkopo wa ng'ombe na wanyama wengine kama mbuzi ili waweze kujiendeleza katika Mikoa yetu pamoja na Wilaya zetu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende katika suala la mwani, ni kwamba hivi sasa suala la mwani ni matatizo makubwa kwa wananchi kwani bei ya mwani ni ndogo sana. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri tuanze kutoka nje kama tulivyotoka kutafuta zao la karafuu na kupata bei nzuri, basi sasa hivi ipo haja Mhe. Waziri achukue na ma-*backbenchers* wa Baraza hili kwenda nchi za nje kutafuta bei hasa sio bei ya shilingi 400. Mhe. Mwenyekiti, bei ya shilingi 400 haiendi na wakati twende nje kama tulivyoweza kwenda kutafuta bei ya zao la karafuu basi tunao uwezo wa kwenda kutafua bei ya zao la mwani. Mhe. Mwenyekiti, huko najua wananchi wetu wanaweza wakashukuru sana badala ya kuuza kwa shilingi 400 wakaja wahusika wakanunua kwa dola wakafaidika wananchi wetu wa kipato cha chini.

Mhe. Mwenyekiti, zaidi ya hayo kwa leo sina mchango mwingi kwa sababu muda wenyewe ni mdogo na watu wengi tunataka kuchangia. Mhe. Mwenyekiti, mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Koani tunaunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi asubuhi hii. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kufika hapa katika Baraza hili tukufu nikiwa na afya njema. Pili nimpongeze Mhe. Waziri jinsi alivyoitoa bajeti yake hii muhimu na makini yenye kuleta matumaini kwa wa Zanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze na mchango wangu moja kwa moja kwenye suala la mifugo na nitauelekeza mchango wangu ndani ya Wilaya ya Wete. Mhe. Mwenyekiti, Wilaya ya Wete ni miongoni mwa eneo lenye fursa nyingi za uendelezaji wa mifugo, lakini kwa bahati mbaya hakuna uimarishwaji wa mifugo hiyo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atwambie ana mkakati gani juu ya uendelezwaji wa mifugo katika Wilaya hii.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba nijue hatma ya kuhusiana na mambo mawili muhimu. Jambo la kwanza ni kuhusiana na shamba la mifugo lililopo Chamanangwe Wilaya ya Wete Jimbo la Ole. Mhe. Mwenyekiti, shamba hili limetupwa kwa muda mrefu, haliulizwi, halileti tija wala halizalishi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atwambie kuhusu hili ana mkakati gani wa kuliendeleza shamba hilo.

Mhe. Mwenyekiti, pili anieleze juu ya eneo la ofisi ya mifugo liliopo eneo la Ole, eneo hilo Mhe. Waziri lina vyumba na madarasa ya kulala wanafunzi. Kwa hivyo, kwanza naomba nikuulize suala Mhe. Waziri wewe unalijua eneo hilo na umeshawahi kwenda pahala hapo na kama umewahi kwenda kuna mkakati gani wa kuendeleza sehemu hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, maeneo muhimu mawili niliyoyataja hapa ni maeneo ya muda mrefu yaliyokuwa yakitumika kwa sababu ya mifugo na yalikuwa yakileta tija sana, na yalileta maslahi mengi kwa taifa hili. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nataka nikwambie kwamba hatuna tabia ya kuendeleza miradi inapomalizika serikali au wizara haiendelezi miradi ile. Mhe. Mwenyekiti, miradi ile ilikuwa mizuri, imetumika kwa muda mrefu na kila mmoja nafikiri alikuwa anapata tija kutokana na miradi ile iliyokuwepo pale. Kwa hiyo maeneo yale ni muhimu namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atupe ufafanuzi wa kina juu ya maeneo mawili hayo, moja likiwa pale Ole kwenye Ofisi za Mifugo na moja likiwepo Chamanangwe shamba kubwa lenye tija nyingi na lina eneo kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niipongeze sana wizara hii kwa kutafua nafasi kwa wananchi kuwapeleka masomoni kwenda kusoma juu ya mazao ya baharini. Lakini naomba nimwambie Mhe. Waziri katika jimbo langu la Ole eneo la Kangagani kuna shamba kubwa sana tena zuri la wafugaji wa samaki. Mhe. Mwenyekiti, katika utafiti wangu nimefuatilia nikaona wao hawajapata hii fursa ya kwenda kusoma kama wenzao walivyopata fursa hizo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atwambie ni lini kikundi hiki chenye wakulima wa mazao ya baharini ya kufuga samaki watapata na wao fursa hii ya kwenda kujifunza kama vile wenzao walivyopata nafasi ya kwenda kujifunza ili kujiendeleza na maisha.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niingie katika sekta ya mifugo ya kuku. Ni kwamba wanawake wengi wa Zanzibar wanajiimarisha na wanahamasika na mifugo ya kuku wa kisasa. Lakini tatizo linalowakwa wananchi hawa hasa akina mama ni bei ya chakula na dawa. Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri atumie jitihada zake zote za kuwaonea huruma wajasiri amali hao ili yale madawa na vyakula yawe ya bei nafuu wapate kujiendeleza kimaisha, kwani serikali inapiga kelele kila wakati watu wajiajiri wenyewe. Mhe. Mwenyekiti, wananchi wetu wako tayari kujiajiri lakini nyenzo zinakuwa ngumu, madawa yanakuwa bei ghali na vyakula halikadhalika vinakuwa ni ghali sana vyakula vya kuku. Kwa maana hiyo Mhe. Waziri utakapowasaidia hawa wanawake kuwanyanyua kimaisha itakuwa serikali imepiga hatua yakuwasaidia wananchi wake ambao ni lengo kuu la serikali kuwasaidia wananchi wa nchi hii hasa akina mama na watoto.

Mhe. Mwenyekiti, nikija kwenye suala la uvuvi ingawaje watu wengi wameshalizungumzia. Mhe. Mwenyekiti, uvuvi ni sekta muhimu katika nchi yetu na sote ni watu tunaotoka ndani ya visiwa, hivyo wavuvi wetu naomba nikubali kwamba ni kweli katika kipindi cha karibuni samaki wanavuliwa kwa wingi mno. Lakini sasa kuna matatizo mawili makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo la kwanza hawa samaki wanakuwa na bei ghali sana. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atwambie ana mkakati gani wakufanya wizara yake ili hawa samaki wawe na bei nafuu kila mwananchi wa nchi hii na yeye apate kula ili apate afya njema, kwa sababu suala la samaki ndio unapata afya nzuri na unapata siha na ndio unapopata nguvu za kufanyia kazi katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala la pili ni kwamba samaki hawa wanapovuliwa kwa wingi watu wanakosa lile eneo la kuhifadhia samaki. Kwa hivyo, namuoma Mhe. Waziri ajaribu kufanya mipango yake yote na kwa juhudi zake zote anazozijua yeye na Mwenyezi Mungu atamsaidia kutayarisha ghala za samaki ili kunusuru wale samaki watakaovuliwa kwa wingi wasiharibike na kuleta hasara kwa wavuvi na serikali kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile wachangiaji ni wengi na leo ni siku ya Ijumaa kwa niaba yangu binafsi na wanawake wa Wilaya ya Wete naunga mkono hoja asilimia mia moja.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi niweze kuchangia katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri kwa kutuwasilishia mpango wake huu wa hotuba hii ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa wizara yake hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze kwenye ukurasa wa 14 Idara ya Mipango na Utafiti. Mhe. Mwenyekiti, katika idara hii ameeleza majukumu ya idara, mimi nasogea kwenye ukurasa wa 15 kuhusu utekelezaji wa malengo ya mwaka 2010/2011 ameeleza hapa katika kifungu cha (b) kwamba idara imeandaa mapendekezo ya miradi ya miundombinu ya uvuvi na mifugo anasema uchambuzi yakinifu, ufugaji wa samaki, viwanda vya ukaushaji wa dagaa pamoja na programu ya kuwaendeleza wavuvi Zanzibar na kuziwasilisha serikalini na washirika wa maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka kujua huu mpango kazi hasa katika suala zima la viwanda vya ukaushaji wa dagaa, maana mimi katika jimbo langu nina uanikaji wa dagaa wengi pale, lakini sijaona hivyo viwanda kufika pale kwangu wala huo mpango sijawahi kuusikia pamoja na maendeleo ya wavuvi wadogo wadogo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho anisaidie huu mpango kazi wake katika suala zima la viwanda vya ukaushaji wa dagaa pamoja na ule mpango kazi wa kuwaendeleza wavuvi wadogo wadogo, ili na mimi wananchi wangu waweze kujua hilo na tuone namna gani tunaweza tukawasaidia katika hilo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije kwenye ukurasa wa 17 kwenye Idara ya Uendeshaji na Utumishi amezungumza hapa Mhe. Waziri majukumu ya idara hii ni kutunza mali za serikali zinazomilikiwa na wizara, kufuatilia upatikanaji wa hatimiliki kwa maeneo yote ya serikali yanayomilikiwa na wizara na mambo mengine. Mimi nilikuwa nataka kujua tu Mhe. Waziri katika kufuatilia hili kwenye wizara yako kuna majengo mangapi umeshapata hati, na yale ambayo hujapata mategemeo kupata ni lini.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuna suala zima hapa la gari, kulikuwa kuna gari moja ilinunuliwa na Idara ya Uvuvi, nafikiri kwenye mambo ya *MACEMP for tuner* ambayo alikuwa akitumia Mhe. Waziri wa Kilimo kipindi kile Mhe. Buruhani Saadat Haji ileleta utata katika manunuzi yake na watu wa *World Bank*. Nafikiri ilinunua kwa karibu ya US$ 40,000 katika Kampuni ya *Zenji motors* hapa. Hebu suala hili twambie Mhe. Waziri limefikia wapi, kwa sababu wale jamaa wa World Bank walikataa zile pesa kutumika na ilibidi Serikali ya Mapinduzi iingie hasara ya kugharamika kuzilipia zile pesa, kwa sababu wao walizikataa kutoa kwa hivyo SMZ ilizilipa zile pesa. Mimi nataka kujua ni hatua fani zilichukuliwa kwa wale ambao walisababisha upotevu ule au hasara ile kwa serikali. Kwa sababu zile fedha zilizotumika ni za walipoa kodi sasa ni lazima tupate maelezo yake ili Mhe. Waziri tumuingizie na hizi nyengine ambazo anatuomba leo tujue ataziweka katika utaratibu mzuri na zitafuata taratibu zilizopangwa.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu mimi unaendelea katika Idara ya Maendeleo ya Uvuvi ukurasa wa 35. Mhe. Waziri hapa ametueleza mengi kabisa katika idara hii, lakini mimi nina mambo mawili matatu hapa kidogo yamenitia wasiwasi hivyo nataka maelezo kidogo. Katika maelezo yake hapa ameeleza mengi sana, mimi nakuja kwenye suala zima la wavuvi ambao walinyang'anywa mitego yao ambao walikuwa wakiitwa wavuvi haramu. Wavuvi hao wamenyang'anywa mitego yao lakini hadi hii leo hawajalipwa chochote na kwa makubaliano ilikuwa unanyang'anywa mitego ile kwa sababu ni ya haramu watapatiwa zana mbada ya zile.

Mimi mwenyewe ndani ya jimbo langu ninao wavuvi wa aina hiyo katika Shehia ya Kivunge, Kibeni ambao wamenyang'anywa mitego yao lakini mpaka leo hawajapewa zana mbada ya zile ambazo walinyang'anywa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri utakapokuja kwenye majumuisho yako naomba unisaidie katika suala hili, ni lini wavuvi hawa watapata zana mbadala ya zile walizonyang'anywa. Kwa sababu muda umekuwa mrefu na kama utakumbuka zana zile wao ndio zilikuwa zikiwasaidia kuweza kupata kipato, yaani wakijiendesha maisha yao kupitia uvuvi, lakini mlipowanyang'anya zana hizi hamjawapa nyengine maana yake mnawaacha walale na njaa. Kwa hivyo kwa muda ambao mpaka sasa hawajalipwa mimi ningeomba Mhe. Waziri

atakapokuja anipe maelezo ya kutosha katika hili ili wavuvi wangu wale waweze kujua ni lini watapata zana mbadala ya zile walizonyang'anywa.

Pili nisogee katika suala zima la uhifadhi, maeneo yenye hifadhi kama vile *MENAI, PECCA* na *MIMCA*. Mhe. Mwenyekiti, wakati unaanzishwa mradi huu wa hifadhi ya huba hizi kulikuwa kuna makubaliano ya wanavijiji wa maeneo haya, kwamba makusanyo yatakayokuwa yanakusanywa watakuwa wanapata pato kutokana na makusanyo hayo. Lakini cha kushangaza hakuna pato ambalo wanavijiji hawa wanapata mpaka hivi sasa. Kwa hivyo, naomba maelezo katika hili ili tuweze kujua fedha hizi ambazo zinakusanywa wananchi hawazipati au wanakijiji hawa zinakwenda wapi.

Jengine ni suala zima la ugawaji wa maboti ya uvuvi kwa wananchi au kwanavijiji au kwa wavuvi. Mhe. Mwenyekiti, Mradi wa *MACEMP* umekuwa na utaratibu wa kutoa hizi boti na zana zake kama mashine na kila kitu, lakini ugawaji wake mimi nahisi una dosari, sioni utaratibu gani unafuatwa katika ugawaji huo. Kwa sababu unaweza kukuta wale wananchi ambao wanastahiki hasa wapate hawapati matokeo yake anapata mtu badala ya kikundi, mtu mmoja anaweza akapewa boti, mashine na nini kwa sababu tu ya usuhuba au kujuana kwake na watu wengine au wahusika wengine. Sasa hili linatupa tatizo kidogo, kwa sababu wananchi wetu wanalalamika juu ya suala hili, Mhe. Waziri hebu nataka uniambie hasa, katika kipindi cha miaka hii mitatu maana huu mradi unamalizika mwaka 2011 kwa mujibu wa maelezo yake, lakini mimi nachukua hii miaka mitatu, ni mabotiu mangapiu uliweza kuyagawa kwa wananchi na vikundi gani ambavyo vimepata maboti yale na kutoka wapi. Utakapokuja Mhe. Waziri naomba maelezo ya kina juu ya suala hili kwa sababu limekuwa linaleta mzozo sana huko vijijini kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, nisogee kidogo kwenye Idara hii hii kwenye suala la ujenzi wa fisi za *MIMCA* katika kijiji cha Uroa na *MENAI* katika Kijiji cha Kizimkazi. Ujenzi wake umekamilika kama ambavyo ametueleza Mhe. Waziri kwenye hotuba yake hapa. Lakini pana ujenzi pale wa uzio baina ya Uroa huko na Kizimkazi. Masikitiko yangu ni kwamba uzio ule mpaka leo haujamalizika. Sasa Mhe. Waziri nakuomba sana utakapokuja hapa hebu nipe maelezo ya kutosha kabisa juu ya ujenzi huu ni nani mkandarasi, mkataba wake ukoje, muda gani anatakiwa amalize na kwa nini mpaka leo hajamaliza. Utapokuja utupatie maelezo hayo ili nipate nafasi ya kuwaeleza wanavijiji wa maeneo hayo ambao wamenutuma kuja kwako kueleza haya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu ni mdogo sana katika hili, nilikuwa zaidi nataka kugusa kwenye hii Idara ya Uvuvi kuliko hizi idara nyengine kwa sababu naona Mhe. Waziri amekwenda vizuri sana na maelezo yake yanajitosheleza. Lakini nigusie kwenye suala la ujenzi wa masoko ya samaki.

Katika kitabu chake hapa Mhe. Waziri ameeleza juu ya azma ya serikali ya kujenga au kusimamia ujenzi wa soko la kisasa Tumbe. Mimi nataka nimuulize Mhe. Waziri, Tumbe unawajengea soko la kisasa lakini na sisi tuna soko pale la aina hiyo la Bwekunduni, sijui ni lini litakuwemo katika orodha ya masoko unayoyajenga. Kwa sababu soko hili linawasaidia wananchi wetu kweli kweli, karibu asilimia 90 ya akina mama wanaojishughulisha na biashara hizo za dagaa katika Wilaya ya Kaskazini 'A' wanakwenda kwenye soko hili. Soko hili kwa kweli linahitaji kuangaliwa kwa sababu halina hadhi ya kuweza kufanya kazi zile kwa sababu ya yale mazingira yaliyokuwepo, halijajengwa zile ngazi hata za kushukia kule chini kwenda baharini ni mbovu yaani ni soko ambalo limechakaa kweli kweli. Sasa nataka kujua hii wizara yako itatusaidiaje juu ya kuwasaidia wananchi ili nao waweze kupata soko la kisasa pale Bwekunduni kama ambavyo wenzao wengine wa Tumbe na kwengine ambako mmejenga mkaweza kuwasaidia.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, mimi Mhe. Waziri atapokuja kunipa maelezo ya kina kabisa katika haya niliyokujanayo basi bajeti hii nitakwenda nayo, lakini kwa sasa nitakwenda hamsini na hamsini nazibakisha mpaka nikipata maelezo ya kutosha nitamuachia Mhe. Waziri, sikupata katika maeneo hayo itakuwa kwangu kwanza nitazuia kidogo bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nikushukuru kwa kunipa nafasi nipishe wenzangu kama wenzangu waliotangulia wanasema leo ni Ijumaa, tusaidiane kidogo muda tugawane ili tupate kuchangia wengi. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunioa fursa hii na mimi kupata nafasi ya kuchangia bajeti ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Kwa kweli nimefarajika sana kwanza kama walivyoanzia wenzangu nikutakie Ijumaa karim.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli bajeti hii ni nzuri na imefafanua mambo mengi ambayo yanahusu uvuvi na mifugo. Kwanza niende na suala la wavuvi. Kwa kweli Mhe. Waziri aandae mkakati ambao utawasaidi hawa wavuvi, kwani inaonekana kwamba wanaofaidika zaidi ni wachuuzi. Kwa hivyo, serikali ichukue juhudi za makusudi ili kuwapatia soko hawa wavuvi ambao wakiwapatia soko na soko hili ni yenyewe serikali wanunue samaki hawa kutoka kwa wavuvi, kama watachukua fursa hii lile lengo la kujenga afya kwa wananchi wetu litapatikana, kwa sbabu itakuwa ni rahisi na kila mtu atamudu kupata huduma hii ambayo tunataka kuijenga miili yetu ili tupate kufanikisha maendeleo ya nchi yetu.

Vile vile suala jengine ni kuona kwamba kuna haja ya wavuvi katika zile zana ambazo wamepewa basi ili ziwe endelevu Mhe. Waziri awe karibu nao kila muda ili aone shughuli zile na vyombo vile vimo katika hali nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimuulize Mhe. Waziri kwamba kuna mazao mengi tu ya baharini yakiwemo makombe, kaurwe nilipokuwa mdogo nilikuwa naziona namna gani zinatumiwa na wananchi wanazitafuta kule pwambi na baadae kuuza na kupata kujikwamua katika maisha. Kwa hivyo, sijui kama serikali imefuatilia soko la vitu hivi ambavyo ni moja katika mazao ya baharini na yanatoa ajira kwa wananchi kupata mahitaji yao ya lazima.

Changamoto inazozikabili sekta hii na ili mafanikio yapatikane katika jamii na tunajua kwamba mafanikio yakipatikana katika sekta hii kwa vile sekta hii inachangia kwenye pato la taifa tunapata revenue, kwa hivo serikali inaiomba suala hili ilizingatie sana na ilitie katika mkakati wake.

Sasa twende kwenye Idaa ya huduma za utibabu na mifugo, Mhe., Waziri naomba suala hili la ukatili wa wanyama kama vile ng'ombe na punda wanaobebeshwa mizigo kupita kiasi, basi idara hii naomba iwena askari ambao watalifuatilia suala hili na mtu atapopatikana na kosa basi hatua za kisheria zichukuliwe ili asa hao wanyama wapate ile uslama wao. Kwa kweli wanaadhibiwa sana wanyama hao.

Mhe. Mwenyekiti, pia niseme kuhusu suala la hawa ng'ombe na punda kusema kweli tatizo ni kwamba serikali sasa ichukue juhudi za makusudi ili iwapatie ajira hawa watoto wetu au vijana wetu wanaoshughulika na ajira hii ya kutumia hawa wanyama. Kwa kweli ni kero pia katika mji wetu, usione kwamba magazri ya ng'ombe, magari ya punda yanaranda. Kwa kweli sasa hivi tubadilike tuwatafutie mbinu mbadala hawa watoto wetu a vijana mitaani ni aibu sasa kutokana na hali tuliofikia vyombo ni vingi. Kwa hivyo tutumie mbinu mbadala ili kuondosha tatizo hili la punda na ng'ombe kuranda ovyo mijini mwetu, tukienda mijini kwa wenzetu huko hatukuti matatizo haya, lamsingi ni kuwatafutia ajira watoto wetu hawa ili na wao wajikwamue kimaisha. Ng'ombe au punda na hasa punda tunaweza tukawatumia zaidi mashambani ili kurahisisha kazi za wakulima.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi niseme kwamba bajeti hii nimeichangia na vile vile nimshukuru Mhe. Waziri kwa mikakati ambayo ameichukua. Vile vile nimpongeze kwenye ukurasa wa 44 juu ya kahamasisha wakulima wa mwani kujiunga na jumuiya zao za uzalishaji. Kwa kweli hili ni la kumpongeza na kuweko kwa jumuiya kama hizi kunasaidia zaidi kwa sababu jambo la mtu mmoja mmoja siku zote linakuwa na udhaifu wake. Kwa hivyo, nimpongeze kwa hayo.

Vile vile kwenye malengo ya mwaka 2011/2012 kwenye kifungu cha kuhamasisha matumizi ya mwani ikiwemo kutengeneza sabuni na usarifu mwengine kwenye matumizi ya vyakula mbali mbali. La msingi nimuombe Mhe. Waziri kuwapa utaalamu zaidi ili hivi vifaa watavyotengeneza au mambo mbali mbali watayotengeneza basi yawe na ubora zaidi ili na soko lipatikane kwa mujibuwa ubora wa vitu hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, niseme na mimi nimeshaichangia bajeti hii ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani ambao wamenichagua kwa kura nyingi naomba kuunga mkono hoja.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi asubuhi hii kunipatia nafasi ya kutoa mawazo yangu machache juu ya Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. Kwa hivyo, kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha asubuhi hii kufika hapa katika shughuli zetu za kawaida ya kazi zetu. Pili nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti kwa kukiongoza kikao hiki leo kwa ufanisi. Kadhalika nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuwasilisha kwake hotuba yake vizuri kama walivyofanya wenzake. Kwa kweli mawaziri wetu wote wamekuwa ni wataalamu wa lugha ya Kiswahili, kwa sababu kila anayekuja unamuona ni bora kuliko mwenzake aliyepita.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimpongeze waziri kwa kuanzisha huu mtambo wa kupata *liquid nitrogen* ambayo itakuwa inasababisha upandishaji wa ng'ombe kwa sindano kutoka 500 na kufikia 1,275. Hii itaongeza kupata idadi ya ng'mbe zaidi baadae kwa ajili ya kupata mahitaji ya nyama na maziwa.

Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, hii ni miongoni mwa wizara moja nzuri sana, kwa sababu mambo yake yote ni ya vitoweleo, na kuna vitoweleo vingi na vizuri. Kuna ng'ombe tunapata maziwa na nyama, kwa hivyo tunakunywa halafu tunakula nyama. Kuna mbuzi yuko hivyo hivyo, kondoo, kuku, bata na kadhalika. Vyote hivi ni vitoweleo ambavyo vinaongeza siha katika miili yetu, vyote hivi ni vitu ambavyo vina *protein* kwa wingi kwa hivyo ni chakula kizuri. Kwa hivyo nimpongeze waziri kuwa kapata wizara nzuri hii ya mifugo na uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianzie kwenye hii mifugo na nianze kwenye hawa ng'ombe. Tunao ng'ombe wetu wa kiasili tunaowaita kuwa ni ng'ombe wa kienyeji ambao wenyewe tunafuga mabondeni kwa kuwapa majani ya kawaida. Mhe. Mwenyekiti, ng'ombe hao kwa mtizamo wangu mimi maziwa na nyama yao ni nzuri zaidi kuliko hawa tunaowaita ng'ombe wa kisasa. Kwa hivyo, ipo haja na hawa ng'ombe wetu wa kiasili na wao kuwaendeleza ili na wao angalau waweze kutoa maziwa kwa wingi na nyama yao izidi kuboreka. Kwa sababu

nyama yao nzuri kweli kweli kuliko hawa wa kisasa.

Sasa miaka hii tuliyonayo kuna huu ufugaji wa kisasa ambao ng'ombe zaidi tunawafuga na miradi inayotokana na *TASAF* na *PADEP*, tunawalea ng'ombe kama mke anayependwa. Ng'ombe anajengewa banda anawekwa humo, lengo la wananchi wetu kutokana na miradi hii ni kuondolewa umasikini na kuwapatia ajira, lakini sisi tulioko vijijini miradi hii hatukupata ajira lakini tumepata kazi.

Mhe. Mwenyekiti, sisi watu wa vijijini katika miradi hii hatukupata ajira ya kutuondolea umasikini lakini tumepata kazi. Kwa taaluma ndogo tu ya ufugaji ng'ombe hawa tunahangaika mchana wa kutwa kuwatafutia majani na kuacha kazi zetu nyengine za kilimo kwa kumhudumia huyu ng'ombe, ng'ombe huyu anahitaji madawa ya kununua ambapo hatuna pesa, ng'ombe hawa wanahitaji chakula cha kununua ambacho hatuna pesa. Kwa hivyo, baada ya kupata ajira badala yake tumepata kazi nzito, ngumu na kwa hivyo inatuongezea ule umasikini ambao lengo lake ni kuuondoa. Sasa ningeiomba wizara hii ituongezee taaluma sisi wafugaji wa vijiji tuliopewa mifugo hii ili lile lengo lililokusudiwa ni kuwa hii iwe ndio njia ya kutuondolea umasikini wala sio kutuletea umasikini.

Mhe. Mwenyekiti, wafugaji wengi wa ng'ombe hawa nadhani walichagua miradi hii bila ya kufikiria sana na pengine wataalamu mara nyengine hawakushauri vyema kwa sbabu mimi katika jimbo langu atu wengi ambao wamepata ng'ombe hawa ama kutkka kwa *PADEP* au *TASAF* zaidi ya asilimia 60 hawa ngombe wamekufukuacha, nadhani ni kwa sababu nyingi tofauti, moja ni taaluma ndogo ya sisi wafugaji pengine hatuwezi kuwakimu vilivyo, ukosefu wa matibabu ya mara kwa mara kwa wanyama hawa, lakini kubwa zaidi ni mazingira wanayotoka wale wanyama na kule wtunakowafuga sisi. Wengi wao ng'ombe hawa wanatoka katika sehemu za baridi wanakuja katika shehia yangu ya Mkungu ambayo *almost* wakati wote ni joto. Kwa hivyo yale mabadiliko ya hali ya hewa pia yanachangia ng'ombe hawa kupotea.

Mhe. Mwenyekiti, hapa wafugaji wetu wamepata kazi kubwa badala yake hakuna walichopata, hivyo ni kwamba wamefanya kazi ambayo haikuleta matunda. Ningeiomba wizara inapoleta miradi kama hii iwasaidie wananchi kuwashauri ni miradi gani wachague ili ilete maslahi. Kwa sababu mara nyengine wananchi wanachagua mradi kwa utashi tu, anataka kufuga bila ya kutazama athari nyengine za mazingira ya pale walipo. Sasa Mhe Waziri itabidi hawa wataalamu wako ambao hapa umeonesha unao wachache tu wenye elimu ya juu kidogo ambao ni kama 38 kwa wizara yako nzima, uongeze kusomesha wataalamu zaidi wa mifugo ili waweze kuwahudumia wafugaji wetu wa vijijini.

Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba Mhe. Waziri wataalamu wake wa mifugo wasingojee kuwa mfugaji apeleke ombi kuwa ng'ombe au mbuzi wangu au kuku wangu anaumwa. Wapange ratiba maalum ya kuwafikia wafugaji katika maeneo yao kwa kuwahudumia. Tusingojee pale ng'ombe yuko taabani atafutwe daktari hata akija watu ng'ombe wameshamla nyama kwa kuwa hawamwachi akafa kwa sababu anakuja daktari.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri na wataalam wake wa mifugo kuhusiana na utibabu waweze kuzunguka kwa ratiba kuwahudumia hawa wanyama ili walete tija kama iliyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye Idara hii ya Utibabu wa Mifugo mwaka uliopita 2010/2011 walitarajia kukusanya shilingi milioni 48 lakini halisi walizokusanya ni milioni 27,924,590. Mwaka huu 2011/2012 wameweka matarajio hay ohayo ya kukusanya kama walivyoweka mwaka jana. Lengo ambalo mwaka jana hawakulifikia na mara hii wamejipangia lengo hilo hilo na fedha walizokusanya ni asilimia 50 na kidogo tu. Hii inaonekana kuwa bado kuna matatizo ya taaluma kwa wafugaji kuweza kuwapeleka wanyama wao katika sehemu za tiba. Kwa hivyo, narudia kusema tena kuwa elimu ya tiba iongezwe ili haya mapato yaweze kupatikana.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, makusanyo haya yameonesha kuwa ni kwa Unguja tu. Nimuulize Mhe. Waziri huku Pemba hakuna wanyama na kama wapo wao hawatibiwi, kama wanatibiwa wao hakuna mapato ya serikali inayopata. Kwa sababu hapa haikuonesha.

Mhe. Mwenyekiti, halikadhalika wafugaji wetu wameanzisha vikundi kadhaa vya ufugaji wa kuku, wengine wanafuga kuku wa kienyeji, wengine kuku wa kisasa. Lakini bado watu wanaanzisha ufugaji huo bila ya taaluma ya ufugaji. Kwa hivyo, mtu anaanza na kuku wake 10 baada ya kuongezeka wanapungua. Kwa sababu kule Pemba kuna mabanda ya kuku kila sehemu ina lahaja yake ya lugha. Mimi katika eneo langu mabanda ya kuku watu wanaita magwa. Kuku anaumwa anatoka urenda puani na mdomoni na kufa. Sasa badala ya mifugo kuongezeka mara nyingi inakufa kwa kukosa hizi huduma za matibabu.

Kwa hivyo, tukianzisha miradi iwe tumejipanga namna miradi hiyo kuweza kuihudumia. Vyenginevyo lile lengo tulilojipangia kuondosha umaskini badala yake itakuwa tunawapa kazi ili wajiongezee huo umaskini.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie sekta ya uvuvi. Mhe. Spika, sekta hii ni muhimu ambayo inawapatia pato wavuvi wetu. Lakini kwa sehemu kubwa wavuvi hawafaidiki sana na kazi yao ya uvuvi wanayofanya, zaidi

wanaofaidika ni watu wa kati kati, pengine mchuuzi atakuwa na maslahi zaidi kuliko mvuvi mwenyewe. Sijui tatizo ni lipi, lakini Mhe. Waziri kwa sababu kawekwa hapa ni mtaalam anaweza akanisaidia kwa nini mchuuzi anafaidika zaidi kuliko mvuvi. Kwa hivyo, hawa wavuvi wetu tuwapatie zana za kisasa za kuweza kuwasaidia.

Mhe. Mwenyekiti, kama sikufahamu vibaya juzi kwamba huku ukitumia nyavu inaonekana kama samaki wanapayuka payuka kwa hivyo hawapendelei sana. Wanaambiwa watu zaidi watumie mshipi ambao kwa mawazo yangu mimi ni kurudi nyuma kwa sababu uvuvi huu ni wa kiasili ambao ulikuwa ukitumika huko nyuma. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kama nilifahamu vibaya ningeomba Mhe. Waziri anisaidie na anielimishe ili na mimi nikawaelimishe wavuvi walioko katika jimbo langu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache naunga mkono hoja hii, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Kabla hatujamkaribisha Mhe. Hassan Hamad Omar naomba Waheshimiwa Wajumbe tumkaribishe Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ili aweze kutoa hoja juu ya utaratibu wa kesho na kesho kutwa.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mkutano wetu huu wa Nne wa Baraza hili la Nane unaendelea kujadili Bajeti za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2011/2012. Kwa kuwa bado kuna wizara nyengine nne ambazo bajeti zake hazijawasilishwa na kujadiliwa na kupitishwa kwenye Baraza hili. Kwa kuwa kuna miswada ya kuidhinisha matumizi ya serikali kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na miswada mingine miwili kutoka Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Kwa kuwa tunakusudia kumaliza shughuli zote za Mkutano huu wa Bajeti kabla ya kuingia kwa mwezi mtukufu wa Ramadhan.

Kwa hivyo, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu liendelee kukutana hata siku za mwisho wa wiki yaani Jumamosi na Jumapili ya tarehe 23 na 24 Julai, 2011 na tarehe 30 na 31 Julai, 2011 ili tuweze kukamilisha shughuli za Mkutano wetu huu wa Bajeti kwa ufanisi mkubwa. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ametoa hoja na hoja inataka kuamuliwa, lakini sijui kama tuliomo humu ndani kwa mujibu wa

kanuni zetu tunatimia idadi ya kuweza kufanya maamuzi. Kwa sababu kwa mujibu wa kanuni zetu ili tufanye maamuzi tunahitaji kufikia angalau nusu ya wajumbe. Kwa hivyo, niombe kwamba labda ipigwe kengele ama wangeitwa wajumbe ili tutimie tuweze kufanya maamuzi.

Katibu: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli wajumbe wako 35 kwa hivyo nusu ya wajumbe haijatimia, tunatakiwa tuwe wajumbe 41 tuweze kufanya maamuzi.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo, tutaomba tuendelee hadi hapo wajumbe watakapokuwa wamekamilika. Endelea na utaratibu Mhe. Mnadhim wa Baraza ili uhakikishe wajumbe wako wametimia tuendelee na utaratibu mwengine.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru nami kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu wakati hautoshi nianze na mchango wangu moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ni visiwa vilivyozungukwa na bahari, kuna wavuvi wa kutosha kwa kila sehemu yenye bahari na ndio rasilimali yetu kuu Mwenyezi Mungu aliyotujaalia.

Mhe. Mwenyekiti, nikizungumzia sekta ya uvuvi, wavuvi wetu ni wavuvi wadogo wadogo ambao hawana uwezo wa kwenda sehemu za mbali katika shughuli zao za uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, sekta hii ya uvuvi inaongezeka, wavuvi wameongezeka na pato la taifa linaongezeka vile vile. Ukiangalia mwaka 2009 pato la taifa limeongezeka kutoka asilimia 5.2 mpaka kufikia asilimia 6.1 mwaka 2010. Hili ni ongezeko kubwa lakini nathubutu kusema katika ongezeko hili la pato la taifa Wakojani wanaongoza kwa asilimia kubwa katika kuchangia pato hili.

Mhe. Mwenyekiti, nimesema Wakojani ni wavuvi kama wavuvi wenzao lakini wao wako juu zaidi. Katika kisiwa cha Kojani hakuna nyumba hata moja isiyokuwa na mvuvi. Wakojani wanaoishi nje ya Zanzibar nao wanaishi kwa uvuvi vile vile, ni watu wachache tu wanaofanya biashara nyengine. Lakini walioko Dar es Salaam wengi wao ni wavuvi na wanaishi huko. Kwa hivyo, wanachangia kiasi kikubwa cha pato la taifa.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, jambo la kusikitisha Wakojani hawa hawakupewa kipaumbele kama ni wavuvi wanaochangia kiasi kikubwa cha pato la taifa. Lakini nimpongeze Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa kuwa na azma nzuri huko tunakoelekea. *Inshaallah* Mwenyezi Mungu ampe uwezo na ufanisi mzuri atujenge katika mambo ya uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, nimesema kwamba sekta hii ya uvuvi imeajiri watu wengi sana, hata siku hizi pale Mikunguni wafanyabiashara ya samaki basi wapo wanawake. Mhe. Mwenyekiti, pia Mhe. Waziri akitaka kufanya takwimu zake aende soko kuu la Malindi atawaona Wakojani wako mbele. Nenda Pemba Tumbe, basi hiyo iliyosababisha mpaka kujengwa soko la kisasa Tumbe nathubutu kusema ni wavuvi wa Kojani, ndio wanaochangia asilimia mpaka kuonekana pana hadhi ya kujengwa soko. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rufai Said Rufai ni shahidi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini wavuvi wetu hawana vifaa vya kufika maji mengi na kupata maslahi mazuri ya uvuvi. Zamani hapa palikuwa na maduka ya vifaa vya uvuvi sijui maduka yale mpaka leo yapo au yamekufa. Nafikiri Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho hili atueleze kwa bayana. Ilikuwa kunauzwa vifaa vya uvuvi kama vile nyavu, mashine, mishipi na kila kitu pale Malindi lakini sasa hivi hatuioni huduma hiyo kama inaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, Wakojani sasa hivi nawaomba watambue na wamejipanga wana Jumuiya yao ya Maendeleo ya Wavuvi wa Kojani na ofisi yake kuu ipo pale Mtoni kwa Mhe. Nassor Ahmed Mazrui. Mhe. Mwenyekiti, hawa wakiendelezwa watafikia hatua na *inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tutafikia mafanikio kila mtu atapea kwa nguvu na atakula samaki wenye lishe nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, wavuvi wetu wa Zanzibar wanapokwenda Dar es Salaam katika shughuli zao za uvuvi wakitokea Unguja au Pemba wanapata matatizo. Matatizo wanayoyapata wavuvi wetu ni kukatishwa leseni za uvuvi mara mbili. Sijui Mhe. Waziri hili analijua na kama analijua lipate ufumbuzi, kama halijui vile vile atatufahamisha.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, ni kuwa wavuvi wetu hapa wanataka leseni ya mvuvi shilingi elfu nne na wanapofika Dar es Salaam huwa wanakatishwa leseni nyengine shilingi elfu kumi na sita jumla shilingi ishirini elfu hili lipo. Wakati wavuvi kutoka Dar es Salaam wanakuja kuvua bahari ya Zanzibar na hatuoni kukatishwa leseni, tunayakuta maboti makubwa yanapaki pale Forodha mchanga katika sehemu zao za mapumziko wakenda wakimurika taa huko hatuoni kukatishwa leseni. Namuomba Mhe. Waziri alifuatilie suala hili kwa nguvu zake zote.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea natoa pongezi sana kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi tuna matumaini makubwa. Nasema hivyo kwa sababu kuna vijana 30 tayari wameshaorodheshwa na baada ya muda mfupi watakwenda Jamhuri ya Watu wa China katika mafunzo ya

ufugaji wa samaki. Mhe. Mwenyekiti, Wapemba watampongeza sana Mhe. Waziri kwa hatua za mwanzo hizo zinazotupa matumaini makubwa na mimi ndani ya jimbo langu nimefaidika yumo mmoja nashukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie Kisiwa cha Misali ambacho kiko katika mambo ya hifadhi, lakini jambo la kusikitisha hifadhi ile iliyoko katika Misali kuna ubaguzi. Kuna wengine wanavua na kuna wengine hawaruhusiwi kuvua hili ni tatizo. Tunamuomba Mhe. Waziri akija hapa atufahamishe. Wanaoonana hivyo ni wavuvi, wavuvi wa Kingoji wanaruhusiwa kuvua lakini wavuvi wengine hawaruhusiwi, wengine wakipita tu pale wanachukuliwa hatua za kisheria. Naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze kwa kina.

Tunaomba utaratibu na sheria zitumike kuwa watu wote ni sawa mbele ya haki ya sheria. Kama mahali pamezuiliwa kuvua basi wote wasivue, akiwa mvuvi wa nyavu, akiwa mvuvi wa dema, akiwa mvuvi wa mshipi na wengineo wote wasivue. Lakini isiwe leo Suleiman anavua Juma haruhusiwi hili ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, katika mambo ya ufugaji wa samaki hili ulilolianza kwenda kuwasomesha vijana wetu katika ufugaji wa samaki ni jambo zuri. Mwenyezi Mungu akiwajaalia wakihitimu hawa wataupunguza ule uzito wa bahari kidogo wengine wataelemea katika mashamba ya ufugaji wa samaki. Wenzetu pale katika soko la kimataifa Feri Dar es Salaam wanakuja samaki wanaitwa Kamungu wanakuja kwa ndege, hawa ni watu wanaofuga samaki tu kule. Wenzetu katika maziwa huko Mwanza wanaleta samaki wa minofu.

Sasa ikiwa hapa tutafanya mifugo kwa kutumia mashamba hayo ya samaki tutafaidika vya kutosha na nchi yetu nayo itasafirisha samaki na watatutosheleza kwa kula.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kwamba hatujafikia huko lakini huu uvuvi tulionao kuna siku wavuvi wetu hawana soko wakati wa *season*. Tunashuhudia samaki wakiuzwa kwa njia ya magari pale Mikunguni na sehemu nyengine wakitembezwa hawana soko. Kwa Pemba ni Machomane hukamata samaki wengi mpaka wachuuzi wameshashiba hawana pakuwapeleka wanakwenda mitaani. Tunaomba masoko yawepo au tupate vifaa vya kuhifadhia samaki hapa tutakuwa tumepiga hatua.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie ukulima wa mwani. Mhe. Mwenyekiti, ukulima wa mwani wananchi kidogo wanashukuru wamepiga hatua nzuri kutoka kilo shilingi 250 mpaka 400. Sasa hivi kuna kampuni nyengine inayoitwa *Aqua* wao watanunua mwani kwa shilingi 500. Kampuni hii tayari imeshaanza shughuli zake sehemu za Mkoani na karibuni Wilaya ya Wete wataanza shughuli zao wameshakodi nyumba yao pale. Kwa hivyo,

tunashukuru.

Lakini vile vile kuna migogoro ya hawa wavuvi wa mwani na wavuvi wengine. Mhe. Mwenyekiti, kuna matatizo lazima yaangaliwe kwa kina na yaweze kutatuliwa. Kwa sababu mnamopandwa mwani ni sehemu ya hifadhi, maana yake ukishakupanda mwani huwezi kufanya shughuli nyengine. Kwa hivyo, watengewe maeneo na shughuli nyengine zifanyiwe maeneo ya uvuvi. Lakini siku zote kama utapandwa mwani basi itafikia kama kule Marumbi na Chwaka. Juzi nilisikia kwenye mawio wanazungumzia bado wanagombania kwa nafasi ndogo ya uvuvi kwamba wakati huu wa kusi hawawezi kwenda katika bahari kuu, kwa hivyo wanafanya shughuli zao za uvuvi sehemu ndogo tu na haikidhi haja.

Mhe. Mwenyekiti, tunaomba wavuvi wetu wapatiwe vifaa vya uvuvi. Pia namuomba Mhe. Waziri asije kuleta kiboti kimoja kile kwa kila sehemu akasema amewasaidia wavuvi. Nathubutu kusema boti moja ya Mkojani inabeba mabaharia kuanzia 50 mpaka 55 na ukitaka kujua nenda Malindi ukakae pale na mimi nitakuwa mwenyeji wako nitakupeleka. Lakini viboti vile ulivyotuonesha katika semina ile vya watu 6 havikidhi haja bado utakuwa hujafanya kitu.

Mhe. Mwenyekiti, tunaomba katika kuelekea huko tunakokusudia utuletee meli Wakojani na wavuvi wengine wana uwezo huo kuweza kukaa baharini hata miezi mitatu na bado wanastahamili. Kwa sababu Wakojani ni watu wa kutoka kwenda madago sehemu zote wameenea na katika madago yao wanachukua miezi mitatu mpaka sita wengine hawajafika majumbani mwao. Namuomba Mhe. Waziri aliangalie kwa kina suala hili ili wavuvi wetu wapate tija.

Mhe. Mwenyekiti, nikirejea katika sehemu ya hifadhi ukurasa wa 39 nimeona kuna sehemu tengefu ambayo tayari imeshatengwa na wakati wowote zinaweza kutangazwa kuwa sehemu za hifadhi na Kojani imo ndani. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kupitia Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi Kojani kama itawekwa hifadhi ya baharini nasema ni tatizo kwa sababu za msingi. Hifadhi hiyo inakusudiwa kuwekwa kisiwa Subi mpaka kisiwa cha Kikwajuni ikiwa eneo lote la sehemu ya uvuvi imefungika na Wakojani wanaishi kwa kufanya kazi za uvuvi. Naomba Mhe. Waziri aliangalie kwa kina suala hili ndio afanye maamuzi.

Kwa sababu upande wa pili kuna bahari kuu na bahari kuu inakwenda kwa misimu tena kaskazi tu, ikitoka wakati wa kaskazi hakuna hata mmoja anayevua ndani wote wanavua bahari kuu, lakini wakati huu wa kusi huwezi kufika huko hata siku moja. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hatupingi kuweka hifadhi lakini aangalie na mazingira jinsi yalivyo. Ukisema unataka kuweka

hifadhi kwa kulinda mazingira halafu ukaweka hifadhi ya kuua wananchi kwa habari hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hapa kwa kurudia mara ya pili kama hakuna nyumba hata moja Kojani isiyokuwa mvuvi. Nasema shughuli yao ni hiyo tu, Wakojani wanasoma kuna wengine wana digrii ya sheria, diploma, ni wengi tu vijana sasa hivi wanasoma vizuri sana, lakini katika kusoma kwao na wavuvi wamo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja hapa alete ufafanuzi mzuri ili wananchi wapate kuelewa, tuko pamoja na wewe wala sina haja ya kuweka buti kwa jambo lolote. Najua una nia njema na *inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu utatufurahisha.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu leo ni siku ya Ijumaa na bado wachangiaji ni wengi naomba kwa muda huu niishie hapo. Nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru muumba wetu Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujaalia tuwe na neema hii ya uhai na uzima tukaweza kukutana tena katika ukumbi wa Baraza hili kujadili masuala ya maendeleo ya nchi yetu na watu wake. Mhe. Mwenyekiti, pili nikushukuru na wewe kwa kunipatia nafasi hii katika kikao hichi cha asubuhi Ijumaa ya leo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo naomba nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Hotuba yake kusema kweli ni ya kina na katika maeneo mengi imetosheleza kiu zetu hasa katika kule kuonesha jinsi alivyojipanga na watendaji wake kuleta yale ambayo Rais wetu Dk. Ali Mohammed Shein anayaita mapinduzi ya sekta hizi za mifugo na uvuvi katika Zanzibar. Maana unaweza ukawa na kauli mbiu kama hizi lakini halafu mipango isijioneshe hivyo. Lakini kwa hapa nathubutu kusema kwamba ukiitazama hotuba hii imeonesha malengo madhubuti.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na uzuri wa hotuba hiyo nilikuwa naomba Mhe. Waziri kuna maeneo machache nitoe maoni yangu na pia niombe ufafanuzi wake katika baadhi ya maeneo hayo. Naomba nianze na Idara ya Uzalishaji Mifugo ambayo imezungumziwa katika ukurasa wa 21 hadi 27 wa hotuba yake.

Mhe. Mwenyekiti, katika kueleza malengo ya kuimarisha sekta hii ya uzalishaji wa mifugo katika ukurasa wa 25 kifungu cha (i) amezungumzia suala la kushajihisha ufugaji wa kuku wa kisasa kwa mashirikiano baina ya wawekezaji wa ndani na wafugaji wenyewe ili kuongeza uzalishaji wa ndani wa mayai na nyama. Halafu akatwambia naomba nitoe habari njema kwamba kampuni ya Sheikh Al-Youseif na wizara yangu zimo katika hatua ya kutayarisha hati ya makubaliano ya uanzishaji uwekezaji mkubwa wa ufugaji wa kuku wa mayai

hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, sekta hii ya uzalishaji wa kuku na mayai hasa kwa shughuli za kibiashara hivi sasa inaonekana kushika kasi Zanzibar na tunao Wazanzibari wengi ambao wamejiingiza wakiamini kwamba wanaweza kuchangia katika kubadilisha maisha yao lakini pia kusaidia kuajiri watu wengine.

Sasa katika hili nilikuwa nataka maelezo tu ya Mhe. Waziri kwamba tunapokaribisha mwekezaji wa nje pamoja na ukarimu mkubwa wa watu Sheikh Al-Youseif wala hatutoi shukrani. Lakini je, haitakuja hii kupelekea kuwatoa hawa wawekezaji wetu wa ndani wadogo wadogo ambao wameanza kuinukia katika sekta hii. Kwa sababu wawekezaji wakubwa mara nyingi wakiingia wanakuja na uwezo mkubwa.

Hivi sasa Mhe. Mwenyekiti, kuna ushindani mkubwa katika sekta hii baina ya hawa wazalishaji wa ndani na wanaoagiza vifaa hivi kutoka nje. Sasa tukianza kuweka mwekezaji mkubwa kama nilivyosema, lakini sisemi kama namkataa lakini nataka nihakikishiwe. Mimi nadhani kwa sababu hakuna maelezo ya kutosha hapa waziri hebu anisaidie, kama Sheikh Ali Yussuf atatusaidia kuja kuwekeza katika kupata wale wanaitwa kuku mama ambao watasaidia kutoa vifaranga na mayai ambayo yatakwenda kwa wale wawakezaji wa ndani basi mimi naukaribisha sana mradi huu. Lakini ikiwa yeye mwenyewe atajiingiza katika uzalishaji huu wa vifaranga na kuzalisha kuku wa mayai, basi bila shaka tutawasaidia pakubwa vijana wetu ambao tayari wamejijenga.

Mhe. Waziri najua anawajua kwa sababu moja katika sifa yake kubwa na wanamsifu wawekezaji katika sekta hii kwamba mara tu baada ya kuteuliwa alikwenda kuwatembelea na akajionea mwenyewe kazi kubwa ambayo wanaifanya. Kwa hivyo, nilikuwa naomba katika hili alitizame kwa makini na naomba maelezo akija anisaidie huu mradi wa Sheikh Ali Yussuf utajielekeza huko au ndio utakuja kuwa wa ushindani na kuanza kuwatoa hawa wawakezaji wetu wa ndani.

Pili Mhe. Mwenyekiti, nimuombe katika hili awasaidie hawa wawekezaji wetu wa ndani, sekta hii imekuwa inaathirika kwa sababu kama ilivyo katika sekta nyingi, kutokana na gharama kubwa za uzalishaji. Ukitizama hata bei ya chakula ukilinganisha Bara na hapa basi kuna tofauti kubwa. Kwa hivyo, pengine serikali ingeweza kuangalia vipi inaweza kuwafidia na kuwasaidia hawa ili waweze kuzalisha kwa gharama nafuu.

Katika sekta za kilimo Mhe. Mwenyekiti, niliwahi kumsikia Mhe. Rais akisema kwamba lengo letu ni kuanzisha ule utaratibu wa kutoa ruzuku au ku-*subsidize*. Sasa kama tuna *subsidize* katika kilimo hata katika sekta hizi za uvuvi na

mifugo pia tuone umuhimu wa kufanya hivyo. Kwa hivyo, nilikuwa nasema kuna masuala ya chakula, kuna masuala mazima ya kuweka pengine udhibiti fulani wa hizi bidhaa kama hizo zinazotoka nje ili kusaidia kukuza uzalishaji wa ndani. Nadhani hilo ni muhimu sana.

Pia Mhe. Mwenyekiti, katika hili niseme kuwa wanalalamika wawekezaji kwamba pamoja na kuwa tuna idara ya huduma za utabibu, lakini wanafika miaka mitano wengine au miaka saba hawajawahi kutembelewa na daktari katika maeneo yao wanayofuga. Kwa hivyo, nasema kama kuna upungufu wa vifaa au daktari basi waziri atuambie na atuambie kwa nini inatokezea hivyo, na kama kuna upungufu huo basi wizara yake imejipanga vipi ili kuukabili upungufu huo ili tuone kwamba vijana wetu wanaojiingiza katika sekta hizi waweze kunyanyuka.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo nimuombe waziri akija anisaidie Zanzibar tulipewa eneo la makurunge Bagamoyo pale na mara nyingi linaulizwa swali hili, lakini majibu yake yanakuwa siku hizi kila siku yanapishana pishana. Hebu tuambiwe *status* ya Makurunge sasa hivi iko wapi au ikoje. Tunavyoelezwa ni kwamba eneo hilo limevamiwa. Sasa mimi nilikuwa nadhani kama tumepewa basi ilikuwa ni mali ya Zanzibar. Lakini kuna tatizo zima la kuwa tumepewa lakini hakuna hatimiliki ya kumiliki eneo lile. Sasa kama tulipewa na bila shaka ndio itakuwa katika zile faida chache za Muungano wetu basi hebu tuambiwe katika hii *status* ya Makurunge. Kwa sababu huku kunaweza kufanyika mradi mkubwa kama ulivyokuwa mwanzo wa kufungua *ranch* ya ng'ombe, lakini inaonekana hivi sasa mradi huu hata kuzungumzwa hauzungumzwi tena suala la Makurunge. Kwa hivyo, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri akija anisaidie maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, katika sekta hiyo hiyo ya mifugo kwenye idara ya huduma za utabibu, nilikuwa naomba kujua kwamba dhamana ya kusimamia uhakika wa afya za wananchi wetu katika masuala mazima ya kutunza vitoweo katika masoko yetu. Kwa sababu kila ukiyatizama masoko yetu hali zake ni mbaya sana, kuanzia pale inapowekwa hiyo nyama unavyoitizama, huko unakokatiwa na wale wanaoibeba ile nyama ukiwatizama mtu utamkuta kajitwika kichwa kiko wazi na huku kajitwika paja la ng'ombe anakwenda nalo sokoni pale.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, tunazungumzia Zanzibar kubadilika, lakini hatuwezi kubadilika ikawa mambo yetu bado yanaendeshwa ki-*local kiasi* hiki, zile *standard* zinataka zibadilike. Sisi sasa hivi sekta kubwa tunayoitegemea ni utalii, sasa hatuwezi kuzungumzia utalii mgeni anakwenda pale akiiona nyama hata kuila anaifikiria mara mbili mbili. Kwa hivyo, ndio nasema kuna haja ya kuona, sijui kama wizara hii inahusika, lakini kuona ukaguzi wa masoko na sio ukaguzi tu, maana unaweza ukakagua halafu ukaondoka ukaridhika. Lakini ku-

enforce zile kanuni, yaani kuzitilia nguvu kanuni zetu ili kuona kwamba kuna imarika huduma kama hizi katika masoko yetu.

Mhe. Mwenyekiti, labda niseme kabisa hapa isiwe kwa nyama tu lakini hata kwa samaki. Ukenda pale katika masoko kuanzia pale Malindi, ambapo wavuvi *standard* kama Mhe. Mansour juzi mpaka nyimbo katuimbia hapa. Ukenda kutizama wanapoteremshwa wale samaki hali yake wanavyobururwa pale au pale kwenye soko kuu la Darajani ukenda kutizama hali yake hairidhishi hata kidogo Mhe. Waziri. Kwa hivyo, kwa vile tunazungumzia Zanzibar mpya ya maendeleo basi mambo madogo madogo kama haya tuyaweze.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili niseme kwamba kuna suala zima. Maana yake tunatilia nguvu wakati fulani zile kanuni halafu tunaziwacha. Nitatowa mfano wa Forodhani ingawa haihusiki hapa. Ilipokabidhiwa mwanzo kulikuwa kuna *strict regulation*, ukenda pale watu wote wamevaa ma-*apron* na makofia yao. Lakini baada ya muda tumewaachia, nafikiri baada ya kuondoka Taasisi ya Aghakhan katika usimamizi tumewaachia na tumerudi kule kule tulikotoka. Anaanza mmoja kuwachwa na ndio katika maumbile ya binadamu. Nilisema jana kama hakuna kutilia nguvu sheria basi sheria zitakuwa hazina maana. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba tulitizame sana hili la kuwajengea watu wetu utamaduni wa kuheshimu vitu kama hivi.

Mhe. Mwenyekiti, katika hilo la mifugo kumalizia hapo nije katika suala zima la sekta ya uvuvi. Katika sekta ya uvuvi nimeona Mhe. Mwenyekiti, na nampongeza sana Mhe. Waziri katika miradi yake hasa ule mradi ambao uko katika kiambatisho nambari 1, unajielekeza kwa kiasi fulani kuliko kuzungumza. Kujenga machinjio ya kisasa ya kuku ya ng'ombe na mbuzi. Sasa nilikuwa nadhani katika hilo kuna sehemu kuna mradi mwengine unahusu ujenzi wa masoko haya ya samaki. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nilikuwa naomba upatupie jicho sana pale Malindi na mimi naomba niseme hasa kwamba wakati umefika lile soko pale halifai tena, hebu tutafute eneo jengine la kwenda kujenga soko, pale lile eneo limezidiwa mno na shughuli nyingi, huku bandari inapanua shughuli zake. Pale pana eneo pamewekwa mwekezaji nafikiri panajengwa kiwanda cha mafuta ya kula sijui kitu kama hivi.

Sasa ukija huku ile hali ya uchafu iliyokidhiri ni mbaya sana, kwa hivyo nadhani soko lile tungelipatia pahala pengine. Mhe. Mwenyekiti, tuna eneo zuri la Kizingo labda pangeweza kutizwamwa pale kama panaweza kuwafaa, kwa sababu wavuvi wengi wanapendekeza kwamba pale ndio wangejengewa soko la kisasa. Lisiende Tumbe tu kwa Mhe. Rufai Said Rufai, lakini pia tupate soko la kisasa katika Mji wa Zanzibar ili lilingane na hadhi ya mji wetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 9 hotuba ya Mhe. Waziri kwenye malengo ya sekta hii kazungumza habari ya kugawa vifaa na misaada mbali mbali kama mashua na mashine. Kwa hivyo, nilikuwa naomba anisaidie kwamba katika hili basi asiusahau na Mji Mkongwe, maana yake mara nyingi kumekuwa na kawaida ya kuona labda wavuvi wako katika maeneo ya mashamba tu, lakini Mji Mkongwe ndiko kwenye wavuvi *sturdy* kama Mhe. Mansouri hapa, hata Mhe. Mansour angependa na yeye akapatiwa mashine na mashua ili aweze kuvua vizuri zaidi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba, sio peke yake Mhe. Mansour kuna na wavuvi wengine kule Malindi wanaovua Forodha mchanga hapa wengi wana ushirika wao. Wengine wamekuwa wakilalamika kwamba huko nyuma tulikotoka pengine na siasa zilivyokuwa walikuwa hawapati fursa walizokuwa wakizipata wengine. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri alitupie jicho la rehma Jimbo la Mji Mkongwe.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 11 nilitaka kumpa changamoto tu Mhe. Waziri, hapa katuelezea kukua kwa uvuvi, lakini zile takwimu zake kwenye kifungu cha (a) mimi kidogo namuomba Mhe. Waziri akaze buti zaidi. Sisi katuomba tusimpigie buti, lakini namuomba yeye akaze buti zaidi. Kwa sababu katuzungumzia kuongezeka kwa tani za samaki wanaovuliwa, lakini ukitizama kilichoongezeka ni kama tani 300. thamani imeongezeka, lakini naamini thamani imeongezeka kwa sababu ya dola kwa siku hizi *exchange rate* zinabadilika. Lakini ukitizama ukitizama samaki wanaovuliwa tani 25,396 wameongezeka kufika tani 25,693, ni kama tani 300 tu. Kwa hivyo, naomba katika hili Mhe. Waziri ajipange zaidi ili tuone kwamba tunakuza hili.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije katika Idara ya Maendeleo ya Uvuvi katika mradi hasa huu wa *MACEMP*. Mhe. Mwenyekiti, katika hili naomba maelezo kidogo kwenye fedha ambazo zimepangwa kutumika. Nilipoangalia kiambatisho nambari 5 katika hotuba ya Mhe. Waziri na kwa sababu ya kupisha muda sikusudii kuisoma. Pale pametajwa fedha zile ambazo zinatumika, labda nisome haraka haraka. Jumla ya gharama inasema ni bilioni 31.34 Benki ya Dunia, bilioni 25.194 Shirika la Uhifadhi wa Mazingira Duniani, *GF* bilioni 5.187 na Shirika la Maendeleo ya Japan JSDF ni milioni 959.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nilipozitazama hizi na hizi zinazopangwa kutumika kwa mwaka ujao wa fedha ambazo ziko katika ukurasa wa 61, kidogo hazilingani kimahesabu na hesabu ambayo kamati ya Mhe. Asha Bakar Makame ilitutajia katika ripoti yake. Katika ripoti ya kamati katika ukurasa 83 katika buku hili tulopewa, palitajwa kwamba mradi umepata ufadhili wa mashirika mbali mbali wa maendeleo kama Shirika la Uhifadhi wa Mazingira Duniani dola milioni 10, Benki ya Dunia dola milioni 51 na SMZ imechangia jumla ya milioni 142, 195,000. Kwa hivyo, hesabu hizi hazilingani na hesabu za Mhe. Waziri ambazo ziko katika kiambatisho chake. Mimi naamini kamati

itakuwa imezipata kutoka kwa watendaji wa wizara. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri akija hapa atusaidie huu mgongano wa kimahesabu umekosekana wapi.

Hapo hapo Mhe. Mwenyekiti, niseme nikiisoma ripoti hii ya Mhe. Asha Bakar, ripoti ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwekezaji na Habari imetaja kwamba fedha hadi kufikia Novemba 2010 kiasi cha dola milioni 16.5 zilikwishatumika kwa Zanzibar na fedha zilizobaki milioni 8.5 zitatumika kwa kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Idara ya Uvuvi, Ujenzi wa Mamlaka ya Uvuvi, Ujenzi wa Soko Tumbe na mambo mengine. Kwa hivyo, nilikuwa nasema nikifanya mahesabu hizi sesabu zilizotolewa ujumla wake kwamba zipo hapa, halafu nikijumlisha zinazotumika dola milioni 16. 5 na zilizobaki milioni 8.5 bado ziko chini ya hii hesabu ya jumla ambayo imetolewa hapa. Kwa hivyo, naomba maelezo kutoka kwa Mhe. Waziri akija.

La mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti. Naomba nije katika suala la uvuvi wa bahari kuu. Mhe. Mwenyekiti, sote ni mashahidi hapa. Kwanza uvuvi kama wenyewe uvuvi haumo katika orodha ya mambo ya Muungano. Lakini wenzetu katika ile ile kutupenda ndugu zetu wa damu wakaja na sheria ya kuhusu uvuvi wa bahari kuu wakasema inatumika pia Zanzibar. Tukavutana wee mwisho Baraza hili hili likaikwamisha ile sheria isitumike Zanzibar mpaka papatikane ufumbuzi wa mgawanyo wa mapato. Pakawekwa *formula* kwamba katika fedha zile asilimia 50 zitakazopatikana zitumika katika uendeshaji wa mamlaka ya bahari kuu na mambo ya utawala na asilimia 50 iliyobakia igaiwe asilimia 60 iende Bara na asilimia 40 iwe ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nasikitika katika kitabu kizima cha Mhe. Waziri hatukuona popote mapato tuliyopata kutoka Uvuvi wa Bahari Kuu. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nacheka kidogo kwa sababu rafiki yangu Mhe. Waziri katika kuelezea changamoto pale pale za sekta hii ya uvuvi katika kitabu chake kazungumzia kwenye ukurasa wa 12 kifungu (e), kazungumzia kupungua kwa mapato ya bahari kuu kunakotokana na tishio la uharamia baharini. Sasa nikawa najiuliza huu uharamia, hata haujakuwepo uharamia hatufaidiki kitu, kwa hivyo huu uharamia umetuathiri nini sisi, kwa sababu kitabu kizima hiki hakioneshi tumepata nini.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nimebahatika haraka haraka kupitia Hansard ya Bunge ya tarehe 15/Juni/2011, alikuwa akijibu swali lililoulizwa na Mbunge kutoka Zanzibar Mhe. Thuwayba Idris, Mhe. Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi wa Jamhuri ya Muungano, naomba ninukuu kwa ufupi.

Mhe. Mwenyekiti, uvuvi wa bahari kuu uliingizia serikali mapato kutokana na ada za leseni za uvuvi na usajili wa meli zinazovua kwenye eneo husika. Katika

mwaka 2010/2011 ni mwaka mmoja tu Mhe. Mwenyekiti, jumla ya meli za uvuvi 71 zilisajiliwa na kukatiwa leseni za kuvua katika bahari kuu. Mapato yaliyopatikana ni jumla ya dola za Kimarekani milioni 2,074,400. Hata hivyo, katika miaka ya hivi karibuni uvuvi katika bahari kuu umeanza kuathirika kutokana na uharamia katika Bahari ya Hindi kama nilivyosema.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka Mhe. Waziri akija hapa anisaidie. Katika hizi dola milioni 2,074,400 sisi Zanzibar kwa mgao wa mfumo huu uliowekwa tumepata kiasi gani. Kama hazijatolewa kwa nini hazitolewi. Mhe. Mwenyekiti, nimeliuliza hili kwa sababu nilibahatika pia katika pitapita katika mtandao, kuona. Usinitizame sana Mhe. Mwenyekiti ndio namalizia, ndio nukta yangu ya mwisho hii.

Mhe. Mwenyekiti, nilipata kuona makala hii iliyoandikwa kuna blog moja inaitwa Zanzibar Islamic News Blog. Humu kuna taarifa iliyohusu ziara ya Kamati ya Fedha na Uchumi ya wakati huo, ikiongozwa na muadhamu Mhe. Salmin Awadh Salmin. Taarifa hii Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa ya tarehe 15/05/2010 kabla ya uchaguzi uliopita, inamnukuu Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini wakati huo, Mhe. Mussa Aboud Jumbe akisema Zanzibar haijajua hatima ya mafao yake, nanukuu Mhe. Mwenyekiti.

Zanzibar haijajua hatima ya mafao yake baada ya Serikali ya Muungano kuingia mkataba na meli za uvuvi za Hispania zenye thamani ya dola za Kimarekani laki 600,000 kwa mwaka. Hizo milioni 2 mbali hizo zilikuwa laki 600,000. Hata hivyo, alisema suala hilo bado linashughulikiwa na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira ya Zanzibar kwa wakati ule kwa kuwasiliana na Wizara ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji Tanzania Bara ili kujua mapato ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, sasa najiuliza, na kuna sehemu nyengine anazungumzia hapa, kauli hiyo ya Mkurugenzi Jumbe imekuja baada ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi Joahn Magufuli kutangaza kuwa Hispania imetoa zaidi ya dola laki 600 kwa ajili ya kuendesha shughuli za uvuvi wa bahari kuu kwa upande wa Zanzibar. Sasa Mhe. Mwenyekiti, najiuliza mapato hayo tunayopata halafu hayagawanywi na wawakilishi wako siku zote wamekuwa kidete. Mhe. Salmin Awadh hapa taarifa hii inamnukuu alipokuwa na kamati yake wakihoji suala hili, na mimi leo nalihoji.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri atuambie ndugu zetu wa damu wanavyotupenda wametusaidia kiasi gani katika mgawanyo huu. Suala hili naliuliza Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu nasikitika, nilidhani mimi hata lile jengo la makao makuu ya uvuvi wa bahari kuu pale Fumba, ambapo namshukuru Mhe. Waziri alinialika nikenda kushuhudia uwekaji wa jiwe la

msingi alipokuja kuweka Mhe. Rais wakati wa sherehe za Mapinduzi. Mimi nilidhani ile ni katika angalau uwekezaji wa Serikali ya Muungano katika suala hili, kumbe nimekuja kupekuwa vitabu nikaona kwenye hiki kitabu cha hotuba kuna jengo kutokana na fedha za *MACEMP* ambazo zinakuja kwa Zanzibar zinahudumia ujenziwa jengo lile. Sasa sisi Mhe. Mwenyekiti, tunafaidika nini katika masuala haya. Tukisema tunaonekana wabaya, lakini kila wakati najiuliza, kila sekta unayoigusa unajiuliza Muungano huu unatufaidisha nini sisi Wazanzibari Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba Mhe. Mwenyekiti, akija Mhe. Waziri anisaidie katika hili sana, sikusudii kuondosha kifungu chochote lakini nataka maelezo ya kina. Lakini ni mpaka lini Zanzibar tunaendelea kulea uoza huu wa upande mmoja wananufaika na sisi tunachumia ndugu tu, hufa maskini Mhe. Mwenyekiti. Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja na naomba nipatiwe maelezo ya kina, nakushukuru sana.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, na mimi Ijumaa hii na asubuhi hii kunipa fursa ya kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Kwanza napenda kuwapongeza kwa kuyaona maeneo mengi ambayo wamekusudia kuyafanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, mengi yameshazungumzwa lakini kila mmoja ana njia yake ya kuwasilisha imani yake. Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze kidogo kwenye suala la mwani na chaza mazao ya baharini. Hivi sasa Mhe. Mwenyekiti, wananchi wengi hasa wanawake wanajihusisha na upandaji wa mazao ya mwani pamoja na chaza. Kutokana na shughuli hiyo wengi wanajiona kwamba tunapata kipato, lakini nahisi kipato chao ni kidogo mno. Naweza kusema hii inatokana na mengi, haya makampuni ambayo yanakuja kununua huu mwani ndio wanaowafadhili wale watu wetu ambao wanazalisha ule mwani au wanapanda mwani. Sasa kwa vile wanatufadhili wao na bei nina imani kwamba watapanga wanayoitaka, kwa sababu Waarabu wanasema anayekufadhili anakuwa ni bwana wako.

Sasa mimi ningewaomba wizara wakaangalia, kama walivyofanya wizara ya biashara kuangalia bei ya karafuu ambayo hivi sasa Alhamdulillah tunashukuru, basi na wao wakaangalia kwa kina, je hizi bei huko ulimwenguni ndivyo zilivyo au hizi bei wanatupangia wao tu kwa sababu wameshakuwa wafadhili wetu, kwa hivyo wanapanga wanavyotaka wao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kijijini kwangu ninao wapandaji wa chaza, wapandaji hawa wamewezeshwa wamepewa kila kitu, lakini huyu mfadhili yeye anachokitaka katika hizi chaza, yeye anataka lulu. Sasa lulu hakuna hata mmoja anayejua soko lake liko wapi, ispokuwa ni yeye mwenyewe ndiye anayejua

soko iko wapi na bei ikoje. Kwa maana hiyo akija kununua kwa mwananchi anapanga bei anayoitaka, sisi hatujui chochote kuhusiana na suala lile.

Kwa hivyo, mimi naiomba wizara na hili nalo ikaliangalia kwa kina, Wizara ya Biashara,Viwanda na Masoko ina mpango wa kufanya *branding* katika suala la karafuu, basi na sisi tuende katika mfumo huu ili kuwahakikishia wananchi kwamba wanapata bei inayoridhisha, kwa bei ya 500 kwa mawazo yangu ni ndogo sana. Kwa sababu hizi Kampuni ukiangalia *activity* zao na jinsi wanavyotumia pesa basi utahisi kwamba zao hili lina bei kubwa huko nje. Kwa hivyo, hilo ndio ombi langu kwa wizara.

Nikitoka hapo Mhe. Mwenyekiti, niingie katika suala la uhifadhi wa maeneo. Hivi sasa Mhe. Mwenyekiti, wananchi wameshajihishwa katika kila eneo hili kuweka hifadhi maalum baharini. Ninacho kijua mimi ni kwamba wakihifadhi hii bahari inakuwa ni katika haya maeneo ya pwani, hizi sehemu ndogo ndogo yaani sijui ndio *territorial* au sijui zinaitwa vipi. Ni eneo ambalo wavuvi wetu wengi wanajishughulisha hapo, kutokana na kwamba tunawashajihisha waweke maeneo ya hifadhi, sasa kunatokea eneo ambalo la kuvua hivi sasa ni dogo kwa sababu wavuvi wetu hawawezi kuvuka hilo eneo la *territorial*, wanakuwa mara nyingi wapo hapa hapa na maeneo yote hivi sasa ni hifadhi, kwa hivyo itafika wakati wavuvi wetu watakuwa hawana pakuvulia kwa sababu maeneo yetu yote yatakuwa ni hifadhi.

Kwa hivyo, mimi ninamuomba waziri akaliangalia hilo. Hawa wawekezaji ambao ametutajia wanataka kuja kuwekeza basi wasije wakawekeza tu katika maeneo haya madogo madogo au wakatumia zana zetu ambazo tunazo sisi, au maliasili yetu tuliyonayo. Hivi sasa Mhe. Waziri, kumezuka wavuvi wengi sana kama ulivyotuambia katika taarifa zako na wavuvi hawa wanatumia rasilimali zetu sisi, ikiwemo miti. Sasa miti hii wanaiharibu, kuna uchafuzi mkubwa hivi sasa wa mazingira, kwa sababu wanaounda mashua wanatumia miti, wanaounda mitubwi wanatumia miti na vijana wengi wanaomaliza masomo hivi sasa ajira yao kubwa inakwenda kwenye uvuvi. Kwa hivyo, miti mingi hasa ya miembe na miti mikubwa inaonekana kupotea kwa sababu ya kukatwa na hawa wavuvi wetu. Kwa hivyo, mimi namuomba watakapokuja hawa wawekezaji basi wakaangalia mbinu nyengine ya kutafuta nyenzo za kuendea baharini. Hizi mashua za mbao zinatuharibia mazingira kwa sababu mikoko inakatwa kwa ajili ya kupata mataruma.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika suala hilo la uvuvi, hivi sasa kumekuwa na malalamiko mengi kuhusu kulinda maeneo. Yaani wananchi wanakuwa kijijini bila yao kujua kwamba eneo hili ni huru la kulimwa, lakini kwa vile mtu anatoka pengine Tumbatu anakwenda kuvua Jambiani basi haruhusiki hata kama eneo lile sio eneo la hifadhi, lakini kwa vile anatoka kule na anaonekana

atapata samaki wengi atavua, pengine na kusababisha bei pale kushuka basi anatakiwa aondoke na mara nyingi hii inatokea kwa jamaa zetu wa Kikojani. Wanapokuwa wanasafiri kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine, wanaonekana kama wao ni waharibifu wa wale samaki, sasa matokeo yake wanaambiwa aah! Ondokeni hatutaki muvuwe katika eneo hili. Kwa hivyo, hii inazua mgogoro, hivi sasa kunakuwa na migogoro kati ya wananchi, inazua uadui, watu wanaonekana adui kwa sababu wamekwenda kuvua.

Sambamba na hilo ni kuwa pia Mhe. Mwenyekiti, hata bei kwa sababu wao wanaweza kusema wamepata wale samaki lakini ikawa hawawauzi katika eneo lile, wanasema kuuza samaki wetu eneo hili bei yake inakuwa ni ndogo. Kwa hivyo, wanaondoka katika eneo lile wanakwenda kuuza kwenye eneo jengine.

Natoa mfano. Mvuvi kavua samaki Mkoani, akivua samaki Mkoani anaweza kuona aah! Bei ya Mkoani ni ndogo, kwa hivyo nakwenda kuuza Chake Chake. Sasa hilo linawakera wananchi kwa nini sisi tuliopo hapa katika kijiji hiki tusifaidike na hawa samaki halafu wanakwenda kuuzwa sehemu nyengine, matokeo yake wanazua sababu ya kuwaambia muondoke katika eneo lile msipate kuvua. Pia katika suala hilo, zile hifadhi ambazo zimewekwa za kuvua hazina alama maalum, kwa hivyo unamkutia mtu anakwenda kuvua lakini anaambiwa hilo ni eneo, lakini hakuna alama ambayo inaonesha kwamba hili ni eneo fulani limehifadhiwa. Sasa matokeo yake unawakuta wavuvi baharini wanapigana yale mapondo na mengineyo na inaendelea kusababisha kuwa ni ugomvi hivi sasa kati ya wavuvi wa sehemu moja na sehemu nyengine, kwa sababu hawataki kuingiliana katika maeneo yao. Huyu anasema ni langu, huyu anasema nyinyi msije na huyu anasema hivi. Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Waziri hilo uliangalie.

Mhe Mwenyekiti, jengine ambalo nataka kuzungumza hapa ni suala la majosho ya ng'ombe. Mhe. Waziri umetuambia na nashukuru kwamba josho kwa wilaya nzima ya Mkoani josho liko Kangani. Sasa Kangani mimi niliyekuwa Wambaa ni karibu kilomita 15, haitokuwa jambo la rahisi kuchukua ng'ombe wangu mimi nikampeleka katika josho lilioko Kangani kilomita 15. Kwa hivyo ningekuomba suala hili ukaliangalia na baadae ukatusambazia haya majosho sehemu mbali mbali. Au ukafanya utaratibu wa angalau wa kuwa na usafiri maalum wa kwamba ng'ombe akitokewa na matatizo ya kupelekwa kwenye josho, basi kuwe kuna usafiri ambao utaweza kuwasaidia wananchi kupeleka wanyama wao katika sehemu ile.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka kuzungumza ni suala la Kiwanda cha Uzalishaji Barafu kilichokuwepo Malindi. Hivi sasa wananchi wengi au wavuvi wengi huwa wanasafiri mpaka Tanzania Bara kwa ajili ya kutafuta barafu ya kuhifadhia samaki wao wanapokwenda bandarini. Lakini ninachokumbuka ni

kwmaba katika eneo la Malindi tulikuwa tuna kiwanda chetu kinazalisha barafu. Sasa sijui Mhe. Waziri utaniambia nini kuhusu kiwanda hiki, kimefikia hatua gani na hivi sasa kiko katika mkono wa na nina bado kiwanda hiki ni cha serikali au kiko katika mkono wa mtu binafsi na hakizalishi sijui kwa sababu gani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, naomba nimalizie hapo na kwa jumla naunga mkono. *(Mkofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujaahirisha kikao hiki cha sasa. Kesho Jumamosi tutakuwa tuna kikao hapa na keshokutwa Jumapili. Kwa hivyo, tumuombe basi Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ili aweze kutuelekeza utaratibu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kkkk imetimia na kwa kuwa mkutano wetu huu wa nne wa Baraza letu hili unaendelea kujadili bajeti ya Serikali ya Mapiduzi ya Zanzibar ya mwaka 2011/12, na kwa kuwa bado kuna wizara nyengine nne ambazo bado bajeti zake hazijawasilishwa na kujadiliwa na kupitishwa kwenye baraza hili. Kwa kuwa kuna kuna miswada ya kuidhinisha matumizi ya serikali ya mwaka 2011/12 na miswada mingine miwili kutoka Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Kwa kuwa tunakusudia kumaliza shughuli zetu zote za mkutano huu wa bajeti kabla ya kuingia kwa mwezi mtukufu wa Ramadhan.

Kwa hivyo, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu liendelee kukutana hata siku za mwisho wa wiki, yaani Jumamoti na Jumapili ya tarehe 23 na 24 Julai, 2011 na tarehe 30 na 31 Julai, 2011 ili tuweze kukamilisha shughuli za mkutano wetu huu wa bajeti kwa ufanisi mkubwa. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji basi wale ambao wanakubalia na hoja ya Mhe. Waziri wanyooshe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe, kwa vile wachangiaji bado tunao kumi ambao wanataka kuchangia katika hotuba hii. Sasa basi niwaombe Mhe. Suleiman Hemed Khamsi, Mhe. Rufai Said Rufai, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, Mhe. Asha Abdu Haji, Mhe. Ashura Sharif Aki. Waheshimiwa Wajumbe hawa wawahi kufika na mapema zaidi ili waweze kuchangia katika wakati wa jioni,

baadae tutaendelea na orodha nyengine ambayo itakuwa kama ilivyo, tutaangalia na wakati. Lakini tuhakikishe kwamba bajeti hii leo tunaimaliza. Baada ya maelekezo hayo basi

UTARATIBU

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Baraza lako tukufu, limekubali kuendelea na vikao siku za Jumamosi na Jumapili na kwa kuwa kanuni ya Baraza letu tukufu inataka vikao hivyo viendeshwe asubuhi mpaka saa 7:00 na saa 11:00 hadi saa 1:45 jioni. Kwa hivyo, naomba Waheshimiwa Wajumbe wakubali kuweka kanuni kando ili Baraza hili katika siku za Jumamosi na Jumapili lianze saa 3:00 za asubuhi hadi saa 9:00 na iwe ndio mwisho wa shughuli hizo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kwa vile hoja imetolewa. Sasa naomba kuwahoji Waheshimiwa Wajumbe, wanaokubaliana na hoja hiyo ya Mhe. Mjumbe wanyooshe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

Waheshimiwa Wajumbe, nachukuwa fursa hii kuliahirisha Baraza hili hadi saa 11:00 jioni leo.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Saa 6:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia katika Hotuba ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba tuko visiwa viwili ambavyo vimezungukwa na bahari, takribani tukiwagawa wananchi wetu tunaona kwamba wako katika makundi yasiyopungua manne. Kwa hivyo, ndani ya makundi ya nchi hii tumo wavuvi, wakulima, wafanyakazi pamoja na wafanyabiashara.

Lakini watu wetu wengi wamejikita katika kambi mbili, yaani kambi ya bahari na kilimo. Kwa hivyo, hivi sasa tutazungumzia kuhusu uvuvi wa bahari ambao

tunahamu nao tuuzungumze na kwa sababu ndio unaotusaidia katika kuleta uchumi wa nchi hii pamoja na kuleta maendeleo ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, katika uvuvi wa bahari tumegundua kwamba, uvuvi uliopo mkubwa hivi sasa ni uvuvi wa kutumia vyombo vidogo vidogo, ambavyo vyombo hivi vidogo kutokana na hawana uwezo wa kuweza kumiliki boti kubwa za kuweza kwenda masafa makubwa, basi inakuwa uvuvi wao ni wa maji kidogo, matokeo yake uvuvi wao unakuwa wa dagaa sana.

Kwa hivyo, si rahisi kwa wavuvi hao wa muda mrefu wameendelea kuvua samaki wadogo na ukawaambie wakavue samaki waliowengi, si rahisi kutokana na uwezo wao ni mdogo. Kwa maana hiyo, utakuta njia peke ya kuwaondoa hawa, ili wasiendelee katika uvuvi mdogo ni kuwezesha watu hawa wakaweza kupewa maboti makubwa, kwa ajili ya kuvua bahari kuu.

Mhe. Mwenyekiti, katika bahari yetu Mwenyezi Mungu aliyetujaali, kwamba hii ni rasilimali yetu ni muhimu sana tena hii tunao uchumi mkubwa sana, lakini bado serikali yetu haijaweza kuzingatia hali halisi ya rasilimali hizi zilizoko baharini.

Kwa mfano, katika bahari tunao samaki wadogo na wakubwa wenye thamani kubwa sana. Vile vile tunao pweza, kombe, ngisi, chaza na katika chanza inapatikana hata lulu ambayo pia ni rasilimali ikipatikana kwa nafasi nzuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, zaidi ya hayo tunapata kitu ambacho kimo na kama uzuri wa bahari, ambapo unafanya kama pambo la bahari na hayo ni matumbawe. Kwa kweli matumbawe hivi sasa watalii wanakwenda kuangalia na hayo ni yote katika kuleta maendeleo ya watu wetu. *(Makofi)*

Sasa bila ya kuwawezesha watu hawa wakaweza kuvua bahari kuu basi itakuwa ni uvuvi wetu huu mdogo. Kwa hivyo, ninamshauri Mhe. Waziri kwamba ajitahidi, ili kuweza kunyanyua uchumi wa nchi hii na kuwapa faida wananchi kwa kupata samaki wengi kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na wengi wa kuuza, basi ni lazima tujikite katika uvuvi wa bahari kuu. Hivyo, ninamshauri Mhe. Waziri aende mbio zake, ili suala hili tuweze kufanikiwa.

Vile vile nimwambie Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba aangalie hii bahari kama ilivyokuwa katika nchi kavu tunao askari wa kuilinda hii nchi kwa ajili ya kuleta usalama wa nchi hii, basi ni lazima na bahari tuilinde. Kwa kweli ndani ya bahari yetu kuna rasilimali za kutosha, hivyo rasilimali hizi hakuna mtu wa kuzilinda.

Kutokana na hali hiyo, basi ni vyema kujiandaa na wala si kwa hapa Unguja, isipokuwa ni eneo lote la Unguja na pamoja Pemba, kuona kwamba kuna watu wanaingia kinyume na sheria wakaingia katika nchi yetu na kuanza kuvua kwenye bahari yetu na kuchukua rasilimali za nchi hii.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri ajiandae angalau aweke ulinzi rasmi katika bahari yetu ya Zanzibar na hii itaweza kutusaidia. Hilo la kwanza.

Pili pia katika ulinzi huo kuna uvuvi mwengine ambao tunauita uvuvi haramu, basi ninamuomba Mhe. Waziri ajitahidi kuhakikisha kwamba huu uvuvi haramu hauna haja katika nchi yetu, kwa sababu hao wanatumia nyavu za macho madogo, hivyo wanavua samaki wa kubwa na wadogo.

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba ni muhimu kuona kwamba kwa hivi sasa idadi ya vyombo vya hao wanaovua samaki wadogo vimekuwa vingi pamoja na idadi ya wavuvi wamekuwa wengi sana. Kwa hiyo, ninamuomba Mhe. Waziri ni vyema kutoa taaluma ya kutosha katika uvuvi huo.

Suala jengine ambalo ni muhimu katika suala hili ni kuona pamoja na uvuvi huu wa dagaa ambao unavuliwa bado hakuna usalama wa dagaa ambalo linalovuliwa. Kwa kweli dagaa hili halijawekwa *scientifically* likaonekana kwa njia ambalo ni ya halali tena nzuri ya kuwalinda samaki kwa sababu hawa wanakuja kutumiwa na watu.

Kwa hivyo, hofu yetu ni kwamba kuna haja ya kuwa na ulinzi wa kutosha pamoja na utaratibu mzuri wa kuona kwamba, dagaa lao wanalovua na kuweka taratibu zote za kuhifadhi dagaa hili na njia nzuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, tusisahau kwamba hii bahari inatusaidia kuweka afya zetu, kwa sababu ndio tunapata samaki wa kila aina.

Suala jengine ambalo nataka nilizungumze Mhe. Mwenyekiti, nataka nimwambie Mhe. Waziri kuna suala zima ambalo limejitokeza hivi sasa ni kuhusu ukataji wa mikoko. Kwa kweli tukifanya hivyo tukakata mikoko ilioko pembezoni mwa bahari na tunaweza kusababisha athari mbili.

Hivyo, athari ya kwanza ni kwamba tunawakimbiza samaki maeneo yale na wala hawaishi tena wanakimbia, kwa sababu yale ni maficho pamoja na mazalio ya samaki. Kwa hivyo, hilo linatendeka na Mhe. Waziri hilo ulielewe.

Pili ambalo ni kubwa linatuathiri sisi wenyewe katika bahari usawa ni sawa na ardhi kama mikoko ile itakatwa basi maji yataingia ndani na iko mifano mingi

sana Mhe. Mwenyekiti katika nchi yetu maji yameshaingia ndani ya nchi.

Kwa mfano, Kisiwa cha Pemba kina *in and out*, yaani nje na ndani au *zigzag* nyingi sana na maji ya bahari yanaingia sana. Sasa katika zile sehemu ambazo zina usawa wa bahari na usawa wa ardhi uko sawa basi uwezekano wa maji kuingia katika ardhi upo kwa kiasi kikubwa.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwamba maeneo mengi ya Pemba na Unguja yanaingiza maji ndani ya ardhi yetu, hivyo hali hii inawasababisha wakulima washindwe kulima mipunga yao katika maeneo ya mabonde.

Mhe. Mwenyekiti, kama wananchi watapitiwa na kushughulikiwa wakapewa miche wakapanda kwenye maeneo yale ambayo mikoko imekatwa, basi nafikiri wao wenyewe watakuwa ni walinzi wa kuhakikisha kwamba mambo yale yasiendelee.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa muda wangu ni mdogo sana nina mambo mengi ya kuzungumza, lakini nitakwenda kwa haraka.

Suala jengine kuna hili Soko la Samaki. Kwa kweli namuomba Mhe. Waziri sisi katika Msuka tunalo Soko la Samaki, lakini bado halijamalizika. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri katika jitihada zake zote basi na hili suala kwa sababu tayari tumeshawahi kulizungumza asisahau kutoa mchango wake katika lile Soko la Msuka.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo mengine kuhusu mazao ya baharini. Kwa kweli mazao haya ya baharini kuna makundi ya wafugaji wengi na tumepewa taarifa hapa kwamba tayari wameshaanza kufaidika na ufugaji mdogo wa samaki, ufugaji mdogo wa kamba pamoja na mambo mengine mbali mbali watu wamo katika jitihada.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri katika kueleza fani hii ya uvuvi wa mmoja mmoja ambao ni uvuvi wa nje, basi wangeweza kupitiwa maeneo mengi kwa ajili ya kueleweshwa na kupata taalamu pamoja na njia za kutafuta nyenzo na mbinu za kuweza kuhifadhi vitu kama hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo nataka nilizungumze ni suala zima la uzalishaji wa chumvi kwa njia ya mioni ya jua. Kwa kweli watu wamo katika jitihada kubwa angalau mtu kupata chejio chake, yaani kupata chakula chake, kwa sababu watu wanajitahidi katika kufanyakazi, lakini ni lazima mkono wake mwananchi ni mdogo hivyo ni vyema au lazima mkono kwa serikali uingie.

Kwa mfano, tukiangalia ukanda wote wa Mashariki, yaani *Eastern Side of* Pemba *and Eastern Side of* Unguja ukanda ule ni mzuri sana kwa uzalishaji wa chumvi na watu wengi sana wanazalisha chumvi. Lakini tatizo bado serikali haijakaa sawa kuona namna gani tutaweza kuwasaidia hawa wazalishaji wa chumvi.

Kwa hivyo, ninamshauri Mhe. Waziri kwenye suala hili hebu tujipange vizuri kama vile ilivyokuwa mfano zamani *ZSTC* karafuu zetu tulikuwa tunawauzia wao, tuweke jumuia moja na tutafute wawekezaji wakae pahala pamoja na chumvi izalishwe na iweze kuuzwa ikiwa ni kampuni au shirika, ili sisi tutafute soko mahala pa kuuza, kwa sababu bahari tunayo na chumvi tunayo kwa nini tusiitumie bahari hii kwa ajili ya kuzalisha chumvi.

Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri afanye kila jitihada ya hao watu wenyewe vikundi mbali mbali wanaozalisha chumvi waweze kusaidiwa na kuweka shirika moja kubwa la kuweza kuuza mali zetu tunazozizalisha.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hilo nataka niendelee katika suala zima la hawa wakulima wa mwani. Mhe. Mwenyekiti, nimepata taarifa kwamba ukulima wa mwani unaendelea vizuri na ni kweli maeneo yetu yote ya Pemba na Unguja watu wanazalisha mwani.

Lakini uwezo wa watu wetu ni mdogo na wanahitaji kama ni Waziri basi kuweza kuwapitia watu hawa na kuweza kuwapa nyenzo hata kwa njia ya kukopeshwa, ili waweze kujiendeleza. Kwa hivyo, pia tunashukuru kwamba bei kidogo kutoka shilingi 200 imepanda mpaka shilingi 400 na ninaamini baada ya muda si mrefu tunaweza kupata bei nyengine.

Nikiondoka hapo kuna suala jengine ambalo nataka nilizungumzie kuhusu ufugaji wa ng'ombe. Mhe. Mwenyekiti, *traditional* watu wa nchi hii ni wafugaji tukitaka tusitake, lakini uwezo wa kufuga ni mdogo pamoja na utalaamu wa ufugaji ni mdogo.

Kwa kweli ng'ombe wanaofugwa katika nchi hii ni *more less traditional* ni za kikale au kiasili, ambazo kwa uchunguzi tumeona kwamba ng'ombe hawa wanaofuga watu wetu ni ng'ombe ambao uwezo wao katika kuzalisha ni mdogo sana, yaani lita moja mpaka lita moja na nusu. Mhe. Mwenyekiti, mtu anahangaika mchana kutwa kufuga ng'ombe hata jioni akikamua maziwa analita moja na nusu.

Sasa si vibaya kuwa na *traditional cows*, yaani si vibaya kuwa na ng'ombe wa kiasili kwa watu wetu ndio waliozoea. Lakini tuwatoe katika ule kikalia muda mrefu mapato yao ni madogo na tuwaingize katika kufuga wanyama ambao

wanaweza kuzalisha maziwa mengi. Vile vile wengine *multi purpose*, yaani unaweza ukachinja au ukakamua maziwa.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri hapa bado, isipokuwa nasema namshukuru Mhe. Waziri kwamba yeye bado ni mpya katika wizara hii na wizara yake ameichukua hivi karibuni. Kwa kweli anajitahidi sana na watendaji wake wote wanajitahidi kuangalia hili suala, lakini uwezo ni mdogo na fedha aliyoipata ni ndogo. Lakini pamoja na hayo kwamba fedha aliyopata ni ndogo, hivyo ajitahidi na sisi tutampigia debe baadaye kuona na yeye anapata fedha za kutosha.

Hivyo, suala la kuwezeshwa wananchi katika kutafuta ng'ombe bora ambao wa kuweza kuzalisha maziwa. Mhe. Mwenyekiti, tunajua kuna maeneo mengi tu kule Pemba pamoja na hapa Unguja watu wamekaa kwa makundi, lakini rasilimali ile inaonekana kwamba watu ni wengi na wanyama walionao ni kidogo na wala haitoshelezi kwa kuzalisha.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri kwenye suala hili la ng'ombe ili tuwatoe kule katika uzalishaji ule tuwapeleke kwenye uzalishaji mkubwa. Mhe. Mwenyekiti, nashauri kwamba watu hawa wakawezeshwa na kupewa ng'ombe waliokuwa wazuri.

Vile vile katika hii *crossbreed* tuangalie kuna mambo mengi yanajitokeza kama hawa ng'ombe *traditional* wanao uwezo wa kuweza kustahamili kupe ambao ni wabaya sana kwa kuwatia homa ng'ombe. Hali kadhalika kama tutafanya *crossbreed* kwa kuchukua ng'ombe kutoka Tanzania Bara tukawaletea wananchi kwa sababu ya kuwa watapa maziwa lita 15 mpaka 20, basi ni lazima ng'ombe hawa waweze kuhifadhiwa kwa madawa.

Kwa hivyo, ninachokisema katika suala hili ni madawa ni ghali na watu wetu wengi wanashindwa kununua madawa haya na kila siku madawa yanapanda bei. Hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwa kuwa hawa ni wanyama na kuumwa wanawajibika, homa wanazipata kutokana na homa zao zinazoitwa *ECS*, yaani homa kali sana na mnyama anapunguza uzalishaji wakati anapopata homa, hata hawa ng'ombe wa asili wakipata homa kama vile kupe wengi, basi wanapunguza uzalishaji.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri jitihada moja kubwa kuhakikisha kwamba madawa angalau bei kidogo zinateremka chini, ili wafugaji wetu waweze kuwahudumia hawa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, zingatia muda.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, tayari namalizia. Kwa kweli suala jengine ambalo naomba tulikuwa na kitu ambacho tukiita zamani majosho ya kuoshea ng'ombe. Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri zile shughuli za asili tusiziwache, kwa sababu mimi nakumbuka mara nyingi watu wetu wenyewe tayari wanakuja na ng'ombe wao na wanalipa au wanatoa ada katika shughuli zile.

Kwa mfano, tukaweka sehemu moja kubwa tukaleta ng'ombe wote kama Kaskazini au kwengineko kwenye ng'ombe wengi tukaweka sehemu ile maalum kwa ajili ya kukosha ng'ombe wao, nadhani watapungua maradhi ya kupe. Kwa hiyo, hilo ni jambo zuri Mhe. Waziri na ninaomba uliweke kwenye mazingatio, ili watu wetu waweze kufaidika.

Mhe. Mwenyekiti, naheshimu wakati wako na ninakushukuru. Hivyo, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Konde naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Mwenyekiti, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa jioni hii kwa kunijaalia kupata nafasi hii adhim nikaweza kusimama kwa ajili ya kutoa mchango wangu mdogo katika Hotuba ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa mzima wa afya na kuweza kutoa mchango wangu huu.

Pili nimpongeze Mhe. Rais kwa kuona kwamba Zanzibar ni visiwa. Visiwa ambavyo vimezungukwa na bahari ya maji ya chumvi, ambapo bahari hii imejaa samaki pamoja na mambo mengine mbali mbali ambayo inaweza kuwa ni tija kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu kuhusu suala la ufugaji wa ng'ombe. Kwa kweli tunao ng'ombe wa aina mbili, yaani tunao ng'ombe wetu wa kawaida wanaopatikana hapa Zanzibar na huo mtaji ulioingia wa ng'ombe wa kisasa wa maziwa.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani kwamba hawa ng'ombe wetu wa Kizanzibari hawa bado wanao uwezo wa kuzalisha maziwa mengi na nyama nyingi. Lakini wananchi wetu bado hatujawalenga kwamba hii ni idara ambayo inaweza kujitosheleza kwa mawiza na kitoweo.

Kwa mfano, ukimchukua ng'ombe chotara huduma zake anazozipata na kama tutawalazimisha wafugaji wakawapa ng'ombe wetu wa Kizanzibari kama

huduma anazozipata ng'ombe wa chotara basi nadhani tunaweza kuvuna maziwa sawa sawa, sasa kinachokosekana ni hii taaluma tu.

Kwa hivyo, bado ng'ombe wetu wa asili wanao uwezo wa kuzalisha maziwa na nyama kwa kiwango kikubwa, basi nafikiri kama wafugaji tutawaelekeza vizuri basi upo uwezekano wa kupata maziwa ya kutosha.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, katika ufugaji wa ng'ombe wa kisasa nadhani kipindi kilichopita tulikuwa na Mradi wa *PADEP*, lakini wafugaji wengi wamepoteza nguvu zao nyingi na ng'ombe hao walioletwa na ndugu zetu wa *PADEP* wafugaji wamekula hasara kubwa sana. Kwa mfano, katika jimbo langu kuna vikundi mbali mbali ambavyo vilikuwa na mradi huu, lakini ng'ombe hawa kutokana na hali ya hewa ya Pemba na huko walikotoka ikawa ni dhaifu.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani na hata hawa ng'ombe walioletwa hapa Zanzibar kwa kweli sio ng'ombe bora, kwa sababu kuna ng'ombe wa maziwa *special* na ng'ombe machotara. Kwa hivyo, ndugu zetu wanapokwenda kule wanachukua tu ng'ombe na ng'ombe wengine kule hawafungwi, yaani wanaingizwa katika makundi na kuchungwa.

Lakini wakati anapotolewa kule na kuletwa hapa, basi mfugaji analazimishwa amjengee banda na wala asipigwe na mvua na abakie katika hema lile, sasa kubakia mule wakati ni mambo aliyoyazoea, basi ng'ombe yule anaanza kupata athari ya kuathirika na hatimaye kupoteza maisha.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini nikasema wale walikuwa si ng'ombe bora, kwa sababu wale ng'ombe walikuwa ni ng'ombe matumbo si nyama. Kwa hivyo, malisho yanakuwa makubwa sana kuliko ile tija itakayopatika kwa yule mnyama wenyewe. Kwa hiyo, hili nalo likawa ni pingamizi kubwa sana, yaani wakawa wanalisha sana, lakini mapato madogo.

Kwa hivyo, naomba nimueleze Mhe. Waziri kwamba hapo nyuma hii ilikuwa ni idara tu, lakini sasa ni Wizara nzima ya Mifugo na Uvuvi. Kwa maana hiyo, Mhe. Rais ameona kwamba itakapokuwa hii ni wizara basi kuna matarajio makubwa kwa wananchi pamoja na nchi kwa jumla kufaidika na huu ufugaji.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumshauri sana Mhe. Waziri kukaa na wataalamu wake na kuangalia mbegu ambazo ni bora na wala sio ubora wa ng'ombe na badala yake wawe ng'ombe bora, ili wafugaji wetu waweze kufaidika na mpango huu wa ufugaji.

Vile vile kuhuhsu hawa madaktari wanaowatibu hawa wanyama, ninamuomba sana Mhe. Waziri kwani wengi wao ni watu ambao wameshakuwa na muda mrefu kazini na pengine hawajapata mafunzo kwa muda mrefu, pia makongamano mbali mbali pamoja na semina kwa ajili ya kuongeza ujuzi wao.

Kwa hivyo, namuomba sana afanye jitihada za kila hali ili wataalamu wetu hawa waweze kuongeza ujuzi, ili wafugaji wetu waweze kufaidika na taaluma watakayoipata kwa hawa madaktari wetu. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu ufugaji wa kuku. Mhe. Mwenyekiti, Wazanzibari wengi wa mashamba na mjini wanapenda sana kufuga kuku, lakini wengi wao wanafuga na wala hawana taaluma. Kwa kweli kitu chochote kile utakachokifanya kama huna ujuzi nacho, basi itakuwa ni sawa na kuchukua tambara kwenda mtoni na kufua au kukosha. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ninamuomba sana Mhe. Waziri awatafute sana wafugaji hawa, yaani wapitiwe sana kwa ajili ya kupata taaluma na kile wanachokifanya basi waweze kukifanya kwa uhakika na kinyume na hivyo, itakuwa serikali pengine inatoa vifaranga, lakini faida kwa mfugaji ikawa haipatikani. Sasa itakuwa Mhe. Rais ameweka wizara ya ajili ya kuisaidia nchi na hatima yake ikawa nchi nido inakwenda chini.

Hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri viorodheshwe vikundi hivi vya wafugaji wa kuku, mbuzi, ng'ombe, ili wapatiwe taaluma kwa kupitia mafunzo mbali mbali kwa ajili ya kuendeleza huu mtaji ambao lengo lake ni kuweza kuwasaidia katika maisha yao ya kila siku. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo sasa nizungumzie kuhusu mazao ya baharini, tunayo Idara ya Mazao ya Baharini. Kwa kweli kwanza nataka niwapongeze sana vijana wetu hawa wa Idara hii ya Mazao ya Baharini hasa wale ambao tumeshashirikiana kufanya kazi hii kule Pemba. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimueleze Mhe. Waziri kwamba anao vijana wenye uwezo kabisa, ubunifu wa kutosha pamoja na kupenda kujituma, kwa sababu mimi mwenyewe binafsi nimeshawahi kutoka nao na kwenye maeneo mbali mbali baharini na ninawaona ule ujarisi wao walionao. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ni vyema wizara kujitoa ofisini ikenda kwa walengwa kama hawa vijana wanavyojitolea, kwa ajili ya kuimarisha uchumi pamoja na Idara ya Mazao Baharini iweze kuendeleza haya mazao, basi taasisi zetu hizi ni kufanyakazi kikamilifu na kuwafikia walengwa.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwamba kwa awamu hii ya mwanzo ya vijana hawa 30 watakaokwenda China na mimi ni mmoja nimefaidika katika Jimbo langu la Tumbe, tena huyu ni miongoni mwa hawa wanaoanzisha hizi shamba za kufuga samaki, kamba pamoja na mambo mengine. *(Makofi)*

Kwa hivyo, yote hayo yasingepatikana kama hawa vijana wa Idara hii ya Mazao ya Baharini kama hawakuwa katika harakati hizi za kuitaka wizara ifanikishe, basi na sisi tungekuwa hatuna watu kama hao na ingekuwa ni sehemu nyengine tu. Lakini nashukuru kwamba kwa Pemba nzima hawa vijana wametembea na wanawapa wananchi wetu ujuzi wa kuweza kufuga samaki pamoja na mambo mengine.

Hivyo, sina budi kumshukuru Mhe. Waziri katika kuhamasisha kwake na Jimbo la Tumbe likabahatika kutoa mwananchi wetu mmoja huyu kwenda kujifunza kwa ndugu zetu wa China. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa nizungumzie kuhusu suala la uvuvi. Kwa kweli kuna uvuvi wa kienyeji ambao tuliourithi kutoka kwa mababu zetu na uvuvi wa kisasa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, zimebakia dakika mbili.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru. Kwa hivyo, uvuvi wa kienyeji ndio uvuvi ulioenea sana hapa Zanzibar na uvuvi huu ni kwamba kwa sasa hauwaletei tija wavuvi wetu. Kutokana na hali hiyo, naishauri sana wizara ndani ya upya wake pamoja na kunung'unika sana hapa Wajumbe kwamba fedha ulizoingiziwa ni kidogo, lakini pamoja na udogo, nadhani serikali inaitizama wizara itafanya nini, je hiki tulichowaingia kitafanyakazi au vipi.

Kwa hivyo, nadhani kwa kuwa vijana wale ni mahiri basi wataweza kuzitumia fedha hizi vizuri, isipokuwa naiomba Wizara ya Fedha wawawezeshe wenzetu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ili waweze kuendesha shughuli hizi kwa ajili ya kuwatoa wavuvi wetu katika uvuvi wao waliouzoea zamani na kuhamia kwenye uvuvi wa kisasa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na muda haupo, lakini nilikuwa nimejipanga vizuri kwa ajili ya kutoa maoni yangu katika wizara hii, sasa dakika mbili ndio zimekwisha hizo.

Kwa hivyo, mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Tumbe tunaiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba hii ya mkwe wangu Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Lakini kabla ya kuendelea namuona Mhe. Waziri, Katibu pamoja na Mkurugenzi wake nadhani walikuwa wakiomba dua, ili hotuba yao ipitishwe kwa mara moja tu, kwa sababu wote wamenyanyua mikono kwa ishara ya kuomba dua, kuna picha kwenye *caver page* ya kitabu cha hotuba ndio inayoonesha hivyo.

Mhe. Spika, mimi nije kwenye mafanikio ya kwenye sekta ya mifugo kwanza nataka niipongeze sekta hii kwa kupata mtambo wa upandishaji ng'ombe wa sindano, mtambo ambao kwa muda mrefu ulikuwa unashindwa kuzalisha mbegu za ng'ombe kutokana na mtambo huo kuharibika. Nataka niwapongeze kwa kupata mtambo huu kwa juhudi zake Mhe. Waziri pamoja na serikali nataka niwaponge ili kuendeleza uzalishaji wa ng'ombe wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa sita kwenye changamoto, hapa nimpongeze tena Mhe. Waziri kwa kukubali kwake kwamba sekta hii ya mifugo imekabiliwa na changamoto kubwa juu ya mifugo, zikiwemo changamoto na uhaba wa nyenzo kama alivyozitaja kwenye ukurasa huu wa sita kifungu namba 2 (1) 3 nakubaliana nae kwamba uhaba huu wa nyenzo ni kweli kwa wafagaji wetu, wana uhaba wa nyenzo kama vile vitendea kazi na elimu kwa wafugaji. Hili ni tatizo kubwa sana kwa kiasi ambacho wafugaji wetu hasa vijijini kurudi nyuma kutokana na elimu hii ya wafugaji.

Lakini vile ile Mhe. Mwenyekiti ndicho kinachowafanya wananchi wetu kutokuendelea na shughuli zao kwa ujumla, kwa hivyo basi namuomba Mhe. Waziri afanye juhudi na bidii kubwa kuweza kuzitatua changamoto hizi kwa wananchi wetu hawa, lakini nikija kwenye hii Idara ya Mifugo. Mhe. Mwenyekiti ingawa umesema muda ni mdogo lakini na mimi nitaomba niendelee kidogo tu kwenye Idara ya Mifugo, Mhe. Mwenyekiti asilimia kubwa ya Wazanzibari hutegemea mifuto ikiwemo kuku, ng'ombe, kondoo na mbuzi sekta ambayo inaathiriwa sana na wezi sekta hii inaathiriwa na wezi hasa wa ng'ombe.

Je, Mhe. Waziri haoni kama kuna haja ya kuweka utaratibu wa kurekebisha uchinjaji wa ng'ombe, ili kukimbiza wimbi hili la wizi wa ng'ombe uchinjaji wang'ombe hasa Kisakasaka lakini bado zipo sehemu nyengine ambazo wachinjaji wa ng'ombe huchina kwa kisiri siri sehemu hizo ambazo sio za kihalali.

Mhe. Waziri haoni kama kuna haja ya kupiga marufuku nyama zote zinazoletwa sokoni, ambazo hazina vibali maalum kwa matumizi ya binaadamu Mhe. Mwenyekiti, vile vile namuomba Mhe. Waziri nyama hizi zitakapoletwa sokoni ahakikishe kwamba zina kibali maalum kilichothibitishwa na wahusika.

Mhe. Mwenyekiti sasa nije katika ukataji wa mikoko ukataji wa mikoko katika fukwe zetu ni moja yaathari zinazoharibu mazingira na pia kupanda kwa maji ya bahari ambayo hayana kizuizi, pia kuleta mmong'onyoko wa ardhi hii ni athari kubwa sana Mhe. Mwenyekiti, watu wetu bado hawajakuwa na taaluma ya elimu hasa ya ukataji wa mikoko na zaidi watu wetu wa mwani. Na hili pia nimwambie Mhe. Waziri apate vifaa maalum ambavyo ni page za kupandia mwani la si hivyo mikoko itamalizika na athari zake baada ya muda mfupi tutaona.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nije katika hawa wafugaji weu wa ng'ombe kule kwetu ninao wafugaji ambao hivi sasa wana matatizo makubwa sana kuhusu ng'ombe hawa wanaoita machotara, lakini nasema Mhe. Mwenyekiti hawa sio ng'ombe wa machotara wametuletea wananchi wetu ng'ombe waondoe umasikini, lakini bado wamewaletea kuweka zaidi umasikini sio kuondoa umasikini lakini kuzidisha umasikini kwa sababu ng'ombe hawa mmoja kwa kutwa anakula poli sita za majani. Ngombe yule anapozaliwa aidha hufa mama au hufa mtoto mimi namuomba Mhe. Waziri aje Kangani aje aniulize au nimpeleke kwanye wafugaji hawa awaulize wafugaji wangapi walipata ng'ombe wake mmoja tu wa uhakika, hayupo hata mmoja.

Aidha ng'ombe akizaliwa anakufa mama au anakufa mtoto na hivi sasa Mhe. Mwenyekiti wamekuja na jambo jengine jipya wanapiga, halafu isitoshe vile vile wanapozaa watoto huwala, kwa hivyo naomba Mhe. Waziri uje na wahusika wako ili kuwapa elimu watu hawa ya nini maana ya ufugaji hili ni tatizo kubwa Mhe. Mwenyekiti.

La mwisho Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye matumbawe ni pambo la bahari na vile vile matumbawe ni nyumba za samaki, kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri afanye bidii yote ili kuleta video au senema kuonyesha watu nini athari za ukataji wa matumbawe baharini. Mhe. Mwenyekiti, matumbae ndio yanayoficha samaki, matumbawe nip ambo la bahari ikiwa hakuna matumbawe samaki wengi tutawakosa. Mimi namuomba Mhe. Waziri aje na video katika sehemu za vijijini ili kuonyesha nini athari za matumbawe.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo naomba nisipoteze muda wako naunga mkono hoja. Ahsante.

Mhe. Asha Abdulla Haji: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema na kutufikisha hapa, pili napenda kukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii jioni hii na tatu napenda kumshukuru Mhe. Waziri na watendaji wake kwa kuleta bajeti yao hapa.

Mimi nitaingia kwenye sekta ya uvuvi kwa kuwa mwani ni zao kubwa wananchi wanalipenda sana hususani wanaweke, tunaipongeza sana wizara yako kwa kuongeza bei zao hili bado bei hii haijatosheleza kutokana na zao hili kuwa na kazi kubwa na wanawake ndio wenye kufanya kazi hii, kazi hii ni ngumu kutokana na kazi yake zao hili bei haijatosheleza kabisa, ningemuomba Mhe. Waziri wakati anaijua wizara hii ugumu wa kazi hii ni mkubwa. Ningemuomba Mhe. Waziri afanye kila jitihada aongezee bei angalau kilo moja shilingi elfu moja.

Mhe. Mwenyekiti, ningekuomba wizara yako ione bei hii kutokana na ugumu wa zao hili wanawake hivi sasa ndio zao lao kubwa kwenye kando kando za bahari. Mhe. Mwenyekiti, ningekuomba zao hili hivi sasa ndio baba watu wanapanda kwenye maji mengi ningeomba wizara yako itupatie boti na vifaa angalau wale wanawake wanaokwenda kwenye maji mengi wapande lile bodi, na wanavyovuna vile vile waingize kwenye boti lile.

Mhe. Mwenyekitiki, ningeiomba wizara yako ione suala hili iwapatie vifaa na bodi ili warahisishe zao hili la mwani.

Sasa naingia kwenye sekta ya uvuvi kwa kuwa bahari yetu ni kuu lakini hatuna dhana za uvuvi ningeiomba Wizara yako itupatie zana za uvuvi kwenye bahari kuu ili wananchi wapate rasilimali kwenye bahari kuu, naiomba wizara yako ilione hili wapatiwe wananchi vifaa vya uvuvi, maboti, nyavu, ndoana kubwa za kuvulia samaki wakubwa.

Mhe. Mwenyekiti sasa nakuja suala la ufugaji kule kwetu Jambiani kuna ufugaji wa mbuzi, lakini mbuzi wale walioletwa kule sio mbuzi bora hawazai watoto wengi hawatoi maziwa mengi, ningeomba wizara yako ilione suala hili utupatie mbuzi bora wenye kuzaa watoto wengi na wenye kutoa maziwa mengi.

Jengine kuna tatizo la bahari kwa watu wa Muungoni na Uzi tatizo hili sijui wizara yako inajua au haijui, ikiwa unalijua ningekuomba tatizo hili ulitatue mara moja kabla hakujatokea athari yoyote. Kuhusu wapandaji wa mwani. Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi naunga mkono hoja mia juu ya mia.

Mhe. HIja Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na najua muda ni mchache sana kwa hivyo nitachangia kwa

kifupi naomba univumilie angalau dakika kumi na tano, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa jinsi alivyotuletea hotuba yake nzuri iliyoandikika na iliyojaa mahesabu.

Mhe. Mwenyekiti mimi nianze na kituoa cha uvuvi kwa haraka haraka na nimwambie tu Mhe. Waziri kwamba sekta hii kwa Zanzibar ni muhimu sana kama alivyotueleza kwamba ni sekta moja ambayo inatoa mchango mkubwa kwenye pato la taifa, kwa ongezeko la samaki na wavuvi wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tukubali kwamba sekta hii ni changamoto kubwa kwa wavuvi wetu na changamoto ya kwanza ambayo wenzetu wanaipata ni ukosefu wa vyombo vya kuvulia kupitia kwenye bahari kuu, Idara ya uvuvi iliyopita kwa kweli imefanya kazi kubwa ya kugawa vyombo vya wavuvi pamoja na mashine yake ingawa niseme tu kwa bahati mbaya sana walengwa waliokusudiwa sio waliopewa vyombo vile, tutaendelea kujenga hoja hii kwa sababu sisi ndio tunaoishi vijijini na ndio tunaoona nani waliopewa mashine zile.

Mhe. Mwenyekiti namshukuru sana Mhe. Waziri kwa sababu alifanya ziara Mwambe aliuona mgongano baina ya kamati ya sheha na wavuvi kwamba boti ilienda kwa kamati ya sheha na wavuvi sio waliopewa boti ile, kwa hivyo kigezo kile sio Mwambe tu lakini kwa Zanzibar nzima kwamba sio wavuvi waliopewa boti zile. Kwa hivyo Mhe. Waziri akifika hapa namuomba anieleze ametoa boti kwa Zanzibar na walengwa ni wangapi na ngapi hadi leo ziko hai bado hazijauzwa.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo changamoto inagusa ni mitaji nadhani serikali kama inakusudia kuwasaidia mbali ya kuwapatia vifaa vya uvuvi pamoja na maboti lakini nadhani serikali ingeangalia uwezekanzo wa kuwapatia mitaji vile vikundi ambavyo vinashiriki na shughuli za uvuvi, Zanzibar sasa hivi inakabiliwa na wimbi kubwa na ajali za baharini kwa wananchi wetu ambao wanavua, takribani kila mwezi wavuvi wanapotea kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo na upepo na ajali ambazo wanazipata na samaki. Ushauri wangu ni kwamba nadhani Wizara hii ingewaandalia bajeti ya bima ya ajali za baharini pamoja na kuwapatia mfuko maalum wavuvi ambao utawasaidia pale watakapopata athari mbali mbali .

Mhe. Spika, labda niseme tu kwamba Mhe. Ismail Jussa Ladhu asubuhi alizungumzia mapato ya bahari kuu, tuliwahi kusikia tu mwaka juzi kwamba Tanzania kupitia Waziri wa Maliasili Mhe. Magufuli ilikamatwa meli kubwa pale ya samaki ambao ilituibia na ilikuwa ikiendesha kesi mbali mbali lakini nasikia kesi imemalizika, naomba kujua Zanzibar tumeingia hasara vipi au tumefaidika vipi kutokana na samaki wale waliovuliwa bahari kuu ambapo

Zanzibar ni sehemu ya hiyo bahari kuu.

Mhe. Mwenyekiti jengine kwenye bahari kuu naomba kujua tu yale mapato ambayo Mhe. Ismail Jussa Ladhu ambayo ameyagusia asubuhi asilimia yetu 40 hadi sasa tumepata shilingi ngapi kwa maslahi ya Wazanzibari na kwa maslahi ya wananchi wetu.

Jengine ambalo ningelisema haraka haraka ni suala al mradi wa *MACEMP* kwa kweli umefanya kazi nzuri hapa Zanzibar, lakini tumegundua kwamba kulikuwa na matumizi ambayo yalikuwa na wasi wasi hasa kwa wenzetu wa Benki ya Dunia, tumeona baadhi ya nyaraka mbali mbali ambazo Benki ya Dunia hawakuridhika na matumizi ya fedha zile. Kwa mfano kulikuwa na manunuzi ya gari iliyonunuliwa kwa dola 40 na mia kidogo hivi benki ya Dunia walikataa matumizi yale na kuomba serikali ilipie fidia ile, taarifa ambazo zipo serikali ililipia matumizi yale kwa hivyo naomba matumizi yale yalikuwaje na je Serikali ilipie suala hilo kiasi gani.

Mhe. Mwenyekiti jengine ambalo ningetaka kuligusia ni suala zima la machinjio Kisakasaka, Mhe. Waziri hapa ametwambia ana mpango wa kuendeleza machinjio yale katika hali ya ubora zaidi, taarifa ambazo ninazo ambazo nimefuatilia leo ni kwamba machinjio yale ukweli yako katika hali mbaya sana, machinjio yale hakuna hata daktari pale kama mtu mmoja atapata athari ya kuumia au kupata homa basi nadhani tunaweza kumpoteza kwa sababu hakuna daktari, daktari pale aliyepangwa kwa bahati mbaya hana usafiri kwa hivyo unapopata ajali au unapokuwa na haja ya kuchunguza nyama ya ng'ombe basi lazima daktari yule mpelekee gari ili aje afanye uchunguzi wa nyama ile ya ng'ombe.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani kama kweli tunajali afya za wananchi wetu basi lazima daktari yule apatiwe gari kwa ajili ya kukaa *stand by* kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa nyama za ng'ombe. Lakini mbali na hilo nimegundua kwamba Kisakasaka wanaingia ng'ombe si chini ya mia mbili au mia tatu kila jumamosi na nilifanya utafiti kwamba kila ng'ombe mmoja Wazanzibari wanamlipia shs. 5,500 sasa ninapoambiwa kwamba pale hapana huduma ya maji, ninapoambiwa kwamba pale hapana huduma ya *first aid* napata mashaka kujua kwamba fedha hizi ambazo zinaingia ni kiasi gani kwa mwezi, baya zaidi fedha hizi ambazo zinaingia pale Wazanzibari hawa hawapewi risiti ambayo inakubalika na serikali, wanatoa risiti ya mchele risiti ambayo lazima itapoteza mapato ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kujua kwamba kwa kuwa pale kila jumamosi wanaingia ng'ombe mia mbili mpaka mia tatu, Je, Mhe. Waziri atanieleza mapato gani yanapatinana Kisakasaka na Zanzibar inaingiza shirilingi ngapi

kwa mchango huu wa machinjio ya ng'ombe ndani ya mfuko mkuu wa serikali.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa wajumbe tusubiri kidogo tunabadilisha mitambo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Kwa hivyo Wazanzibari wanapohoji mapato yanayotokana na Muungano ni kwa lengo la kuondosha kadhia kama hii, nimesema KIsakasaka ni mia mbili mpaka mia tatu kwa kila Jumapili au Jumamosi, sasa Mhe. Waziri akija hapa aniambie mapato ambayo yanapatikana ili tuweze kuyajua.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka kuhoji Zanzibar kupitia mradi wa *MACEMP* tulifadhiliwa dola milioni moja kwa ajili ya kujenga soko hapa Mjini Zanzibar, fedha hizo ziliingia Zanzibar lakini hadi leo hatujapata maelezo kamili tulisikia kwamba Zanzibar imepata kiwanja cha kujenga soko hili kwa hivyo naomba dola hii milioni moja iliyoingia kwa ajili ya kujenga soko kwa msaada wa *MACEMP* wapi wamefikia ili tujue maendeleo ya pesa hizi. Mhe. Waziri ukija hapa naomba ufafanuzi wa kutosha kwa nini tunafadhiliwa dola miliono moja kwa ajili ya kujenga soko la samaki hapa Zanzibar lakini hadi hii leo tumeshindwa eneo lwa kujenga soko hilo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka kuhoji nimefanya utafiti kuona kwamba wizara hii ina shamba la mifugo Donge Mchangani shamba ambalo lilikusudiwa kuendeleza hii sekta ya mifugo, taarifa ambazo zipo shamba hili halifanyi kazi na lipo mikononi mwa mtu binafsi. Mhe. Mwenyekiti naomba kujua shamba hili baada ya serikali nani amelihodhi nasikia huyu aliyelihodhi sasa anafanya biashara ya kulima viazi. Sasa Mhe. Mwenyekiti, Wazanzibari wana haja ya mifugo sera ya taifa ya kilimo haijazungumzia habari ya viazi inazungumzia samaki na mifugo, leo tunasikia kwamba shamba hili kubwa ambalo ni mali ya serikali yupo huyu mwenzetu anapanda viazi kwa maslahi yake binafsi.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti namuomba Mhe. Waziri aniambie shamba hili la mifugo la Donge Mchangani nani aliyemiliki badala ya serikali, na kwa nini kulimwe viyazi badala ya kuwekwa mifugo kwa ajili ya kupata nyama za ng'ombe na mbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa niseme tu kwamba hii bajeti ilivyoandikwa ni nzuri, lakini iwapo mwenyekiti atatujibu itakuwa nzuri na akishindwa kujibu itakuwa mbaya kuliko zile mbaya. Mhe. Mwenyekiti naomba kufikia hapo.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kuweza kuchangia na nakuahidi kwamba dakika ulizonipa nitazitumia

vizuri, awali ya yote nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia pumzi ya kuweza kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu, lakini pia nichukue nafasi hii kukushukuru wewe pia kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuwa moja wapo wa wachangiaji wa hotuba hii ya Mhe. Waziri. Lakini pia nichukue fursa hii kwa dhati kabisa kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na timu yake hii ambayo imekaa chini na kuweza kutuletea mambo haya mazuri, naamini kwamba kama hotuba hii kama yaliyokuwemo katika kitabu hiki yatatekelezeka naamini kwamba wananchi wetu wa Zanzibar watafaidika na kupata maendeleo makubwa kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo basi sasa nianze kuingia katika kitabu hiki katika ukurasa wa 21 kwenye Idara ya Mifugo, mimi niipongeze Idara hii kwa kufanya juhudi kubwa kwa kuongeza uzalishaji wa ng'ombe kwa kutumia shindano, kama inavyoonekana katika kitabu hiki wameongeza ng'ombe wengi lakini pia naamini kwamba kama wataendelea na juhudi hizi tunaamini kwamba tutaweza kupata maendeleo makubwa na faida kubwa ya kuweza kuzalisha na kufaidika katika nchi yetu na kuuza nje ya nchi yetu. Pamoja na juhudi hizi basi zilizofanywa na wizara hii yapo maeneo machache naomba nichukue nafasi hii ili niweze kuyachangia.

Mhe. Mwenyekiti sasa nije kwenye ubora wa maziwa sote tunakubaliana kwamba maziwa yanayozalishwa hayana ubora na kiwango kinachostahiki, kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, nije katika maziwa ambayo yanazalishwa hapa . Kuna maziwa ukiyaona juu yana utandu vile vile kuna maziwa mengine unaweza kuyanya ukaona sio matamu na pia hayana ladha ya maziwa halisi na maziwa ambayo tumeyazoea, lakini sio hilo tu kuna mawiza pia unaweza kuyaona yana rangi ya maziwa halisi lakini ukiyanywa unayakuta yana harufu sio yale maziwa ambayo tumeyazoea.

Mhe. Mwenyekiti pamoja na mambo yote ambayo nimeyataja pamoja na aina zote nilizozitaja bado maziwa yetu hayana ubora ambao tunatarajia sisi wananchi ili tuweze kufaidika, lakini pia ili yaweze kutusaidia kwa afya yetu. Mhe. Mwenyekiti, bado ipo haja kubwa ya wataalam wetu wa kilimo waweze kuwapa mafunzo ya kutosha wafugaji wetu ili waweze kutoa maziwa bora ambayo sisi wananchi tunayatarajia.

Mhe. Mwenyekiti nije katika upande wa soko mimi nipongeze Wizara kwa juhudi ambazo wamefanya ya kuhamasisha wafugaji wetu na naamini kwa kitabu hichi wananchi wamehamasika sana na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, mfano nitatoa sisi tulipokuwa kwenye kamati yetu ya ustawi wa jamii tulipata nafasi ya kuwatembelea wafugaji wa ng'ombe pale Fuoni kulikuwa na kikundi cha ushirika kamati yetu tukenda na tukaanalia na wakatupa maelezo ya kutosha jinsi gani wanavyofaidika na ng'ombe wale wa maziwa. Lakini pale

palikuwa ni center ya kituo watu binafsi wenyewe wanafuga maziwa nje, pale wameweka kituo maalum cha wale wafugaji kwa kupeleka maziwa na wakatueleza walikuwa nazo *machine* za kutosha walipata msaada wakwatwambia kwamba kuna machine wanapimia maziwa ili kuyatambua ubora wake. Vile vile walitupa elimu ya kutosha mimi pamoja na kamati yangu tukafaidika sana.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu ilipata fursa yakupewa mtindi, mtindi ule wameuzalisha wao wenyewe tuliuonja mtindi huo kwa kweli ulikuwa mtamu sana. Baadhi ya wajumbe walitoa oda waletewe majumbani kwao. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hii inamaanisha kwamba wananchi wetu wamehamasika vya kutosha na wanajitahidi kufuga ng'ombe, lakini sio hilo tu ni kwamba wafugaji wetu lengo kuu ni kuwa wafuge lakini matarajio yao waweze kupata soko na hatimae wapate pato ili kujitosheleza na kujikimu kimaisha.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba bado wafugaji wetu hawana soko la kutosha, hili sote Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kama tutatembea kuanzia asubuhi unaweza ukakuta mfugaji ana maziwa yake kuanzia asubuhi mpaka mchana maziwa yale hayakupata mteja. Mhe. Mwenyekiti, vile vile wako wafugaji wengine utawakuta wana magari ambayo yamepakia maziwa wanapeleka marikiti, lakini pia hawana soko la kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niombe kupitia Baraza lako tukufu kuwa wizara katika kitabu chake Mhe. Waziri amezungumzia mambo mengi sana, lakini sikuona mwelekeo wao wa kuwasaidia wafugaji wetu kupata soko hili la maziwa. Mimi nakumbuka zamani nilipokuwa mdogo kulikuwa kuna kiwanda cha maziwa, na ilikuwa kila sikukuu unakuta kuna foleni katika vibanda vya maziwa. Pale Miembeni kulikuwa kuna kituo pale cha kuuzia maziwa, lakini sasa hivi kiwanda kile wamepewa wawekezaji na wawekezaji wale lengo la serikali kuwapa wawekezaji ili wakitumie na hatimae wananchi wetu waweze kufaidika na kiwanda kile. Mhe. Mwenyekiti, hatimae kiwanda kile hakifanyi kazi sasa hivi kimefungwa na mabanda yanaharibika kwa sababu nyumba ikiwa haikaliwi inabomoka.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tungetegemea kwamba wananchi wetu wanazalisha maziwa lakini wanapata mahala maalum wanakwenda kuuza na serikali yetu ingewasaidia kuuza. Kwa hivyo, kiwanda kile kingekuwepo kwa kweli maziwa mengi yakutosha tunatumia sisi mpaka tungeweza kusafirisha nje ya nchi. Mhe. Mwenyekiti, maziwa yangelikuwa yanapelekwa kiwandani basi pale kiwandani wangeweza kutumia kwa kutengeneza siagi, mtindi wa kutosha tukafaidika sisi wananchi na tungeweza kupeleka nje ya nchi. Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nimuombe Mhe. Waziri kwamba ipo haja ya kuona kwamba serikali wamehamasisha wananchi wetu, lakini ipo haja ya serikali kuwatafutia soko

wafugaji wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nikiendelea na mchango wangu nije katika ukurasa wa 35 katika suala la uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, sekta ya uvuvi ni sekta muhimu sana katika nchi yetu, lakini naona kwa mtizamo wangu serikali bado haijafaidika na sekta hii ya uvuvi, na matokeo yake sekta hii wanafaidika makampuni ya nje. Kama walivyosema katika kitabu chao kwamba wamewapa makampuni kuvua, lakini mimi mwenyewe huwa najiuliza je, serikali inajua kiwango ambacho wanakivua haya makampuni. Mimi naamini kwamba sio suala la kuwapa leseni kwa sababu tunawapa leseni lakini wao wanafaidika na rasilimali yetu kwa kiwango kikubwa sana. Mhe. Mwenyekiti, kwa taarifa tulizozipata ni kwamba kampuni hizi mwanzo walikuwa wanazalisha katika nchi yao na wamezalisha kwa kiwango kikubwa cha samaki na hatimae samaki wale wamekwisha sasa hivi wamekuja katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba serikali ikae chini na ijipange yakuhakikisha kwamba makampuni haya ambayo tumewapa wanavua kwa kiwango gani cha samaki. Labda Mhe. Waziri atakapokuja hapa kutoa majumuisho atueleze miaka mitatu ya nyuma makampuni haya tuliwapa leseni wamevua kwa kiwango gani. Mhe. Mwenyekiti, sio hilo ni kuwa ipo haja ya kumuweka ofisa wetu katika zile meli ijue samaki wanavua kwa kiwango gani, tusiwape tu tukawaachia tutafika wakati hapa na sisi samaki tunawatafuta kwa sababu watawamaliza na sisi tutabaki tunaagizia nje. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri akija hapa kwanza anieleze kwa kina ili nifahamu wanafanya kwa kiwango gani. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana naomba kuunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa fursa hii na mimi kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba uniongezee japo dakika tano kwa sababu nimo katika fani ya uvuvi basi muda huo utakuwa haunitoshi. Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kuchaguliwa kupewa wadhifa huu wa Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana na watendaji wake na namuombea Mwenyezi Mungu wizara hii aliyopewa basi *inshaallah* ilete mafanikio na tija kubwa katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu ya Zanzibar imefanikiwa au tuna bahati sana Mwenyezi Mungu ametukirimu kwa sababu pamoja na kuwa ni kisiwa lakini ni kisiwa ambacho kimezungukwa na bahari, bahari ambayo Mwenyezi Mungu katukirimu kwa upande huu wa Mashariki baina ya kisiwa cha Zanzibar hakuna mipaka, na kisiwa cha Pemba hakuna mipaka, mipaka yetu ni nguvu yetu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kutokana na adhma aliyonayo basi aijaalie hiyo

adhma Mwenyezi Mungu ampe uwezo waziri isiwe ni adhma ndani ya karatasi, iwe ni adhma ndani ya vitendo.

Mhe. Mwenyekiti, bajeti iliyopita ya wizara hii tulisema kwamba sasa umefika wakati wa kuona nchi yetu tunafaidika na rasilimali zilizomo kwenye nchi yetu. Kwa hivyo, rasilimali zilizomo kwenye nchi yetu moja ni neema ya baharini ambayo Mwenyezi Mungu ametukirimu. Kwa hivyo, tunataka tuone hii neema aliyotukirimu Mwenyezi Mungu inafaidisha wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Zanzibar tuna samaki ambao hawajavuliwa wamo samaki wala hatujawavua na hatuwezi tukafuga mali baharini tukawaachia wageni wakichukua mali hizo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aone kama wakati umefika wa kuwasaidia wavuvi wetu wa Zanzibar, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, wavuvi wetu wanavulia vyombo ambavyo havina uhakika. Ni vyombo vya kubahatisha na wavuvi unajua kuna kipindi cha Masika, kuna kipindi cha jua wavuvi kwa kweli kwa sababu mimi hii fani nimeshaipitia wanapata shida tena sana. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aone kama sasa kuna haja yakuona kama wavuvi wa Zanzibar sasa hivi wamo katika uvuvi unaotakiwa na ulimwengu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia wizara yake afanye jitihada ya kila kinachowezekana lakini ile rasilimali ya uvuvi wa bahari kuu tuione kama inafaidisha wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine nataka nilizungumze kwa Mhe. Waziri ni suala la walimaji wa chumvi. Mhe. Mwenyekiti, ukanda wa Pemba karibu asilimia ya wananchi wa Pemba ni walimaji wa chumvi, na bahati nzuri chumvi hii inapatikana kwa wingi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwake aone kama wa Zanzibari hawa wanaolima chumvi sasa wanataka kusaidiwa na kusaidiwa kwake ni kufanya jitihada kama inavyowezekana tuna nchi jirani ambazo hazina bahari.

Kwa hivyo, sisi tuko kwenye bahari tuone kama sasa kuna haja ya ile chumvi kuzalishwa kikamilifu na kupata soko nje ya Zanzibar, kwa sababu tuna wenzetu ambao hawana bahari. Kwa hivyo, sisi tulioko kwenye bahari ile chumvi sasa hivi ilete manufaa kwa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, wale walimaji wa chumvi watafutiwe soko na waenziwe kwa kupewa ujuzi zaidi, waelimishwe, wasaidiwe na serikali yetu kupitia wizara yake ili tuone kuwa Zanzibar inapata faida kutokana na yale maslahi ambayo kuwa yamo katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo ikiwa sisi tumo kwenye bahari na tunazalisha chumvi ni fahari kuona kuwa Zanzibar inaongeza bidhaa za kuzalisha ili tuweze kuuza nje na moja ni hilo la chumvi. Kwa hivyo, sasa Mhe. Waziri aone

kama anawasimamia wale walimaji wa chumvi walioko kule ili wasaidiwe kupata soko.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni suala la mifugo. Mhe. Mwenyekiti, mimi katika Jimbo langu la Micheweni Mwenyezi Mungu ametukirimu pamoja na umasikini tulionao lakini ni eneo ambalo lina wavuvi wengi na wafugaji. Kwa hivyo, kipindi kilichopita wizara yake Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi alitusaidia Micheweni lakini kutusaidia kwake nilisema kipindi kilichopita kwamba msaada ulikuwa ni mdogo mno, kwa sababu kule Micheweni hakuna asiyejua kwa Pemba kama ni sehemu moja wanaopatikana mbuzi kwa wingi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo msaada uliokuja ulikuwa mtu anapewa mbuzi mmoja tena dume, mtu unampa mbuzi dume unamwambia nenda ukapandishie upate makinda ili wawe mbuzi wa mifugo. Mhe. Mwenyekiti, hivyo haiwezekani mbuzi mmoja ili kukuza hii sehemu ya mifugo na kuwasaidia wananchi kiuchumi, tuone kwamba kuna haja yakupewa watu kama ni ushirika lakini wapewe mbuzi ambao wanatosha ili wanaoweza wakazalisha. Wakati huo huo Mhe. Waziri alileta mbuzi wa maziwa katika wizara yake lakini sikumuona hata mbuzi mmoja Micheweni wa maziwa kufika, na wakati Micheweni inajuilikana kama ni eneo moja la mifugo hasa mbuzi.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwake aone kama kuna haja ya kuanzisha vikundi vya ushirika ili kuwasaidia hawa mbuzi ili wananchi waondokane katika janga hili la umasikini. Mhe. Mwenyekiti, nina imani kama wananchi wa Micheweni watapewa mbuzi hawa wa maziwa basi tija yake tutaiona. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aone kama aache mtindo ule uliokuwepo wa kupewa kikundi mbuzi mmoja au jogoo mmoja, kuna mara moja walikuja wakapewa kila mtu jogoo mmoja hivyo jogoo mmoja mtu atamsaidia vipi, badala ya mtu kumpunguzia umasikini ndio tunamuongezea umasikini. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aone kama tunapofanya kitu tufanye kitu kwa ukweli, tusifanye kitu kwa kujaribu na sisi wa Zanzibari tuna matatizo haya ya kujaribu, kama ni utafiti tukishafanya utafiti basi tufanye jambo ambalo tumelikusudia.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni suala la wafugaji wa samaki, eneo hili nalo ni eneo ambalo Mhe. Waziri ametueleza kama kuna maeneo yanawafugaji wa samaki ambao wanaweza wakatusaidia. Lakini nataka niseme kwamba hawa wafugaji wa samaki na wao kuna haja ya wizara kuwasadia kwa kuwaendeleza, mimi nataka aniambie Mhe. Waziri kama wafugaji wote wa samaki waliomo Zanzibar aniambie ni mfugaji yupi ambaye hafugi samaki wa kitoweo tu, samaki wanaofugwa ni wakitowe tu, hawafugwi samaki wa biashara. Pia nataka aniambie kama sehemu fulani wanafugwa samaki wa biashara?

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema tusijaribu ni vizuri tutekeleze kwa ukweli ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu ili kuwatoa kwenye umasikini walionao. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, umeleta mapinduzi ya uvuvi nakuomba mheshimiwa utekeleze kila fani uliyonayo ili kusaidia Zanzibar na wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, tusiwe tunafuga samaki wa kitoweo bali tufuge samaki wa biashara, ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu. Kwa hivyo, mimi naomba nitoe ushauri mmoja wenzetu kule Kenya sehemu ambazo watu wamechimba fusi kuna maeneo kule walichimba kifusi kwa ajili ya kujengea barabara, basi yale yale yanatengenezwa yanakuwa mabwawa yakufugia samaki. Kwa hivyo, na sisi kuna maeneo mengi ambayo yamechafuliwa mazingira yake kwa ajili ya kuchimba vifusi kwa kujenga barabara, naomba yale mabwawa yanaochimbwa vifusi mheshimiwa ayaendeleze ili tuweze kufuga samaki. Mhe. Mwenyekiti, naheshimu muda wako ahsante na naunga mkono hoja hii.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe.Mwenyekiti, ahsante sana na mimi nichangia kidogo tu. Mhe. Mwenyekiti, moja kwa moja niende katika ukurasa wa 25 katika kuendeleza mradi huu wa kisasa wa kuku.

Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu hiki kuna maelezo ambayo ya mradi wa kuku ambao mradi huu muhisani wake ni Mzee Ali Yussuf ndiye aliyetujengea jengo hili. Lakini Mhe. Mwenyekiti, mradi huu kuna taarifa kwamba umekwama na umekwama kwa sababu ya masharti magumu ambayo yamewekwa katika kuendeleza mradi huu. Kwa hivyo, Mhe. Waziri ningemuomba wakati anatupa majibu yake aje atueleze ni sababu gani zilizofanya kwamba mradi huu ukwame na sababu hizo zilizofanya kwamba masharti ni yapi ambayo yanasababisha mradi huu ukwame.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Idara ya Huduma na Mifugo. Mhe. Mwenyekiti, kuna mradi ule wa Kisakasaka ambao uko katika maeneo ya Fumba, mradi huu juzi katika vyombo vya habari zilizungumzia eneo lile la Kisakasaka na eneo lile ni eneo ambalo mzee wetu Marehemu Abeid Amani Karume mpendwa na wengi aliwapa wakulima na wakwezi ili kukiendeleza kilimo pamoja na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, juzi kulikuwa na malalamiko ya wananchi wale kwamba eneo lile wamenyang'anywa. Kwa hivyo, ningemuuliza Mhe. Waziri ili atakapokuja aje atupe ukweli wa jambo hili kwa nini wananchi wale wamenyang'anywa maeneo yale au ni sababu zipi zilizofanya wanyang'anywe? Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ameshanisikia ukija uje utupe taarifa hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende kwenye ukarasa wa 58 kiambatanisho Nam. 4. Mhe. Mwenyekiti, kuna mradi ule wa maradhi ya mafua ya ndege pamoja na nguruwe. Mradi huu ulitengewa shilingi milioni 133,000,000 kutoka kwa Spinipa pamoja na *UNICEF* ambao walitoa milioni 175,000,000 na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitoa shilingi milioni 77,000,000. Lakini Mhe. Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka huu 2011/2012 katika kiambatanisho Nam.10 mradi huu umetengewa tena milioni 55,000,000 ambazo ni za SMZ, lakini hapa katika mkopo na wahisani hakuna kitu. Mimi nilikuwa nataka kujua kwamba katika mradi huu katika mwaka 2011 hawa wahisani ni vipi naomba atueleze ni sababu gani ambazo hazipo. Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema haya kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Rahaleo naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe bado kuna baadhi ya wajumbe ambao hawajawahi kuchangia, kwa hiyo Mhe. Waziri naomba uwatambue hawa ambao watakuwa wamebakia ili upokee michango yao pia. Kwanza ni Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mhe. Mohammed Mbwana Hamad, Mhe. Raya Suleiman Hamad na Mhe. Salim Abdalla Hamad.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi kidogo kuchangia hoja hii naamini kwamba Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi na watendaji wake mahiri watakuwa kwenye *position* yakutoa maelezo ya kina na ya kitaalamu zaidi kuhusiana na maeneo haya, ila na mimi ningependa nizungumze machache kwa nafsi yangu na kwa wizara yangu ambayo inahusika pia na mambo ya mazingira kwa sababu tunahusika katika maeneo mamoja.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nipende kumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohammed Shein kwa uamuzi wa makusudi wa kuamua kuunda wizara hii mpya ya mifugo na uvuvi kwa lengo zima la kusaidia mpango wetu wa kukuza uchumi na kupunguza umasikini. Na mimi naamini wizara hii itakuwa ni moja ya ngazi zetu za kupanda katika kufikia malengo yetu hayo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nimshukuru sana Mhe. Waziri jinsi ambavyo amewasilisha bajeti yake, imeandikika vizuri na inafahamika kama ambavyo wajumbe wengi wameisifia. Lakini vile vile sifa hizi ziwaendee watendaji mahiri wa wizara hii ya mifugo na uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, naomba unipe ruhusa niwatambue baadhi yao kwa sababu maalum.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais hakuchagua tu waziri makini, lakini kwa umuhimu wa wizara hii alihakikisha kwamba pia watendaji ambao atawapanga kumsaidia waziri basi nao ni mahiri, wenye uwezo, wenye *commitment* ya hali

ya juu. Kubwa zaidi ni wenye utaalamu wa mambo ambayo wanatakiwa kuyafanya. Mhe. Mwenyekiti, naomba kumtambua Katibu Mkuu wa wizara hii amebobea katika masomo yake ya *vetnary science* vile vile Naibu Katibu Mkuu Dk. Omar naye ni daktari katika shughuli nzima za *marine science*, lakini ndugu yetu Mkurugenzi wa Uvuvi Mussa Aboud Jumbe ambaye nae ana shahada ya pili katika mambo ambayo anahusika nayo. Vile vile tunaye Mkurugenzi wa Mazao ya Baharini nae ana shahada ya pili ndugu Mohammed Soud. Pia nae mwana mama ambaye amepewa dhamana ya wizara hii yuko Pemba nae si kalili ana shahada nzuri ya sayansi katika mambo haya ya bahari.

Mhe. Mwenyekiti, muda ni mchache lakini nimewataja pamoja na kuwapongeza sana na niwaombe wawe na mashirikiano ya hali ya juu ili walete mafanikio. Pia tunae Mkurugenzi Dk. Yussuf, ndugu Hafidh Alawi hao wote wako kwenye shahada ya pili na wengine wana PhD, lakini hata aliyepewa kupanga mipango ya wizara hii mwana mama ana shahada ya mambo ya mipango Bibi Aisha Alawi. Mhe. Mwenyekiti, vile vile Mkurugenzi wa Utumishi nae pia ana shahada ya pili. Mhe. Mwenyekiti, mimi nahisi amependelewa sana Mhe. Waziri lakini ni haki yake na kwa kweli kwa wizara hii tunawahitaji, mimi nasema nawapongeza sana. Mhe. Mwenyekiti, naamini katika miaka hii mitano ya kipindi hiki inshaallah tutaona mafanikio makubwa katika sekta hii ya mifugo na uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, pia nizipongeze jitihada za makusudi za Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa sababu tumesema wizara hii ni moja ya wizara ambayo itahusika katika kuwapunguzia wananchi umasikini kwa adhma yao ya makusudi waliofanya ziara Pemba kwenda kuona hali halisi ya ufugaji ikoje. Napenda niwatambue hapa walioandamana na Mhe. Waziri ni Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika Mhe. Haroun Ali Suleiman, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo nia ni nzuri tu yakwenda kuangalia hali ikoje ili waweze kujipanga vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaomba kuzungumza maeneo mawili tu na naomba nianze katika ukurasa wa 11 ambapo Mhe. Waziri ametuelezea juu ya changamoto zinazoikabili sekta hii ya uvuvi. Napenda kusoma pale ukurasa wa 11 anasema changamoto ambayo ameiona yeye kubwa zaidi ni kuongezeka kwa wavuvi kutoka ndani na nje ya Zanzibar katika maeneo ya hifadhi, naomba watu walitambue neno hifadhi katika hili. Pia kuweko na wavuvi wanaojishughulisha na uvuvi haramu na kukithiri ukataji wa mikoko katika fukwe ambao unapelekea kupunguza mazalio ya samaki.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana nimshukuru Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi kwa kweli kama tungekuwa na mwelekeo wa Waheshimiwa Wajumbe wetu wote wa Baraza ule ambao anao Mhe. Mwanajuma basi tungepata faida kubwa.

Lakini kidogo niseme nasikitishwa na baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wako ambao wanahisi maeneo ya hifadhi yanawanyima fursa wananchi wetu kupata mahitaji yao ya kila siku. Mimi nimshukuru sana waziri aliyetufanyia semina na kwa kirefu sana kabla ya hotuba yake hii ya bajeti na ndio maana leo michangio imekuwa michache. Lakini pia tulielezewa kwa kirefu faida ya maeneo tengefu.

Mhe. Mwenyekiti, uongozi ni pamoja na kufanya maamuzi mazito saa nyengie makali, machungu, lakini kwa faida ya nchi na wananchi wenyewe. Kwa hivyo, wananchi naamini wapo wengi wameshafahamu faida ya hifadhi ya maeneo ya bahari, kwa sababu unapohifadhi maeneo yale yana faida zake.

Mhe. Mwenyekiti, wengi wetu wakati wanachangia semina walikuwa wanaeleza jinsi gani wananchi wetu wanahitaji waende mbali na vyombo vya kwendea mbali hawana kwa sababu samaki maeneo ya karibu wamepungua sana au ni wadogo mno. Sasa lengo zima hili la hifadhi ndilo litakalowezesha wananchi wetu hawa hawa waweze kupata samaki wakubwa kutokana na hii hifadhi. Kwa sababu mle ndani watakuwa wamehifadhika wanazaliana na wakubwa watalazimishwa kutoka nje ili kwenda katika sehemu ambazo wananchi wetu wanaweza kuwavua.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri atoe taaluma ya hali ya juu na niombe kwa heshima zote Wajumbe wa Baraza lako tukufu hasa walio katika maeneo ya uvuvi kama Kojani na maeneo mengine ya Tumbe kwa kweli sisi tuwe walimu wa kuelimisha wananchi wetu jinsi ya kutunza hifadhi hizi za baharini kwa sababu ni kwa manufaa yetu na vizazi vyetu vijavyo. Bila ya hivyo Mhe. Mwenyekiti, wananchi wetu tutawaweka katika *position* mbaya sana, tunawapendelea sasa tunaona labda wanapata kumbe matatizo tutakuja kuyaona baadae na tayari nasema matatizo tumeanza kuyaona.

Lakini vile vile niwaombe sana ndugu zetu ambao wanashughulika na uvuvi lakini wanakata mikoko, kwa kweli ni hatari. Mjumbe wako mmoja alikuwa anajaribu kueleza alisema baadae athari tutaiona. Mimi nataka nihakikishe humu ndani ya ukumbi kwamba athari tayari zipo, kuna maeneo mengi ambayo yalikuwa ya kilimo sasa hayawezi kulimika tena kwa sababu maji ya bahari yamepanda kwenye ardhi kutokana na kuondoshwa mikoko ile. Sio hilo tu, lakini tunashuhudia *erosion* ambayo inatokea katika ufukwe, mmong'onyoko wa fukwe katika maeneo yetu. Kwa hivyo, niwaombe sana wananchi tunapozungumza hifadhi katika maeneo ya bahari kwa kweli washirikiane sana na serikali na inatia moyo kwamba hifadhi nyengine zimeanzishwa na wanajamii wenyewe. Kuna wanajamii ambao wanaifahamu sana, kuna zile ambazo serikali imeanzisha kwa mashirikiano, lakini ziko kama *PECCA*, hizi ni jitihada za wananchi wenyewe.

Kwa hivyo, niombe sana Wajumbe wa Baraza lako tukufu wanaporudi kwenye majimbo yao wasaidie sana kuelimisha wananchi, wasione kwamba wanatetea kuwa wavue kwenye maeneo ya hifadhi kuwa wanawapenda, kwa kweli nataka tujielimishe zaidi ili tuielimishe jamii yetu vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo kwa ufupi sana napenda nilichangie ni suala zima la uanzishwaji wa mabwawa ya ufugaji samaki. Nipongeze sana wananchi ambao wamejitokeza katika shughuli nzima hii katika kujikwamua na kupunguza umasikini kwa kuanzisha mabwawa ya ufugaji samaki. Lakini niwaombe sana wananchi, niiombe sana wizara, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Mazingira iko tayari kutoa mashirikiano ya hali ya juu kwa wizara na idara husika na wananchi kwa jumla ili kuangalia kwamba zinafanyika tathmini za kimazingira kabla ya miradi hiyo kuanzishwa. Sasa hivi tuwe tunamsikia mjumbe anasema mule sehemu kulikotolewa mchanga kwenye fukwe basi kuanzishwe mabwawa ya samaki.

Nia ni nzuri na wananchi wetu tuwa-*encourage* lakini naomba sana ashirikiane sana na Idara ya Mazingira katika kuhakikisha kwamba athari za kimazingira zinazingatiwa katika uanzishwaji wa miradi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba niunge mkono kwa dhati kabisa hotuba hii kwa asilimia mia moja nakushukuru.

Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali: Mhe. Mwenyekiti, baada ya kukushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi naomba niwashukuru sana, niwapongeze Mhe. Waziri na watendaji wake kwa umahiri ambao wameanza kuuonesha katika siku za mwanzo kabisa za utendaji wao katika wizara hii mpya. Matayarisho yao hata ya *budget speech* yanaonesha kwamba wako makini.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, nataka nichangie labda kwenye hoja mbili tu, labda kujaribu kuziweka sawa, kwa sababu zimeingia katika kumbukumbu zetu za Baraza letu hili. Mhe. Mwenyekiti, hoja ya kwanza ni ile ambayo aliizungumza Mhe. Rashid Seif Suleiman kuhusiana na samaki wa Magufuli. Katika mazungumzo yake alipokuwa akichangia alisema kwamba ile kesi imefutwa kwa sababu imeletewa hoja Mahkamani kwamba wale watu walipaswa washtakiwe Zanzibar kwa sababu wale samaki walivuliwa katika bahari ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba niseme tu kwamba ile kesi haijafutwa bado iko Mahkamani. Kilichotokea ni kwamba ile kesi ilikuwa na washtakiwa 37 mmoja akafariki, 31 wameachiwa kwa sababu walikuwa ni watumishi tu katika

ile meli hawahusiki na kesi yenyewe, lakini washitakiwa wengine watano (5) ambao ni kepteni mainjinia wawili pamoja na wakala wawili bado hawa wanaendelea na kesi.

Kwa hivyo, kesi bado ipo Mahkamani na hili suala la kwamba hii kesi au suala la kisheria la kwamba walipaswa washitakiwe Zanzibar kwa sababu wamevuliwa samaki Zanzibar halijawahi kuletwa Mahkamani na upande wowote ule wa washtakiwa wala upande wa mashtaka na halimo katika hoja ambayo ni *issue* katika ushahidi wa kesi ile. Kwa hivyo, nidhani kwamba ni vizuri tukaliweka sawa hilo kwa sababu linaweza likatoa pengine picha isiyo sahihi kwa wananchi wetu na katika kumbukumbu zetu za Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, suala la pili ni suala ambalo aliulizia Mhe. Makame Mshimba Mbarouk wakati anachangia. Yeye alitaka kujua na akasema lazima aelezwe uhalali wa sheria ile ya *Deep See Fishing Authority*.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nianze labda pale alipoanzia Mhe. Ismail Jussa kwamba suala la *Exclusive Economic Zone* na masuala yanayoambatana nayo ni moja katika kielelezo cha matatizo yetu katika usimamizi na utaratibu tuliouweka katika Muungano. Kwa sababu sheria hii ni kweli ilipitishwa mwaka 1998 sheria Nam. 1, lakini wakati inapitishwa mimi nakumbuka na kumbukumbu zipo kwamba serikali yenyewe ya Zanzibar ilipinga sheria hii kwa sababu ya utaratibu wake ambao ulikuwa umetungwa. Na ukweli ni kwamba serikali yenyewe kupitia aliyekuwa Naibu Waziri nadhani wakati ule kilimo Mhe. Mwalimu Haji Ameir, alikuwa ni Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi na akasema kwamba Serikali ya Zanzibar sheria hii inaipinga kwa sababu haikuzingatia maslahi ya Zanzibar katika kupitishwa kwake.

Kwa hivyo, Mhe. Jussa mimi napenda kumhakikishia tu kwamba anaposema jambo lina matatizo *at list* kwa hapa Zanzibar hakuna mtu ambaye atamuona mbaya. Kwa sababu serikali yenyewe ilishatangulia kuliona hilo na ilishalisema kwa kupitia Naibu Waziri wa wakati ule wa serikali. Lakini na pili serikali yenyewe ilichukua hatua ya kukataa utekelezwaji wa sheria hii na ndio maana kwa muda wa miaka 10 takriban sheria hii haikuweza kutekelezwa kwa sababu ilikuwa ni wazi ina matatizo na serikali ilikuwa wazi kabisa wala haikuwa na kigugumizi kwamba hii ni sheria ambayo hatuwezi kukubali kuitekeleza.

Kutokana na maelezo hayo na msimamo huo wa serikali, ndio maana sheria hii ikafanyiwa marekebisho mwaka 2007 kupitia Sheria Nam. 17 ya mwaka 2007 ambapo vifungu takriban 21 kati ya vifungu 23 vya sheria hii vilifanyiwa marekebisho. Sasa suala linabaki pale pale kwamba je uhalali au si uhalali kama alivyouliza Mhe. Mshimba. Mimi niseme kwamba hii ni moja katika *grey area* ya Muungano. Kwa sababu unapozungumzia *exclusive economic zone*

takriban katika nchi zote basi inakuwa na matatizo baina ya nchi moja na nchi nyengine. Kwa hivyo unaweza kukuta kwa mfano, nchi kama Jamaica ina migogoro karibu na nchi tisa kuhusiana na suala hili la *exclusive economic zone*.

Nchi za Norway na Warusi walikaribia kupigana kwa sababu ya suala hili hili, Iceland na Uingereza na nchi tarban nyingi tu, Ghana na Nigeria na Cameroon kwa suala la bokasi, Nigeria na Sautome na Principe walikuwa na mzozo ambao pia wakakubaliana kutokubaliana lakini wakaja na suala la busara la kuwa na *joined development zone* yaani kuanzisha mamlaka ambayo hilo eneo wanalobishana basi wataliendesha kwa pamoja. Kwa hivyo, na sisi eneo moja kwa sababu hili si suala la Muungano, exclusive economic zone ni ya Jamhuri ya Muungano sio ya Tanzania Bara sio ya Zanzibar, lakini ya Jamhuri ya Muungano tulivyokwenda kuidai kwa sababu ule mkataba wenyewe wa Umoja wa Mataifa wa sheria za bahari wa mwaka 1982 unatambua *sovereign state*. Kwa hivyo, ni la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Lakini si sehemu ya *territorial area*, yaani si sehemu ya nchi lakini ni eneo la kiuchumi. Na kwa sababu uchumi si jambo la Muungano ndio tukasema kwamba uvunaji wa rasiliamali wa eneo hili ni suala ambalo sio la Muungano na kwa hivyo tulichokubaliana ni kuunda chombo cha pamoja. Kama ingekuwa Zanzibar na Tanganyika ni nchi tofauti labda tungefanya kama walivyofanya Nigeria na Sautome na Prince ya kuwa na *treat* na *treat* ile ndio ikaongoza mahusiano yetu, lakini sisi ni taifa moja kwa hivyo tulichokubaliana ni kuwa na *joint commission* au *joint authority* ambayo itasimamia hii na utaratibu wake umeelezwa vizuri ndani ya sheria Nam. 1 ya mwaka 1998 kama ilivyorekebishwa na sheria Nam. 17 ya mwaka 2007.

Kwa hivyo tumekubaliana kwa sababu si eneo la *territorial area*, hivyo kwa vile ile sheria yenyewe kama ilivyopitishwa na Bunge basi iendelee na kwa sababu ni chombo cha pamoja iendelee kwa utaratibu ule ambao tumekubaliana na sheria hiyo imepitishwa kwa makubaliano na sisi tukasema ni eneo ambao tunakubaliana. Kwa hivyo, uhalali wake sasa hivi sio *issue*, *issue* ni ile ambayo ipo ya kwamba namna gani utekelezaji wake utakuwa kwa kweli. Kwa hivyo, niseme tu kwamba kwa sasa hivi pamoja na makubaliano hayo lakini baada ya kuipitia tena karibuni tu alipokuja Mhe. Waziri hapa Mhe. Said Ali Mbarouk tukagundua kwamba yapo maeneo ambayo tunahitaji kuyaimarisha zaidi katika sheri ahii na hata ile sheria yenyewe ya *EEZ* na ni kazi ambayo tunaendelea kuifanya na tumepewa kazi hiyo rasmi na serikali ili tuisimamie ili maeneo yale yanayohitaji kufanyiwa marekebisho kuimarishwa basi iendelee.

Kwa hivyo, naomba nimtoe wasi wasi kuwa hii sheria kwa sasa hivi suala la uhalali sio issue kwa sababu tumekubaliana kuiendesha kwa utaratibu huo

lakini yapo mambo ambayo tunahitaji kuyafanyia marekebisho na hiyo kazi tunaendelea nayo, kwa sababu tokea tumekabidhiwa si muda mrefu tunaendelea kuifanyia kazi.

Mimi niseme kwamba bado katika maeneo hayo tunaweza kuendelea kuwa na matatizo lakini yanapotokea kama wanavyofanya wenzetu basi tunayachukulia hatua, tumeyaona na tunayafanyia kazi kwa kweli. Baada ya kusema hayo mimi niungane na wenzangu kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na naomba wenzangu tuipitishe, tumuwezeshe Mhe. Waziri na timu yake mahiri waweze kufanya kazi na kutusaidia kupata utajiri katika eneo hili muhimu ambalo wamekabidhiwa ahsate Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nishukuru sana kwa nafasi hii, na hii ni hotuba yangu ya kwanza kuichangia na ninaichangia kwa sababu maalum. Kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana rafiki yangu, swahibu wangu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, nimshukuru yeye lakini pia nimshukuru sana sana na Katibu Mkuu wake kijana barabara makini na Mkurugenzi wake wa Uvuvi na wengine wote kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya nay ale ambayo wameyapanga kuyafanya.

Mhe. Waziri namjua uwezo wake, na simsifu tu kwa sababu leo kavalia suti au vipi, lakini Mhe. Waziri nilipokuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali michango yake naikumbuka vizuri sana, *he was always very constructive*. Siku moja nilimwambia atakuwa kasahau tu, Shehe Saidi nakuotea mambo mazuri *Inshaallah* yanakuja, sasa ndio hayo yashafika leo.

Mhe. Mwenyekiti, nianze nisije nikasahau, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Makunduchi wote naunga mkono hoja ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja. Napenda niwahakikishie Waheshimiwa wote ambao walimuuliza Mhe. Waziri hasa katika masuala ya kuwawezesha wavuvi na wafugaji, kwa vile Mhe. Rais ameunda wizara hii ya uwezeshaji wananchi kiuchumi na ushirika, kuna kila sababu ya wizara hizi mbili na *Inshaallah* kesho nimekusudia vile vile kama utanipa nafasi au keshokutwa nije nichangie Wizara ya Kilimo na Mazingira. Kwa sababu huko ndiko ambako kunahitaji uwezeshaji wa hali ya juu kabisa, na Rais wa Zanzibar alipoamua kuunda wizara hii akaiunda na wizara hii mpya ya mifugo alijua kwamba lazima wizaa hizi mbili zitashirikiana kwa nguvu zake zote ili kuwawezesha wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, tulifanya ziara Pemba na Mhe. Waziri tukafuatana na kinara wetu mkuu wa msafara ingawa walipofika Pemba wakageuza wakanambia mimi ndio mkuu wa msafara, Mhe. Waziri wa Fedha. Nilikubali kwa sababu ndio nimeshakuwa *senior minister* tena. Lakini nashukuru kwa heshima ile

waliyonipa, tukenda kwenye maeneo mbali mbali karibu Pemba yote tuliimaliza, tuliwakusanya wavuvi na wafugaji hasa wavuvi na tumewasikia wavuvi wanavyozunguza, wote wanataka wawezeshwe na Mhe. Mwenyekiti, serikali yetu imejidhatiti vizuri, imejipanga vizuri tutahangaika Mheshimiwa ili kuhakikisha kwamba wavuvi tunawawezesha kwa nguvu zetu zote. Kwa hivyo, wale waheshimiwa ambao walimuuliza sana masuala ya uwezeshaji hayuko peke yake tutashirikiana naye.

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu kidogo nizungumzie masuala ya ujumla ambayo yatazungumzia wavuvi na wafugaji wa Jimbo la Makunduchi. Kwanza nimshukuru sana Mkurugenzi wa Uvuvi, na nimshukuru sana aliyekuwa Waziri wa Kilimo wakati ule Mzee wetu, rafiki yetu mimi *personal* ni rafiki yangu Mzee Burhani Saadat Haji, wametusaidia kutupatia boti kule za uvuvi na mashine nashukuru zinawasaidia wananchi. Lakini Mhe. Waziri Makunduchi jirani yetu upande wa Mashariki ni Indonesia, narejea tena, Makunduchi ukitizama kwenye zile laini za *latitude* kwenye *glob* ile basi ni Indonesia. Sasa wale ndio majirani zetu upande wa Mashariki, kuna visiwa vyengine vidogo vidogo viko juu na chini lakini pale ukikata moja kwa moja nchi ya kwanza utaikuta Indonesia. Hii inaonesha kwamba ukubwa wa bahari yetu tuliyokuwanayo.

Karibu mwezi mmoja au miwili jinsi bahari ilivyochafuka zile boti ndogo ndogo kule hazifiki. Kwa hivyo, Mwenyezi Mungu atapokujaalia na tutashirikiana na Waziri wa Fedha anasikia tutapopata misaada ya maboti yale makubwa ya kukaa baharini yakahimili vishindo vya baharini kama wale wenzetu wanaokuja wakivua kwetu tunawaona kwa mbali wale, basi *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akupe ilham ya kuweza kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Makunduchi na wengine wote ambao wana matatizo kama hayo.

Mhe. Mwenyekiti, Kizimkazi kule Mkunguni na Dimbani siku moja wananchi wangu walinijia wakanambia Mheshimiwa mjini vibua vinavuliwa, sasa mimi najua taratibu za kuharibu na pengine kuleta matatizo ya mazingira katika maeneo ya kule, lakini maeneo ya kule kuna vibua vingi sana. Sasa siku moja wananchi wangu wakanambia Mwakilishi tuna tatizo sisi la maji katika eneo letu hili mashine yetu imeungua, tunakuomba utuombee basi angalau siku moja tu, tukavue vibua ili tupate pesa, lile suala likawa zito kwa sababu naelewa hatari zake na kwa Mkurugenzi Mussa kumwambia masuala hayo pana mtihani kidogo, lakini nilimwambia kanambia Mheshimiwa tunakuomba bora uyaache hayo mambo kama yalivyo.

Lakini hebu tuliangalie Mhe. Waziri, kwa sbabu ni sehemu moja ya kuwapatia uchumi wananchi wale, kama kutakuwa na njia ambayo ya kuwasaidia kwamba uvuvi ule ufanyike bila ya kuharibu hayo maeneo ambayo tunayazungumza

watafarajika wananchi wa kule Mhe. Waziri kwa sababu vibua viko vingi sana kule katika kila hali mimi nina hakika tukitumia mbinu za busara na hekima na tukawasaidia wananchi wetu basi tunaweza tukafanikisha zoezi lile la uvuvi wa vibua, lakini hatari zake vile vile nazielewa.

Sasa Mhe. Waziri naomba maafisa wako ambao wana uwezo mkubwa nimesema Katibu Mkuu wako namuelewa vizuri sana na Wakurugenzi wako nawaelewa hao niliowataja naomba sana tushirikiane kwa pamoja ili kuwapa nyezo wale wananchi wa kule Kizimkazi basi angalau waweze kupata nafasi japo siku moja katika mwaka au katika miezi sita wakapata nafasi ya kwenda kujitafutia risiki zao. Lakini bado naelewa umuhimu wa kulinda mazingira yetu ndani ya bahari na nataka hilo tuliendeleze.

Mhe. Mwenyekiti, la pili wafugaji wapo kule, lakini nakuomba sana maafisa wetu, tunao madaktari wetu wanatupitia kule na mimi ni mfugaji *Alhamdullilah,* nimefuga kuku na nilipokuwa mdogo na mbuzi nilikuwa nachunga vile vile kwa dhiki, lakini upande mmoja nilipenda na mpaka leo mimi ninao mbuzi wengi tu. Utanikuta nimekaa kwenye banda la mbuzi nawatizama tu na *enjoy,* kwa sababu ukiwa na mifugo wakati mwengine kama unavyojenga nyumba mpya unakwenda ukiitizama tu japo kuwa hujengi wewe. Kwa hivyo, na raha ile naiona vile vile. Nimeanzisha konde ya migomba kule kesho nitakuja kuchangia au keshokutwa kusema mambo ninayoyaona kule, migomba niliyopanda miezi sita tu sasa hivi kuna mikungu zaidi ya mia moja ya ndizi iko tayari. Yote hayani kwa sababu wananchi wamekubali kufanya kazi ya shughuli za kilimo na mifugo.

Kwa hivyo, ng'ombe wetu wakati mwengine hasa hao wa kienyeji Mhe. Waziri tuansema wana *resistance* kidogo ya kupata maradhi, wanaumwa wakati mwengine wale. Lakini sasa maofisa mpaka uwaite ndio waje. Mimi ningekuomba Mhe. Waziri ili kuwapunguzia usumbufu wananchi kwa sababu mwananchi akiona ng'ombe wake anaumwa na mafua anaona ni jambo la kawaida tu, lakini pengine athari yake baada ya wiki mbili tatu ndio hivyo tena utakujasikia kaanguka shimoni keshachinjwa. Kwa hivyo, nakuomba wale maafisa wetu hasa wa mifugo, madaktari wetu wasikae mpaka wapelekewe, ningeshauri sana wakawa na *routine* ya kuweza kutembelea wafugaji wote wajue wapi walipo, wanafanya nini, wanafuga nini ili waweze kuwajua na hilo ninahakika litasaidia sana hasa wafugaji wa kuku.

Kuku wa kienyeji wanachukua muda mrefu sana kupata maradhi ukilinganisha na hawa wa *broilers*. Mimi nilikuwa nafuga *broilers* siku moja niliwachukua kwenye gari yangu *double cabin* nikawaweka nyuma kama kuku 30 hivi, kufika mjini wamebakia watatu ule upepo wa njiani tu wamekufa. Wakati wa kienyeji unamtoa Makunduchi unamning'iniza kichwa chini miguu juu mpaka

mjini mzima ukimfungua anakimbia kwa sababu ya *resistance* waliyokuwanayo. Lakini hata hao wa kienyeji wanahitaji kuangaliwa pia, kwa hivyo, naomba sana zitolewe taaluma na mimi niko tayari kwa njia yoyote Mhe. Waziri usiwe na wasiwasi kusaidiana na wewe katika suala zima la kuwawezesha ili iwaweze kupata utaratibu huo.

Kumezungumzwa suala punda hapa, nilikuona siku moja Mhe. Waziri unatoa zawadi kwa punda bora, punda ambaye amefugwa vizuri, ametunzwa vizuri na mfugaji anamuendeleza vizuri na mimi nilimuona kwenye picha anapendeza. Suala la punda kwa baadhi ya majimbo hapa usiyaguse, lakini kweli vijana wetu wanawatumia wale kwa shughuli mbali mbali za kimaendeleo na kiuchumi.

Kuna mzee mmoja Kikwajuni alinisimamisha juzi, akanambia *Yallah Yallah*, kwa hisani zenu jamani Waheshimiwa mnajadili mambo, punda yuko katika hali ngumu hapa, kapakiwa mzigo mtu yuko juu anakwenda nae na mbio anazokwenda na vigongo anachezea. Mimi sina tatizo kwa sababu vijana wetu wanawatumia wale kwa shughuli zetu mbali mbali za kimaendeleo lakini aste aste.
Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni niliona picha kwenye Gazeti la Zanzibar Leo ya ng'ombe, kabebeshwa gari na mzigo nyuma kaanguka, lile la kukaa shingoni ndilo lililomlaza chini, sasa yule hata ukimnyanyua hawezi kunyanyuka keshachoka kwa sababu ya tani ya uzito aliopewa. Sasa tushirikiane sana nadhani na Baraza la Manispaa, kwa bahati mbaya waziri anayehusika na Manispaa hayupo lakini mawaziri ndio sisi taarifa ndio hii tushirikiane tuhakikishe kwamba wanyama hawa tunawaenzi. Wakiwatunza wale na wao watafaidika, wakikaa nao vizuri, wakiwabebesha mizigo kiasi chao basi na wao watapata umri mrefu wa kuwatumikia katika shughuli zao mbali mbali za kimaendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, sikuwa na mengi ya kueleza nilihisi nami nichangie. Namshukuru sana tena Mhe. Waziri na kumtakia kheri. Sheikh Said Ali Mbarouk tuko pamoja ufanye kazi zako ujue una wenzako. Serikali ya Umoja wa Kitaifa tutadumisha umoja wetu kuhakikisha kwamba kazi yangu ndio kazi yako wewe.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na *inshaallah* nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wote. Mimi niliwaomba wavae viatu vya raba lakini baadhi yao wakatafuta na njumu wakaweka. Sasa naomba kwa Mhe. Waziri bajeti yake tuvae viatu vya raba vyepesi vile ili turekebishe. Kwa sababu hotuba yake ilivyoandikwa Mhe. Ismail Jussa Ladhu kasema na mimi namuunga mkono, ni moja katika hotuba ambayo imeandikwa vizuri, inajieleza vizuri kabisa maeneo yote muhimu ya

wizara yake.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na kila nitakapokuomba nafasi ufanye kila njia ili unipe *inshaallah*.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia Bajeti ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, katika masuala yaliyoelezwa hapa moja ni suala la bei ya mwani na soko la mwani. Kama tunavyojua kwamba Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ndio wizara inayoshughulikia masuala ya masoko. Nataka niwahakikishie ndugu zangu wawakilishi kwamba wizara yetu inashirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika suala zima la kutafuta soko la mwani na kuona kwamba bei ya mwani wanayopewa wakulima wa mwani inalingana na hali halisi ya soko la dunia.

Naamini kwamba kwa kipindi kifupi kijacho wananchi watapata bei wanayostahiki kwa sababu tutafuatilia na tutalifanyia kazi ambapo tutakaa pamoja na wafanyabiashara na wakulima wa mwani na tutawapa bei ambayo wanastahiki wakulima kulipwa. Sisi tunaamini kwamba hii bei bado ni ndogo na ipo haja ya kuwapatia bei inayostahiki kulipwa wakulima wa mwani.

Lakini la pili ni suala hili la soko la lulu linalotokana na chaza. Mhe. Mwenyekiti, ningewaomba wale wote ambao wanahusika na miradi hii wafike Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko tupate kuwasaidia masoko ya bidhaa hizi. Naomba kuwatangazia rasmi wale wote wanaotafuta masoko ya bidhaa zao basi washirikiane na wizara yetu ili tuweze kuwatafutia masoko ya bidhaa zao.

Vile vile naomba kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wote kwamba Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inashirikiana kikamilifu na wizara hii katika masuala ya kushajihisha viwanda kwa ajili ya ku-*process* minofu ya samaki. Kama tunavyojua kwamba wizara hiyo kazi yake kubwa ni kuandaa upandaji wa mwani lakini masoko ni kazi ya wizara yetu. Vile vile uvuvi, lakini viwanda vya ku-*process* minofu ya samaki viko chini ya wizara yetu. Kwa hivyo, tunashirikiana pamoja na tunaamini kwamba kwa kipindi kifupi kijacho tutaweza kuanzisha viwanda vya samaki na pia tukawapatia masoko wananchi wetu katika bidhaa wanazozalisha.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, nasema kwamba kwa niaba ya Jimbo la Mtoni naiunga mkono mia kwa mia Bajeti hii ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi hii ya kutoa majumuisho kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Lakini pia nakushukuru sana kwa namna ambavyo leo umeendesha mjadala huu na naomba pia shukrani kama hizi ziende kwa Mwenyekiti mwenzako ambaye jana ndie aliyeanzisha mjadala huu. Kwa kweli umeendesha mjadala vizuri, mjadala ambao umeniwezesha mimi na wenzangu katika wizara hii kupata maelekezo ya kina kutoka kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitangulize kwa kusema kwamba mafanikio yoyote ambayo yamepatikana katika sekta za mifugo na uvuvi basi ni matokeo ya kazi nzuri na kubwa ya wafugaji na wavuvi wetu wakisimamiwa na Wajumbe wa Baraza lako la Wawakilishi katika majimbo mbali mbali. Kwa kweli nawapongeza sana. Ikiwa kuna udhaifu wowote ambao umetokea basi mimi ndie ninayebeba jukumu hilo kama msimamizi wa wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba niwatambue Waheshimiwa Wajumbe ambao wamechangia bajeti hii, wamechangia vizuri sana, wamenishauri sana nashukuru, kuna wengine wamenipongeza nawashukuru, wengine wametuelekeza. Kwa niaba ya watendaji wangu wote waliotupongeza, waliotushukuru na waliotuelekeza tunachukua na tunaahidi kuyafanyia kazi kwa maslahi ya wafugaji na wavuvi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, waliochangia ni Waheshimiwa Wajumbe 30. Kwanza alianza Mhe. Assaa Othman Hamad kwa niaba ya Kamati ya Mifugo, Uwezeshaji, Utalii na Habari, lakini pia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Wete.

Mwengine Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Rashid Seif Suleiman, Mhe. Asha Bakari Makame, Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Mhe. Abdi Mosi Kombo, Mhe. Salma Mohammed Ali, Mhe. Mussa Ali Hassan, Mhe. Farida Amour Mohammed, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, Mhe. Fatma Mbarouk Said, Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe. Hassan Hamad Omar, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Abdalla Moh'd Ali, Mhe. Suleiman Hemed Khamis, Mhe. Rufai Said Rufai, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, Mhe. Asha Abdu Haji, Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mhe. Subeit Khamis Faki, Mhe. Nassor Ali Salim, Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji, Mhe. Mwanasheria Mkuu, Mhe. Haroun Ali Suleiman na Mhe. Nassor Ahmed Mazrui.

Waheshimiwa Wajumbe waliochangia kwa maandishi ni Mhe. Mussa Khamis Silima na Mhe. Mgeni Hassan Juma. Mhe. Mwenyekiti, kama kuna mjumbe nimemsahau basi si dhamira lakini itakuwa ni makosa ya kibinadamu naomba

radhi.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba wote ambao wamechangia wametupa ushauri na maelekezo mazuri na tunashukuru sana. Mhe. Mwenyekiti, kwanza tunaishukuru kamati ya Mhe. Assaa Othman Hamad pamoja na wajumbe wa kamati. Muda wote wamekuwa karibu na sisi, wamekuwa ni sehemu ya wizara kwa njia moja au nyengine, wamekuwa wakitusimamia vizuri sana, wamekuwa wakituelekeza Mwenyekiti, Makamo na Wajumbe wote kwa kweli tunawashukuru sana. Wamekuwa wakitusaidia sana na kwa kweli muda wote tumekuwa tukiwategemea kwa maelekezo yao kutuongoza katika shughuli zetu za wizara. Kwa hivyo, michango yao waliyotupa tunaichukua na tunaifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, jambo muhimu ambalo mara hii wametusisitiza ni kwamba tufanye kila jitihada tuanzishe chuo maalum cha uvuvi hapa
Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, ushauri huu tunauchukua, tunaufanyia kazi na kwa sababu wao wapo karibu na sisi tutashauriana namna gani ya kutekeleza ushauri huo.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo wametushauri na ambalo Mwenyekiti wa Kamati hii ya Mifugo, Uwezeshaji, Utalii na Habari amelikuwa akilisisitiza sana mara zote ni suala la hatimiliki. Hili ni jambo ambalo kamati hii wamekuwa wakali sana, wametusukuma sana na bado leo wametushauri.

Mhe. Mwenyekiti, nakuahidi kwamba ushauri wao tutaendelea kuufanyia kazi, tumeanza pazuri, tumewasiliana na Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, tumewasiliana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, kwa kweli tuna mipango mizuri. Baada ya bajeti hii tukijaaliwa tukipata uwezo basi mwenyewe Waziri wa Fedha anasema hili atalisimamia. Mhe. Mwenyekiti, yale yote ambayo kamati wametuahidi tutaendelea kuyafanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Assaa Othman Hamad alitushauri pia tutafute mifugo michache. Ni kweli Mhe. Mwenyekiti, ardhi ya Zanzibar sio kubwa haiwezi kuhimili kuchunga lazima tufuge na hili ndio wazo la Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk.

Ali Mohammed Shein, ametwambia tuache kuchunga lazima tufuge. Sasa hili linakuja sambamba na wazo la Mhe. Assaa kwa kweli tumeanza kulifanyia kazi tunalichukua wazo lake.

Lakini pia kwa vile yeye ni mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi amekwenda kule ameona mambo mazuri kwamba wenzetu wanategemea kuitumia maabara

ya Temeke kwamba ni maabara ya *SADC*. Kwa hivyo, ametuletea habari hii na kwamba ametutaka sisi kuwasiliana na wenzetu wa Bara kuona namna gani na sisi tutafaidika na mpango huu kupitia program ya *SADC*.

Mhe. Mwenyekiti, tunamshukuru sana na hivi hasa ndio anavyotakiwa Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi afanye. Maana aende kule achume halafu aliletee Baraza la Wawakilishi litumie. Kwa hivyo, namshukuru na kwa kweli tutalifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, suala la kushauriana na Waziri wa Afya namna gani Wacuba wanavyowasaidia na sisi tunavyofaidika, basi tumeshaanza kuzungumza na yuko tayari kuisaidia wizara yangu namna gani kupata *contract* ya Serikali ya Cuba katika masuala mazima ya maabara ya mifugo. Tunamshukuru sana Mhe. Assaa Othman Hamad kwa ushauri wake.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana sahibu yangu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, yeye amezungumzia mambo mengi kama kawaida yake lakini akatushauri kubwa kwamba shamba la Pangeni tulitumie vizuri. Kwa kweli bahati nzuri shamba la Pangeni limo katika Jimbo la Kitope. Ni kweli nakubaliana nae kwamba katika miaka ya karibuni lile shamba lilikuwa hatujaliimarisha vizuri, lakini tuna mazungumzo na wawekezaji watatu na wote wameshakwenda kulikagua shamba tunaendelea na mazungumzo. Kama tunaona maslahi ya taifa yatakuwa mazuri tutashirikiana na Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuangalia namna gani uwekezaji huo tutafaidika pale.

Tunaamini kwamba ni kupitia njia ya wawekezaji ndio mashamba ya aina hiyo yataweza kuendelezwa na pia kupata tija ile ambayo serikali tumeikusudia. Kwa hivyo, wazo lake tumelichukua na bado tumo katika mazungumzo na wawekezaji katika suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la uvuvi limezungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe wengi na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk nae alizungumza kwamba jitihada zifanywe kuona kwamba tunaendeleza kuwatafutia wavuvi wetu zana bora za uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, hilo ndio jukumu kubwa la wizara na kama alikuja juzi katika semina basi huku ndiko tunakokwenda.

Aidha, alitaka tuhakikishe kwamba tunasimamia vizuri utaratibu wa uvuvi haramu. Mhe. Mwenyekiti, mimi nampongeza sana Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kwa sababu baadhi ya wawakilishi wenzangu wengi huwa wanaona haya kuzungumzia suala la kuwa makini katika kusimamia Sheria ya Uvuvi Haramu. Kwa hivyo, Mhe. Mshimba yeye amekuwa makini na amekuwa jasiri katika hili na kwa kweli tunampongeza sana. Hitaji lako la kwamba nije twende

Kairo na Kiwengwa nimelikubali na baada ya bajeti hii nitakwenda.

Mhe. Mwenyekiti, suala la Sheria ya Bahari Kuu namshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu amenisaidia sana na yale ndio majibu ambayo ninayaafiki.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rashid Seif Suleiman yeye alizungumzia suala la kwamba tule samaki kwa wali badala ya wali kwa samaki. Wazo lake ni zuri na kwa kweli tukiweza mipango yetu ya wizara tuliyoipanga kufanikiwa kwamba tuvue katika maji ya ndani, tuvue katika bahari kuu, lakini pia tufanikiwe katika ufugaji wa samaki. Mhe. Mwenyekiti, huko ndiko ambako tunakwenda.

Hivi sasa bahati mbaya tunavua katika maji ya ndani tu, hatujaweza kuvua katika bahari kuu, lakini pia hatujaweza kuimarisha vizuri ufugaji wa samaki. Kwa hivyo, tunaanza sasa katika taratibu za ufugaji wa samaki tukifanikiwa huku. Lakini pia tukipata kufanikiwa kuvua katika bahari kuu kwa wazalendo ninaamini kwamba wazo la Mhe. Rashid Seif Suleiman kwamba tule samaki kwa wali hilo litafanikiwa na hapo ndio yale mapinduzi makubwa katika uvuvi yatakuwa yamefikiwa vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, suala la Mhe. Rashid Seif Suleiman kwamba kituo cha kuzalisha kuku wa kienyeji kwa urahisi tulifanyie kazi. Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo ambalo lingeweza kufanyiwa kazi zaidi na sekta binafsi. Sisi kama wizara tuko tayari kutoa miongozo, tuko tayari kutoa taaluma, ili sekta binafsi ishughulikie masuala haya. Lakini wizara kuanzisha vituo kwa kweli ni sera ambayo imepitwa na wakati kidogo. Sisi kama wizara kazi yetu ni kutoa *regulation,* kutoa utaratibu, kutoa taaluma ama kwa wawekezaji au kwa watu binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, wameshaanza kwa kweli kuna watu hapa tayari wana *incubator* zao za kuzalisha vifaranga wa kuku wa kienyeji. Tunawapongeza na tunawaomba wengine wafanyabiashara wa ndani na hata Wajumbe wa Baraza lako tukufu Mhe. Mwenyekiti, tuko tayari wizara kuwapa taaluma ya kuona kwamba kuku wa kienyeji wameongezeka katika nchi kupitia vituo hivi. Wazo lako la takwimu tumelichukua tutalifanyia kazi.

Suala la ufugaji wa ng'ombe nani mwenye uwezo wa mamlaka ya ng'ombe kuingia nchini, ni sisi wizara kupitia Sheria yetu ya Mifugo inafanya kazi lakini bahati mbaya sheria imekuwa kongwe kidogo. Kama tulivyosema katika bajeti yangu ni kwamba tunafanya *review* ya sheria na sera zote ili ziweze kwenda sambamba na utaratibu wa kileo. Kwa hivyo, ni kweli hapo kati kati mambo yalipoyumba tumeyaona na ndio kazi ya kwanza ya Idara ya Mipango na Sera hivi sasa inapitia sheria zote na sera zilizopo ili kuona kwamba zinakwenda sambamba na utaratibu wa kileo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la diko la Kichuwani. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli hapa tuna tatizo kidogo. Katika diko la Kichuwani kuna tatizo baina ya Kamati ya Uvuvi na Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake. Hili ni kweli na ni ugomvi ambao unatupa matatizo kidogo. Tatizo lenyewe lipo kwamba sisi katika Sheria yetu ya Uvuvi diko liko chini ya Idara ya Uvuvi. Lakini Halmashauri ya Wilaya nao kwa kupitia Sheria yao ya Tawala za Mikoa wana kanuni ambazo wanaweza kuzitunga ili kukusanya mapato.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo hili pia lipo Wesha, kulikuwa na tatizo hili Kengeja mimi na mwakilishi tulikwenda, sasa tumeshakubaliana mimi na Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tukae pamoja mimi, yeye na wataalam wake wa sheria tuangalie migongano iko wapi ili tupate pahala pakutulia. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi awe na subira kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rashid Seif Suleiman alisema kwamba anahitaji soko eneo la Kichuwani. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli masoko yanahitajika maeneo mengi katika nchi yetu siwezi kumuahidi moja kwa moja kama nitamjengea soko. Lakini ningemshauri kwamba baada ya bajeti hii tukijaaliwa tukae mimi, yeye, pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais tuone namna gani ya kujaza fomu watu wake kupitia miradi ya *MACEMP* na *TASAF* ili kupata utaratibu wa kujengewa soko katika eneo la Kichuwani.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Asha Bakari Makame ushauri wake tumeuchukua, suala lake la hatimiliki amelirudia kama kawaida yake anakerwa sana na jambo hili uvamizi haupendi. Mhe. Mwenyekiti, suala hili kama tulivyomuahidi katika kamati tumeanza kulifanyia kazi kama nilivyosema awali.

Nakubaliana nae kwamba wafanyabiashara ni wakati sasa wa kuwekeza katika masuala ya uvuvi wa bahari kuu. Wafanyabiashara wote wapo katika meli baina ya Dar es Salaam na Unguja tu, lakini bado hawajataka kujiingiza katika uvuvi wa bahari kuu. Kuna fursa nyingi, kuna kipato kingi na kuna matumaini makubwa. Kwa hivyo, nakubaliana nae na kupitia hadhara hii natoa wito kwa wafanyabiashara wote wa Zanzibar kuona kwamba wanawekeza katika masuala ya uvuvi ili kuchuma rasilimali yetu iliopo bahari kuu.

Mhe. Mwenyekiti, pia Mhe. Bikame Yussuf Hamad pongezi zake tumezipokea tunamshukuru. Suala la ujenzi wa soko la Tumbe hoja zake tunazichukua. Amesema kwamba upatikanaji wa samaki ni mkubwa lakini suala la ghala baridi na mitambo ya barafu hakuna.

Mhe. Mwenyekiti, *design* iliyofanywa ya ujenzi wa soko lile ndio maana likaitwa soko la kisasa ni kwamba ndani yake kutajengwa pia ghala la barafu na pia kutakuwa na mitambo ya baridi ya kuhifadhi samaki. Kwa hivyo, tukijaaliwa baada ya soko lile kumalizika masuala ya kuuza samaki bure bure au kuoza litakuwa limeondoka.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu bei ya mwani namshukuru sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko wale wote waliozungumzia suala la bei ndogo ya mwani tunalifanyia kazi mimi na Mhe. Waziri wa Biashara, tumeshakaa pamoja, tuna mipango madhubuti kuona kwamba wakulima wa mwani kazi yao ni kuzalisha mwani wenye *quality*. Kwa hivyo, tutahakikisha kuona kwamba mwani wetu umepata bei nzuri na hilo tunalifanyia kazi. Kwa vile ameanza na karafuu naamini na mwani hauwezi kumshinda.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Abdi Mosi Kombo namshukuru sana kwa mchango wake suala la uvuvi tumelipokea tunalifanyia kazi na kwa kweli yote ambayo amezungumza ushauri wake tunauchukua. Yeye ni mvuvi namfahamu sana nishakwenda Matemwe kishanichukua nimeshawaona wavuvi wake, nimeshazungumza. Matatizo yao ya suala lile la Mnemba tumelizungumza katika kikao alikuwepo Mkuu wa Wilaya, alikuwepo Mwakilishi mwengine lakini *Alhamdulillah* tumefika pahala pazuri wameniamini wananchi wale wa Matemwe bado nalifanyia kazi.

Baada ya bajeti hii nimeomba kabla ya mwezi wa Oktoba katika kikao tutahakikisha kwamba tatizo la Mnemba litakuwa limeshafanyiwa kazi. Kwa hivyo, Mhe. Abdi Mosi Kombo wapelekee salamu watu wa Matemwe na waambie kama walivyoniamini waendelee kutuamini kwamba suala lao litapatiwa ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mifugo ya mbuzi ni kweli kwamba kulikuwa na baadhi ya maeneo wamepelekwa mbuzi wasio wazuri lakini tuna tatizo. Mhe. Mwenyekiti, wakati wa kuibua miradi wananchi wetu kidogo wawe makini. Kwa sababu mimi hapa nina vikundi ambavyo vimepatiwa msaada na *TASAF* kupitia *MACEMP* lakini katika aina ya miradi waliyoichagua walichagua hasa mbuzi wa kawaida. Katika miradi hii kuna mbuzi wa maziwa na mbuzi wa kawaida. Sasa baada ya kuona wenzao wanakamua maziwa kutoka kwa mbuzi ndio watu wanaanza kulalamika. Kwa hivyo, nawashauri sana wananchi wanapoibua miradi basi wajue hasa wanaibua miradi ya aina gani.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Salma Mohammed Ali kwa mchango wake. Tatizo la huduma ya kitaalam na ukosefu wa vyombo vya usafiri ni kweli tunalo na tumesema katika changamoto tunazo tunalifanyia kazi. Tumeanza kupeleka pikipiki tatu wiki iliyopita Pemba hazitoshi tunajua

lakini zitaanza kuondoa tatizo. Wataalam hawatoshi nimesema katika kitabu changu cha bajeti. Lakini kuna mpango wa kuajiri tumeshazungumza na Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora tayari tumelikabidhi kwake ametwambia tusubiri kidogo mambo yawe mazuri bajeti ipite. Naamini kwamba mara baada ya bajeti hii tutaruhusiwa kuajiri na tukiajiri basi tatizo la wataalam litamalizika.

Suala la umbali na la wataalam wangu kuwa hawapiti piti ni kweli na tutajitahidi kuwawezesha kuwapatia vyombo vya usafiri ili waweze kuwahudumia wananchi. Kwa kweli wataalam wangu hawapendi kukaa ofisini lakini kwa sababu ya uhaba wa vyombo vya usafiri hulazimika kufanya hivyo wengine huenda kwa baiskeli, wengine kwa miguu. Lakini tukijaaliwa tumekubaliana kwamba tutawapatia vifaa vya usafiri na tumeanza kutoa pikipiki Unguja tano na Pemba tatu ili kuona kwamba angalau kidogo hali inakuwa nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, suala la maabara la Chake Chake kuhusu kupatiwa vifaa vya maabara. Tumezungumza na Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili ambaye ndio anayeendesha Mradi wa *ASSP-L* ameshakubali kwamba kupitia mradi wake maabara ya Chake Chake na zile zote ambazo zimejengwa basi atazisaidia vifaa. Mhe. Waziri nakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwakilishi alizungumza suala la soko la Mvumoni. Kweli Mhe. Mwenyekiti, tuna tatizo kidogo na soko la Mvumoni. Wananchi wenyewe waliomba kupitia *TASAF* na *MACEMP* kujengewa soko. Wizara tukishajua kama fomu imetimiza masharti letu sisi ni kutoa fedha. Kwa hivyo, zikatolewa fedha soko likajengwa lakini bahati mbaya wenyewe waliotaka soko lijengwe katika eneo husika hawalitumii. Mimi mwenyewe nimekwenda nimekaa na Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake, nimekaa na Katibu wa Halmashauri ya Chake Chake, Sheha, Diwani, Mwakilishi alikuwa anaumwa, kumuomba wafanye kila jitihada waone kwamba pesa hizo zitumiwe na serikali.

Kwa hivyo, pesa kama karibu milioni 30 zimetumika kujenga soko kubwa la kisasa kabisa lakini bahati mbaya halina matumizi. Nawaomba sana viongozi wa Wilaya ya Chake Chake, Jimbo la Wawi, pamoja na viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake kuona kwamba kadri walivyoomba sisi tuliwapa lakini sasa ni wakati wa kuona kwamba soko lile wanalitumia.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Salma Mohammed Ali alitupa ushauri wa kushirikiana na Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Ushauri huo tumeuchukua na Mhe. Waziri mwenyewe umemsikia tunashirikiana vizuri tunafanya kazi kwa karibu kabisa.

Mhe. Mussa Ali Hassan tunashukuru vyombo vya uvuvi tutavitafuta tunajitahidi na hilo tutashirikiana na wawekezaji wa nje kuona kwamba wanakuja kuwekeza ili watu wetu wapate vifaa kwa ajili ya kuvulia. Pia Mhe. Mussa amezungumzia suala la mwani Mhe. Waziri ameshatoa jibu.

Mhe. Farida Amour Mohammed amezungumza suala la *potential* ya ufugaji katika Wilaya ya Wete. Ni kweli Wilaya ya Wete ina *potential* nyingi, ina ardhi yenye rutuba. Wizara kwa kweli ina mikakati mingi na Wilaya ya Wete kama ambavyo ina mikakati mingine katika maeneo tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, Wilaya ya Wete tutajitahidi kadri iwezekanavyo kwamba wawekezaji wakija nao tupeleke na tumeshaanza katika shamba la Chamanangwe. Mimi mwenyewe nimeshakwenda pale na wawekezaji wawili kutoka nje ya nchi wamekwenda shamba wamelipenda wanaandaa utaratibu kupitia *ZIPA* wakiwa tayari serikali ikaona ni *potential* kuna maslahi na nchi basi watapewa wataliendeleza.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi ya darasa Ole ni kweli ipo mimi mwenyewe nimeshakwenda. Wazo letu kwa ofisi ile na madarasa yale ni kuanza kufungua kituo kidogo kwa ajili ya kufundisha ufugaji kwa wafugaji wa Pemba nzima. Kwa hivyo, ni eneo ambalo ofisi zipo, *facility* zipo, tutazitayarisha kidogo baadae kila makundi tutachukua ili kuona kwamba wanapata taaluma kupitia ofisi ile.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Farida Amour Mohammed alizungumzia suala la kituo chake cha uvuvi Kangagani. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba kikundi chake cha Kangagani hakikupata nafasi ya kwenda mara hii lakini zilikuwa chache, nafasi zilikuwa 30 haikuwezekana kuzigawa kwa vikundi vyote vinavyofuga Unguja na Pemba.

Lakini kama nilivyoahidi katika hotuba yangu ni kwamba mara kundi hili likirudi kundi jengine litaandaliwa na litakwenda China. Kwa hivyo, wale wote ambao wamekosa fursa mara hii basi wajiandae *Inshaallah* watakwenda katika kundi linalokuja.

Mhe. Farida Amour Mohammed alizungumzia suala la ughali wa madawa ya mifugo na hili pia alizungumza Mhe. Salma na Mhe. Ismail Jussa Ladhu kuhusu ughali wa madawa ya mifugo na vyakula. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwa sababu mambo haya yako katika sekta binafsi, wao ndio wanaoleta. Lakini sisi kama wizara tumeona kwamba kuna tatizo kubwa la wafugaji wetu kuweza kuendelea kwa namna ya ughali wa madawa na ughali wa chakula. Tunashauriana karibu sana na Waziri wa Fedha, kuangalia tutafanyaje katika

hili. Baadhi ya nchi katika ulimwengu wa leo wanatoa *subsidization* katika masuala haya. Sasa sisi tunaiangalia uwezekano wake, uwezo wetu, polisi yetu, ikiwezekana basi mazungumzo yetu na Wizara ya Fedha yakiwa mazuri basi tutahakikisha kwamba na sisi wafugaji wetu tunawaangalia ni namna gani ya kuwafidia. Lakini siwezi kusema kwamba ni mwakani au lini, ni mazungumzo baina ya wizara na wizara pamoja na serikali kuu kuona ni namna gani hatma ya wafugaji wetu katika masuala ya fidia ya dawa na vyakula kwa mifugo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Farida Amour Mohammed pia alizungumzia suala la maghala ya samaki. Mhe. Mwenyekiti, hii kwa kweli ni hitaji ya maeneo mengi sana. Sasa sisi kama wizara tutajitahidi kwa upande wetu lakini sekta binafsi nayo inaweza kufanya kazi nzuri katika hili, tunawaomba waingie kati hii biashara inaweza kuanyakazi vizuri na *Inshaallah* tukijipanga vizuri basi tunaweza kwenda vizuri.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Mtando wa Jimbo la Kikwajuni, kwanza alitaka kufahamu masuala ya mpango kazi wa ukusanyaji wa dagaa na mpango kazi wa kuendelea wavuvi wadogo wadogo. Mhe. Mwenyekiti, tumeandika *concept paper* mbali mbali, tumeshazisambaza, kopi ninazo na akitaka nitampa na zitakapofanikiwa kwa kweli zitafaidisha wavuvi wote wa Unguja na Pemba na wakaushaji dagaa wote wa Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, tunapanga kwa kusaidiana na washirika wa maendeleo na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, kuondokana na utaratibu wa kukausha dagaa kwenye jua. Kwa kweli hii ni hatari sana. Kwa hivyo mpango tuliopanga ni ya viwanda vidogo vidogo, tumeshaipeleka katika Washirika wa Maendeleo, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko wameshaichukua na wanaifanyia kazi ili ikiwezekana pale Maruhubi pajengwe viwanda vidogo vidogo vya ukaushaji dagaa na pia katika jimbo lake nimeshakwenda mimi mwenyewe lakini yeye hajui. Lakini ni kweli pana potantion kubwa sana. Lakini kwa kweli pana *potential* kubwa sana nakubaliana na yeye.

Mhe. Mwenyekiti, kuna siku mimi na Mhe. Nassor Mazrui tulikuwa tunazungumza, kwamba kwa nini hatukihamishi kiwanda kilichoko Nungwi tukakipeleka pale kwa ajili ya watu wale. Tukazungumza tukasema hapana jamii haitatufahamu, lakini eneo lile tunalijua kwamba linazalisha dagaa jingi, utaratibu wa ukaushaji sio mzuri, kile ni chakula ni lazima serikali iandae utaratibu ambao utakuwa unaukaushaji mzuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, suala la hatimiliki ni maeneo mangapi yameshapata hatimiliki na mangapi hatujapata. Mhe. Mwenyekiti, hatujapata hatimiliki hata moja. Hivi sasa tunachokifanya ni mipango na tumeyaorodhesha maeneo yetu, tumeshampelekea Waziri wa Fedha na sisi tumeshachukua na tunashirikiana

katika kuyatafutia hatimiliki. Kuna *process* kubwa, kuna kuyapima yanahitaji gharama kidogo na mambo mengine. Kwa hiyvo, kazi hiyo inaendelea iko chini ya Idara ya Uhakiki Mali ya Serikali inafanyakazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kwa vile muda haututoshi na shughuli ya Mhe. Waziri hii haijamalizika sasa basi niwaombeni tumuombe Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, ili tuangalie utaratibu wa kuweza kuweka kanuni kando ili tuweze kumaliza hii shughuli tuliyonayo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Waziri hajaweza kumaliza kufanya majumuisho na muda ulio mbele yetu hautoshi kumaliza shughuli iliyo mbele yetu. Kwa hivyo, naomba tuweke kanuni kando ili tuweze kumaliza shughuli zilizokuwa mbele yetu. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyooshe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na nawashukuru na Waheshimiwa Wajumbe, kwa kukubaliana kwamba tuendelee mpaka tumalize, *Inshaallah* tutamaliza baada ya muda mchache tukijaaliwa.
Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwakilishi alizungumzia suala la gari ya uvuvi ya *World Bank*, iliyonunuliwa kwa dola 40,000 mwaka 2006. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa mjumbe wa kamati ya *PAC* ya Baraza lako, Mwenyekiti, wetu alikuwa ni Mhe. Abass Juma Muhunzi na Makamo alikuwa ni Mwenyekiti wa sasa na wajumbe wengine ni Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Fatma Ferej, Mhe. Haji Faki Shaali na wengine.

Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka kuipata wakati tuna kamati ya *PAC* wakati ule, kama kumbukumbu zangu ni sahihi na ni wakati ambao kamati hiyo ya *PAC* Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa enzi hizo za upinzani na serikali, tukajaribu kuifuata. Mimi siku hizo nilibandikwa jina la Mwanasheria wa Kamati. Tukaifanyia kazi kwa karibu sana, tukaitafuta kila panapotafutwa, tukaambiwa kuna *special audit* imefanywa. Nakumbuka vizuri sana, kwa hamu ya kuiweka serikali kwenye kona, tukajaribu kuitafuta *special audit.* Kwa wakati huo ilikuwa *CUF* na CCM Barazani. Lakini mimi nilisalimu amri kupata ukweli wa hoja hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, *World Bank* ina utaratibu wake wa matumizi ya pesa, ukiukosea utaratibu wake basi mtagombana, hata kama hujaiba mtagombana. Mimi nilipoingia wizarani juzi nilimwambia Katibu Mkuu nipe hali ya fedha ya *MACEMP,* nitakupa mfano mzuri. Akanipa nikaona matumizi yanavyokwenda,

sikubaliani na utaratibu ulivyo. Kwa nini kwamba utaratibu wa World Bank, ni lazima utumie kifungu kile kile. Unaweza mradi ukawa na mabilioni ya shilingi, lakini ukakosa mafuta ya kwendea kazini, kwa sababu kifungu cha *operation* hakina kitu. Kwa hivyo, nikamwambia katibu kama vifungu hivi vimeshapata basi hivi visitumiwe, ndio maana nikasimamisha ujenzi wa ukuta kwenye *MIMKA* na MENAI ambayo pia mheshimiwa amehoji. Sasa niruhusu ujenzi uendelee kukiuka utaratibu wa matumizi ya *World Bank* haiwezekani, nikawaambia subirini mpaka vifungu vya ujenzi vitiliwe pesa. Tumekaa muda mrefu hawajataka kufanya *reallocation of bank* nikamwambia katibu zuwia. Vijana wanalalamika mheshimiwa hatuna mafuta, nikawaambia hamna, ujenzi simamisha.

Kwa hivyo, juzi *World Bank* wametoa *reallocation*, nikawaambia sasa tumieni. Kwa hivyo, kwa sababu ya ujenzi tatizo ni hilo. Umesimama muda mrefu kwa sababu fedha za ujenzi katika kifungu ilikuwa hakimo na mimi kama waziri kazi yangu moja ni kuisimamia wizara kuona mambo yanakwenda sawa sawa. Kwa hivyo nisingeruhusu watu watumie tu, kwa sababu fedha ziko. Kwa hivyo, nikamwambia simamisha ujenzi au utachelewa, nikamwambia hata hauchelewi, lakini hatuwezi kuitia serikali ije itiwe kona na World Bank kwa sababu ya matumizi mabaya.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya gari nayo, nimeambiwa ilikuwa na tatizo kama hilo, kwamba World Bank wali *query* utaratibu gani mmetumia pesa katika vifungu ambavyo sivyo, kwa hivyo mimi siruhusu. Mhe. Mwenyekiti, na akasema vijana hawa wapewe *procurement* wote wakasomeshwe inaonekana hawana taaluma ya *procurement*. Kwa kweli nashukuru amewasaidia sana wale vijana na sasa hivi wako makini sana. Kwa hivyo, tatizo lile Mhe. Mwenyekiti, liko hapo sio tatizo la wizi, lakini ni masuala ya *reallocation* na matumizi katika suala hilo. Kwa hivyo, ngeomba kusema hilo na juzi lilitaka kunifika mimi, lakini kwa sababu najua mambo yanavyokwenda na kwa taaluma nzuri aliyonipa Mhe. Omar Ali Shehe alipokuwa Mwenyekiti wangu wa kamati, kwa kweil nimejaribu kuhakikisha kwamba tunakuwa makini katika suala la matumizi ya serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, suala la wavuvi ambao walinyang'anywa mitego yao. Mhe. Mwenyekiti, sisi katika wizara tunakwenda kufanyakazi kwa mujibu wa sheria. Baraza la Wawakilishi hili huwa linatunga sheria mbali mbali. Sisi mawaziri majukumu yetu ni kuhakikisha kwamba sheria zinazotungwa chini ya wizara zetu ni lazima tuzishughulikie vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhania Mhe. Mbarouk Wadi Mtando, angetupongeza badala ya kutushtumu. Watu wake wamekamatwa wanatumia mitego ya uvuvi haramu. Mwenyewe amekubali. Sisi ilikuwa tuwapeleke

mahakamani hawa, kwa vile umekubali mwenyewe ina maana watiwe hatiani. Kwa hivyo, wakati mwengine huwa hatufanyi hivyo, lakini hatuwezi kukamata mitego ya macho madogo kisha tukamzawadia muhalifu, hayo hatufanyi. Yaani ukamatwe unaharibu kwa mtego wa Shs. 50,000, kisha mimi niwazawadie kipande cha laki 500,000. Sasa kila mtu si atakwenda tu kuchukua mitego ya uvuvi haramu akavua akijua siku ya pili nikienda kule nitapewa mtego mwengine, hiyohaiwezekani. Sasa Waheshimiwa Wawakilishi tusaidieni. Haiwezekani kama mtu keshakuwa mwalifu halafu sisi tumzawadie, hilo haliwezekani kabisa. Tusaidieni kwamba wavuvi wetu wasivuwe kwa kutumia mitego haramu. Sheria hii hapa inakataza ambayo tumeitunga sisi wenyewe katika Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, katika makubaliano ya kuanzishwa uhifadhi ni kweli kwamba kuna utaratibu wa kugawana mapato. Mapato asilimia 70 yanakwenda katika kuongoza ile hifadhi yenyewe, asilimia 30 inakwenda kwa jamii. Hii tunafanya kwa *MIMKA*, *MENAI*, *NEMBA* na *PEC* Pemba tunafanya hii. Kwa hivyo, sio kweli hata kidogo kwamba hakujaenda kitu. Mimi nimekwenda juzi *NEMBA* Wamatemwe wengi, hivi hamjapata kweli nyinyi, wakasema hatujapata, tumepata milioni 1. Karatasi ninayo, nikamwambia Mkuu wa Wilaya, mheshimiwa vipi hii. Akaniambia aah! Tumeshapewa hii. Mimi nafikiria tatizo liko huko sio huku, mgao unatoka unakwenda, matumizi yako kwao kamati ya uvuvi inakaa inasema tuzitumie vipi. Sisi wakija tunasema wape mgao wao.

Mhe. Mwenyekiti, kulikuja suala la ugawaji wa maboti ya uvuvi. Suala hili alilizungumza Mhe. Mbarouk Wadi Mtando na alilizungumza Mhe. Hija Hassan Hija. Kwanza utaratibu wa ugawaji wa maboti, pesa za *MACEMP* hazisimamiwi na wizara yangu. Sisi ni watowaji pesa tu, matumizi yanaanzia kwenye shehia, watu wanajaza vikundi vyao kwenye shehia. Masheha watu wao wanajaza kwenye vikundi, wanakwenda wilayani vinapitishwa, vinakwenda katika kamati ya *TASAF*, vinapitishwa, vikishapitishwa. Sisi ndio tunauliza je, kikundi hiki kinakwenda *inline with the demand* ya *World Bank*, haiharibu mazingira basi sawa *this is your money*. Kwa hivyo, sisi siowatowaji wa maboti, hapana, kamati za shehia na kamati za wilaya ndio wanaohusika na maboti, sisi tunatoa pesa za kununua boti. Kwa hivyo, kama boti imeuzwa na najua nyengine zimeuzwa, mwenyekiti wangu wa kamati anajua, nyengine zimepigwa moto, wamefanyakazi hiyo wamekwenda.

Ni kweli. Sasa hivyo vikundi Waheshimiwa Wajumbe, ni vyenu sio vya wizara, vikundi viko katika shehia, viko katika wadi na viko katika majimbo yenu, visimamieni ili kuhakikisha kwamba vifaa vilivyopatikana vinafanyiwa kazi vizuri. Hamuwezi kuiga wenzetu. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, vikundi ni vyako vya Kikwajuni, sio vya kwangu, kwa hivyo kama kimepatiwa boti basi

uhakikisha kwamba kinaendelezwa na kinafanyakazi vizuri. Lakini sisi Mhe. Mwenyekiti, kazi yetu ni kutoa pesa baada ya kamati ya shehia. Ile inaitwa *MACEMP, TASAF*. Mhe. Waziri anajua sana, *MACEMP, TASAF***.** Kwa hivyo, tutashirikiana pamoja, sisi ni watoa pesa hatuna mambo mengine, baada ya wenyewe kusema kwamba wanataka vikundi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe Fatma Mbarouk tunamshukuru sana kwa michango yake na ushauri wake tunauchukua na tutaufanyia kazi. Amezungumza kitu kimoja muhimu sana, suala la ukatili wa wanyama. Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo baya sana. Pia Mhe. Haroun Ali Suleiman naye amelizungumzia, hili jambo ni baya sana halifai hata kidogo, tumepoteza hata zile hisia za huruma. Haiwezekani mnyama tumtese kiasi kile na sisi katika wizara tuna kitengo maalum tumekianzisha kwa ajili ya kutoa taaluma hii tunashirikiana, kanuni zinaturuhusu tukamate. Tumewahi kukamata na kuwapeleka mahakamani. Kwa hivyo, kukamata tu sio adhabu muhimu, tuelimishani kuhusu tabia hii mbaya sana dhidi ya ukatili wa wanyama sio jambo zuri. Nakushukuru sana Mhe. Mwakilishi hasa kwa vile unatoka Jimbo la Amani. Tutashirikiana pia na Mhe. MBM pale Mhe. Machano Othman Said ili kuona kwamba suala hili kwa pamoja mimi wewe, Mhe. Machano Othman na Mhe. Hamza Hassan Juma akija ili kuona suala hili tunalipiga vita kwa kiwango kikubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mohammed Haji tunakushukuru mchango wako umekuwa mzuri sana, mtu mzima sana na umetuelekeza vizuri sana, tunakushukuru. Kwa kweli yale yote ambayo umetupa hasa kuongeza taaluma tutayashughulikia. Umezungumza suala zuri sana kuhusu taaluma ya wafugaji, ukosefu wa tiba ya mara kwa mara. Ni kweli, haya ni mambo ambayo yamo katika mipango na mikakati yetu na tutayashughulikia.

Vile vile Mhe. Mjumbe ulizungumzia suala la makusanyo kwa upande wa Pemba, ukisoma kile kipengele cha mwisho cha Pemba basi utaona kwamba pale kuna eneo ambalo makusanyo ya Pemba yamewekwa na yapo katika Idara ya Tiba. Kuna ya Pemba na ya Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, pia alizungumzia suala la uvuvi mbalo nimeshalijibu kama ambavyo umelizungumza. Mhe. Hassan Hamad Omar *Super* A wa Kojani, tunakushukuru sana kwa mchango wako, kwa kweli hili ni eneo ambalo wavuvi wa Kojani hupenda sana wakusikie na kwa kweli mimi nimeshakuja Kojani, nimeshakaa na wewe na Wakojani wako, tumeshakubaliana kuanzisha hifadhi, naona leo unanigeuka mheshimiwa. Kwa hivyo, tutahakikisha kwamba wakati tunaanzisha hifadhi basi itakuwa hifadhi ambayo wavuvi wa Kojani hawata athirika katika shughuli zao za uvuvi. Hilo tutahakikisha mheshimiwa kwa sababu tunajua mazingira ya Kojani na tunajua shughuli zao.

Vile vile Mhe. Mjumbe alizungumzia suala la leseni kupewa mara mbili. Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Uvuvi Zanzibar na Idara ya Uvuvi wa Tanzania Bara zinaongozwa na sheria mbili tofauti. Masuala ya uvuvi sio suala la Muungano. Kwa hivyo, mvuvi akitoka Kojani akienda Mtwara itabidi akate leseni na akitoka Mtwara akija Msuka itabidi akate leseni hata kama kule keshakata. Kwa hivyo, haya maeneo mawili yanasimamiwa na sheria mbili tofauti. Kwa hivyo, tunawaomba wavuvi wetu walifahamu hilo kwamba uvuvi sio suala la Muungano, kwa hivyo kila pahala pana sheria yake, taratibu zake na kanuni zake na ada zake. Kwa hivyo, ukikata hapa subiri mwaka umalize kabla hujenda kule, ukenda tena kule itabidi ukate nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la Hifadhi ya Methali malalamiko yako tutayachukua na kuyafanyia kazi, kama yako hayo sio jambo zuri Mhe. Mwenyekiti. Hatuwezi kuwabagua wavuvi wetu katika maeneo ya hifadhi jambo hili tutalifanyia kazi kadiri itakavyokua.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile alizungumzia suala la ukulima wa mwani, nimeshalijibu. Vifaa vya uvuvi vya bahari kuu. Suala hili tunalifanyia kazi. Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na yeye kwamba wavuvi wa Kojani ni wazuri. Kama wiki moja hivi alikuja mwekezaji wizarani kwangu kuekeza. Akasema katika meli atakazoleta, ni lazima muwe na wavuvi wa Kojani. Kwa hivyo, ni kweli kwamba wavuvi wa Kojani wanasifa kubwa hata nje ya nchi uwezo wao wa kuyakamata maji, hongera sana Mhe. Mjumbe.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu, nakushukuru sana kwa mchango wako, mchango wako umekuwa mzuri *very constructive* kama kawaida yako. Kwanza ulitaka kuzungumzia suala la mwekezaji Ali Yussuf. Jambo hili alizungumza Ustath wa Rahaleo. Wewe umetushauri kwamba hapana. Muwe makini sana. Tunakushukuru. Mhe. Mjumbe alituambia mmm! Kuweni laini kidogo maana mnapoteza muda. Sasa nyote kwa kweli mnatuelekeza nini tufanye. Tutahakikisha kwamba wawekezaji wote wanaokuja, hauuwi hata kidogo uwekezaji wetu, kwa sababu sisi tuna jukumu la kuwaendeleza, hatuwezi kuleta mtu hapa, akaja aka-*flash* mayai laki moja kwa siku, watu wetu na viyai vyao vikaanza kudoda hatuwezi kufanya hivyo.

Kwa hivyo, tutahakikisha kwamba kila mwekezaji anayekuja anahakikisha kwamba tunaweka *terms* ambazo zita-*develop* wafugaji wetu wadogo wadogo wa kuku, ili kuona kwamba tunawakuza badala ya kuwadumaza.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Nassor Salim Ali Al Jazeera, tulichofanya ni hicho ambacho Mhe. Ismail Jussa alichotushauri, kwamba tuwe makini kidogo tusije tukawauwa wafugaji. Kwa hivyo, tunaangalia au tuna *deal* naye kwanza. Punguza hili au tukifika pahala tukiona maslahi ya nchi hayapo basi

tutamwambia karibu, hatuwezi kuvumilia hata kidogo.

Vile vile Mhe. Ismail Jussa alizungumzia suala la madaktari wa mifugo. Kweli, hata hivyo nilisema kwamba tunaupungufu na tutajitahidi Mhe. Mwenyekiti. Ushauri wako tunauchukua kwamba hili ni eneo la kulisimamia zaidi, hatutolikalia kitako. Kama alivyosema Mhe. Waziri Haroun, hatutolikalia kitako lakini tutalisimamia, usiwe na wasi wasi.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la Makurunge. Ni kweli Zanzibar iliazimwa Shamba la Makurunge, haikupewa. Maana yake kupewa ni lazima upewe hatimiliki. Kwa hivyo, muda wote serikali imekuwa ikiitaka hatimiliki. Kuna *infrastructure* pale, mimi mwenyewe nimeshakwenda, lakini haikuwezekana. Kwa hivyo, mpaka umefikia wakati hatukulipata, zilikuwa hekta 30,000. Wenyewe wameshazichukua hekta 24,000, zimebaki hekta 6,000 na hizo hekta 6,000 hawajataka kutoa hatimiliki kwa kadiri ninavyofahamu mimi. Kwa hivyo, suala hili analo Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili, kwangu mimi nimempasia, nimemwambia mzee chukua ngoma hiyo, yeye ataichukua kwa sababu ya kuendeleza Chuo cha Kizimbani tunachokifanyia kazi, lakini tunaamini kwamba kwa mahusiano mazuri tuliyonayo hivi sasa, watu wazima wameingia kati hapo, tutahakikisha kwamba baada ya muda tutapata hatimiliki ili tuweze kulifanyia kazi vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu soko la Malindi kuwa likoje. Ni kweli soko la Malindi hadhi yake sio nzuri, lakini ni eneo mbalo kwa mjini ndio eneo ambalo tunaweza kujenga soko. Kwa sababu ya kina chake kirefu cha maji chini ya soko. Kwa hivyo, bado tunaendelea na mazungumzo na Serikali ya Japan, nimemuomba kwamba ikiwezekana mwaka huu aanze kutujengea soko pale.

Tulikuwa na eneo la Kizingo, wajumbe wengine wamelizungumza hapa. Mhe. Mwenyekiti, eneo la Kizingo ni tatizo kidogo, kwa sababu maji yakijaa eneo la Kizingo basi yako juu kuliko viwanja vile vya mpira na ndio ukaona siku hizi maji yanaingia sana. Kwa hivyo, lile eneo ni *very sensitive*. Kuli *tempo* kwa aina yoyote tutakuja kuyaona maji yameshakuwa Darajani ya chumvi. Kwa hivyo, utaratibu wetu ni kwamba ni eneo zuri lakini kimazingira tunaliogopa na kwa uchunguzi mdogo uliofanywa tukaona hapana tusiliingize katika hili ili kuzuia kuathiri mazingira tukaja kupata mafuriko ya maji bahari katika maeneo ya Mji Mkongwe. Mhe. Ismail Jussa Mji Mkongwe utakuja kuwa hukai kwa sababu maji yakitoka kule kasi yake moja kwa moja mpaka Mji Mkongwe na jimbo ndio hilo kutakuwa mtihani kidogo. Kwa hivyo, tunaomba kwamba ukubaliane na sisi na ushauri wa kitaalamu tuliopewa kwamba hili tuliache kwa ajili ya uhifadhi wa mazingira ya Mji Mkongwe.

Mhe. Mwenyekiti, ufafanuzi kuhusu *MACEMP*. Katika ukurasa wa 59 Mhe. Mwenyekiti, hatujataja lolote kuhusiana na mapato ya bahari kuu. Naomba aangalie kiambatisho nambari 8, katika ukurasa wa 65, kifungu 08 Unguja. Kuna huduma za utibabu, leseni za uvuvi, mazao ya baharini na mapato mengineyo. Mapato mengineyo yalikadiriwa kuwa milioni 925,447,000 zilizokusanywa mwaka 2010/2011 ni milioni 257,512,136 hayo ni mapato ya uvuvi wa leseni za bahari kuu.

Mhe. Spika, ufafanuzi ni kwamba 2009/2010 idadi ya meli zilizopatikana ni 50 na mapato yaliyopatikana kwa jumla ni dola 1,296, mwaka 2010/2011 meli 72 mgao asilimia 50 ni kwa mamlaka, Zanzibar asilimia 20 na SMT asilimia 30 zilizobakia. Sasa ukipiga mahesabu hapo utaona kwamba asilimia 20 na hizo ni dola 171 na 8 na ukipiga mahesabu kwa *rate* utapata hizo shilingi 257,502,135 na hayo ndio mapato ya bahari kuu.

Mhe. Mwenyekiti, pia alikuwa akizunguzia kiambatanisho cha 59 kinachohusiana na masuala ya *MACEMP*. Usahihi wake ni kwamba fedha yote ambayo tumeipata kutoka kwa *MACEMP* ni dola 61.7 na sisi tumepata asilimia 40 ndio hizo zinazokuja dola 25 na kidogo.

Kwa hivyo, fedha hizo ndizo ambazo tunazitumia na zimebakia kidogo, ambazo tunaendeleanazo katika masuala ya ujenzi pamoja na ununuzi wa vifaa vya afisi zinazojengwa, tunategemea kukamilika mwakani na baada ya hapo tutaanza utaratibu wa kuomba *MACEMP II* na Inshaallah tuombe Mwenyezi Mungu atujaalie kuipata. *(Makofi)*

Vile vile Mhe. Mjumbe alizungumzia suala dogo la ujenzi wa Makamo Makuu ya Bahari Kuu. Mhe. Mwenyekiti, lile jengo linajengwa na yeye mwenyewe amekwenda na kuliona, kwa sababu nimemualika kama alivyosema mwenyewe.

Kwa hivyo, mjenzi ni kampuni moja ya Kichina na gharama yake ni dola milioni 1,300,000. Kati ya hizo *MACEMP* Bara watatoa shilingi milioni 700,080,000/= sawa na asilimia 60 na Zanzibar itatoa shilingi milioni 500,020,000/= sawa na asilimia 40. Mhe. Mwenyekiti, kama ule mgao ulivyokuwa wa ile 61 basi na huu ujenzi umekuja hivyo. Kwa maana hiyo, jengo lile ni letu pamoja na lipo pale Fumba.

Kwa mfano, mimi na wewe tumekubaliana kwamba Gando na Mji Mkongwe tufanye biashara, basi wewe ndio wa kwanza utakaesema bora afisi ijengwe Mji Mkongwe na mimi nitasema ijengwe Gando, kwa sababu tunafanya hivyo lolote litakalotokea, basi ofisi umeshakuwa nayo unaweza kuuzia japo mabungo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, afisi tunayo ambayo ni nzuri sana na juzi nimeitembelea iko katika hatua za mwisho na *Inshaallah* kabla ya kumaliza mwaka huu Mwenyezi Mungu akitujaalia tutakwenda kuifunga kwa ajili ya matumzi. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Moh'd Ali tunamshukuru ametupa ushauri mwingi kama vile tujitahidi katika kuzuia uvuvi kwenye maeneo mengine yasiyo na hifadhi, suala hili tutajitahidi. Pili ni kuhusu suala la uwelewa na taaluma ni kweli si jambo zuri Wazanzibari sote tuwe pamoja, kwa sababu mambo mengine hayahitaji nguvu moja kwa moja na ukiwaeleza watu kidogo kidogo basi watakwenda.

Vile vile kuhusu majosho, tayari tumeshaanza na josho la Mjimbini kutokana na hali yetu na hali ikiruhusu basi tutaongeza na maeneo mengine. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kumtoa ng'ombe Wambaa na kumleta Mjimbini ni tatizo, lakini tumeona ni katikati wa Kengeja anaweza kuja, lakini hali ya fedha itakaporuhusu kwa sababu kama nilivyosema kwamba tunao mpango wa kuanzisha miundombinu ya ufugaji, yaani *infrastructure for livestock* na hiyo ndio kazi tunayoifanya. Kwa hivyo, tutajitahidi kueneza pamoja na kuyafufua yale yaliopo. *(Makofi)*

Kiwanda cha Barafu Malindi kilikuwepo kweli na hivi sasa hakipo tena.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, walivyotulia wanaonesha jinsi gani wamekufahamu pamoja na kukuelewa, hivyo nafikiri ingekuwa ni vizuri zadi ungezidi kuwafupishia.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Suleiman Hemed Khamis nakushukuru Soko la Msuka tumesikia. *(Makofi)*

Vile vile kuhusu chumvi tuitafutie na tutazungumza na Mhe. Waziri anayehusika tutazungumza na Mhe. Waziri anayehusika na hiyo haiko kwangu.

Ufugaji bado ni mdogo ni kweli tunalishughulikia hilo.

Mhe. Rufai Said Rufai ng'ombe wa kiasili ni kweli wana nyama nzuri na maziwa safi, *Inshaallah* tutaendelea kuwaendeleza. Kuku pia tutaendelea kufuga kama ulivyozungumza na kuhusu mazao ya baharini tunakushukuru na tutaendelea kushughulikia.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi mama mkwe tunakushukuru, nitakuja kwa ajili ya ya shughuli hii pamoja na shughuli nyengine. *(Makofi)*

Kuhusu wizi wa mifugo ni kweli Mhe. Mwenyekiti umekithiri. Kwa mfano, juzi Mhe. Rais alipokuwa Pemba alitupa kazi kwa pamoja tulizungumze hili kuona kwamba namna gani tutadhibiti wizi wa ng'ombe. Kwa hivyo, alishauri kwamba nyama zote zipigwe muhuri na tutalishughulikia hilo kuona tunalifanyiakazi.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili pia kuna lile la Mhe. Ismail Jussa Ladhu kuna *hygienic* ya nyama. Kwa kweli kazi yangu katika suala la uchinjaji wa ng'ombe ni kuchinja, baada ya kuchinja kazi yangu imemaliza na kile sasa ni chakula, kwa hiyo anayeshughulika ni Bodi ya Vyakula ambayo iko chini ya Wizara ya afya na hilo si suala langu tena. *(Makofi)*

Kwa hivyo, masuala ya *hygienic* pamoja na mambo mengine hayo si yangu, isipokuwa kazi yangu mimi ni kuhakikisha kwamba mnyama anayechinjwa yuko salama kwa kuliwa na akesha kuchinja hicho kinageuka chakula. Sasa anayesimamia huko ni Bodi ya Vyakula na Vipodozi ambayo iko chini ya Wizara ya Afya na amesikia na atalishughulikia suala hilo. *(Makofi)*

Suala la masoko Mhe. Mwenyekiti, liko kwa swahibu yangu Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, suala la kudhibiti *hygienic* ya masoko. Hivyo, tutashirikiana kama serikali *collective responsibility* kuona kwamba masoko yetu yamekuwa ya kileo na yanafanyakazi kileo.

Mhe. Mwenyekiti, pia Mhe. Asha Abdu Haji tunakushukuru kwa mchango wangu mzuri na tunakushukuru kwa ushauri wako na tutajitahidi kwa vikundi mbali mbali vya ufugaji pamoja na mambo mengine. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Mhe. Asha Abdu Haji aliniuliza swali moja muhimu na ninaomba nilitaje kwamba kuhusu ugomvi baina ya Uzi na Muungno unauwelewa.

Mwenyekiti, nauelewa ni kweli upo na tayari nimeshakwenda mimi pamoja na uongozi wa wizara nzima tulikaa na Mkuu wa Wilaya, Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Koani, Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak (Mwakilishi wa Viti vya Wanawake Wilaya ya Kati) pamoja na watu wa Uzi tumeacha kazi inafanywa na tunaamini baada ya muda kazi iliyofanywa Mhe. Mwenyekiti itazaa matunda kuona kwamba Wazanzibari wako pamoja na wala hawana sababu ya kugombana. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija nakushukuru sana kwa mchango wako mzuri sana ulionichangamsha, ulionielekeza ambao utanifanya nifanyekazi ya ziada, nakushukuru na ndio Mwakilishi makini namshukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, vyombo vya kuvulia kupitia bahari kuu tutavitavuta.

Vile vile kuhusu walengwa waliopewa vifaa vya *MACEMP*, inawezekana au haiwezekani, kwa sababu wanaochagua sio mimi ni huko huko kwenye shehia na wilaya. Kwa hivyo, kama shehia na wilaya wamempa asiyehusika, kwa sababu kazi yangu ni kuhakikisha kwamba fomu iliyokuja imetimiza viwango na hilo tunalikagua. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, vikundi vingapi labda Mhe. Mjumbe nimpe kabrasha hili kwa ajili ya kusoma na kuona vikundi vipangi kwa Unguja na Pemba, kila wilaya na shehia ambavyo vipo na tumevipa vikundi hivyo.

Kuhusu mapato ya bahari kuu. Mhe. Mwenyekiti, tayari tumeshazungumza.

Mradi wa *MACEMP* na matumizi na hii ndio bahari niliyonayo. *(Makofi)*

Kisakasaka na Machinjio. Mhe. Mwenyekiti, machinjio yako katika hali mbaya si kweli. Mhe. Waziri wa Kilimo na Mifugo kupitia mradi wa *ASDP-L* ananisaidia kulikarabati vizuri sana Chinjio la Kisakasaka. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mjumbe atembelee ili aone maendeleo ya matengenezo ambayo yanafanywa. Mhe. Mwenyekiti, si kweli hata kidogo labda lilikuwa hali mbaya huko zamani, lakini sasa hali yake kidogo marekebisho yanafanywa vizuri.

Kuhusu risiti pamoja na mapato yanayopatikana. Mhe. Mwenyekiti, risiti zinazotumika naamini ni risiti sawa sawa na mapato ni miongoni mwa mapato yaliomo katika Idara ya Utabibu, ambayo imeeleza humu kwamba imekusanya kiasi cha fedha na miongoni mwa fedha hizi zimetoka katika Chinjio la Kisakasaka. *(Makofi)*

Dola milioni 1 za kujenga mradi wa *MACEMP*. Mhe. Mwenyekiti, hoja hii ni ya siku nyingi na Mhe. Hija Hassan Hija anaijua si ya leo na tumekuwa tunaipigia kelele sana. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ni kweli lilikuja suala la kujenga soko zuri sana katika Mji wa Unguja siku za nyuma, wizara wakati huo haikuwahi kupata kiwanja kizuri ambacho kingeweza kujenga soko hili. Sasa badala ya kupotea hizi fedha, basi fedha hizo ndio imekuwa *transferred* Tumbe na badala yake wizara sasa inashauriana na Ubalozi wa Japan kupitia *JICA* kutujengea soko la kisasa Malindi. Hivyo, si kweli kwamba fedha zimepotea. *(Makofi)*

Shamba la Mifugo Mchangani. Mhe. Mwenyekiti, Shamba la Mifugo

Mchangani amemilikishwa mtu binafsi inavyomkina, kwa sababu serikali imejiondoa katika shughuli za uendelezaji wa mashamba. Kwa mfano, hata leo Mhe. Hija Hassan Hija ukiwa tayari ukiwa na fedha basi njoo na tukikubaliana na *terms* basi tutakukodisha Shamba la Chamanangwe, Kitumba. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mtu yeyote anaruhusiwa endapo atakamilisha masharti ya uwekezaji binafsi kumiliki mashamba ambayo tunamiliki, kwa sababu ndio sera yetu kwamba wawekezaji wa ndani na wa nje wanaruhusiwa kumiliki mashamba haya. Kwa hivyo, awe Mwakilishi ama Waziri au mtu yeyote anaruhusiwa kuja kujaza fomu kupitia *ZIPA* na wakati wowote mashamba atamilikishwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, namalizia namshukuru sana Mhe. Amina Iddi Mabrouk kwa mchango wake kuhusu *value addition* ya bidhaa ya maziwa. Kwa kweli kuna mradi mkubwa unakuja serikalini mwakani tukijaaliwa ambao unahusiana na kuongeza Thamani ya Bidhaa, tukijaaliwa watu wetu mbali mbali wategemee kupata bidhaa kupitia mradi huo.

Suala la uvuvi wa bahari kuu, *monitoring* ni kweli hilo ni suala gumu. Kutokana na hali hiyo, ni kweli tumeunda kamati ya wizara tatu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, kuona kwamba namna gani suala hili tutalifanyiakazi kwa sababu ni suala gumu sana.

Vile vile wangapi wamefaidika na hili? Tumepata tani ngapi? Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba sisi kwa sababu hatuna uwezo, yaani hatuna miundombinu ya uvuvi wa bahari kuu ndio maana meli ambazo tunazipa leseni zinakwenda zake moja kwa moja baadala ya kupitia hapa na nimezungumza hivyo katika *paragraph* 2.2 katika kitabu cha hotuba, namuomba Mhe. Mjumbe aangalie kwenye kitabu hicho. *(Makofi)*

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana Mhe. Subeit Khamis Faki kwa mchango wake, mbuzi wa maziwa Micheweni watakwenda *Inshaallah*. *(Makofi)*

Mhe. Nassor Salim Ali nakushukuru kwa mchango wako. Mhe. Mwenyekiti, watu wa Kisakasaka mashamba yao hawajadhulumiwa na bado tunaendelea wamepewa siku nyingi na dai lao limekuja na tunalifanyiakazi.

Mhe. Mwenyekiti, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote ambao wametoa mchango huu kwa kweli wamenisaidia kujibu hoja wakiwemo hawa wafuatao:-

1. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais,
2. Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika,
3. Mhe. Mwanasheria Mkuu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenyewe binafsi pamoja na wafanyakazi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, tumejitahidi kwa hali ya muda ulivyo kujaribu kujibu hoja za Waheshimiwa Wajumbe mbali mbali na nadhani nimetimiza haja. Kwa hivyo, kwa wale ambao hawakutimiza haja basi nawaomba wanivumilie na Inshaallah michango yao waliyoitoa ni nitaishughulikia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wanaokubali hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi, ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 22 – WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

Kifungu 0301	-	Ofisi Kuu Pemba	3,000,000/=
Kifungu 0401	-	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, msema kweli mpenzi wa Mungu, leo sikuwa na nia ya kupiga buti lakini kidogo maelezo ya Mhe. Waziri yamenifanya ninyanyuke kwa nukta chache tu. Kwa hivyo, nimeona ninyanyuke hapa kwa sababu nilikuwa natizama sehemu ya mapato sikuona mapato yanayotokana na Idara ya Mipango Sera na Utafiti, hivyo nimeona niulize hapa kwenye Idara ya Uendeshaji na Utumishi.

Katika mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, niliulizia mapato ambayo tunayapata kutokana na uvuvi wa bahari kuu na ule mgao wetu kutoka na uvuvi

wa bahari kuu unaosimamiwa na Serikali ya Muungano. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Mwenyekiti, katika majibu ya Mhe. Waziri amenijibu kwamba niangalie kwenye kiambatisho Nam. 8 kwenye mapato mengineyo, ambapo bila ya shaka kama si muongozo wake basi nisingejua kama ndio yanayohusika na uvuvi wa bahari kuu.

Kwa hivyo, alisema kwamba kulikuwa na makisio hayo ya 925,4274,000/=, lakini yaliyokusanywa ni 257,502,136.3030/= na kwa mujibu wa maelezo yake haya ndio yangekuwa mgao wa Zanzibar. Sasa Mhe. Mwenyekiti, naomba ufafanuzi zaidi kwa Mhe. Waziri.

Kwa kweli naomba sana katika masuala ya mapato kwanza tusione haya kudai chetu. Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilinukuu *hansard* ya Bunge ya tarehe 15 Juni ambapo nilisema Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi wa Tanzania Bara na wala simwitwi wa Jamhuri ya Mungano kwa sababu masuala haya si ya muungano.

Hivyo, alisema kwamba mapato yaliyopatikana ni jumla ya dola za Kimarekani milioni 2, elfu 74 na 400 na wala sina *calculator* nikafanya haraka *exchange rate* ilivyo hivi sasa. Lakini kwa haraka kwa *rate* hivi sasa ilivyo hizi ni kama bilioni 3 za Tanzania, kwa sababu hivi sasa *rate* iko kama dola 1,500 na inakimbilia 1,600 huko.
Mhe. Mwenyekiti, shilingi bilioni 3, asilimia 50 ingekwenda kwenye Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu ingekuwa ni bilioni 1 na nusu na tunabakiwa na bilioni 1 na nusu ya asilimia 50, ambayo hii kwa mgawanyo asilimia 40 ingekuja Zanzibar na asilimia 60 ingekwenda Bara.

Sasa katika hizi Mhe. Mwenyekiti hata mimi pocho wa hesabu Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika nilimwambia juzi na naendelea kusema, asilimia 40 hapa ni shilingi milioni 600 na sasa nafanya hesabu ya *round figure* tu na asilimia 60 ni milioni 900. Kwa hivyo, ilipaswa wao wapata shilingi milioni 900 na sisi tupate shilingi milioni 600.

Kwa hivyo, nikiambiwa mapato hayo aliyoyaeleza Mhe. Waziri ni shilingi milioni 257, huku si kupunjwa ni kuibiwa hasa Mhe. Mwenyekiti. Sasa katika hili nataka anisaidie, ndio maana pale mwanzo nilipoanza kunyanyuka katika hili nilisema tusione haya kudai chetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa hesabu hizi ambazo ni majibu halali ni *records* za serikali ambapo yalitolewa majibu Bungeni, hapo kuna chetu. Kwa hivyo, sitaki nimuonee Mhe. Waziri wangu kwa hoja ambayo mimi na yeye pamoja na wananchi wa Zanzibar tumeibiwa, kwa sababu wakati mmoja ilikuwa nongwa

kwa sababu waliambiwa wezi wa mchana, lakini haya ndio yanayowafanya watu wakaitwa maneno kama hayo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, namuomba kwamba hili ani-*promise* na wala sitaki malumbano. Jambo la msingi atumie hii *hansard* ya tarehe 15 Juni akatudaie chetu kilichobakia basi nataka kauli hiyo tu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru na halafu nimshukuru sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Kwa kweli maelezo aliyosema ni kweli, lakini hatujaibiwa na sisi tuko makini vile vile kuona kwamba fedha yetu haibiwi.

Mhe. Mwenyekiti, tumesema kwamba mapato ya mwaka 2009/2010 ni meli 50 na dola milioni 1,296,000. Mapato 2010/2011 ni meli 22 dola 814,000. Jumla meli 72 ni dola 2,111,000. Sasa kati ya dola 2,111,000 zilizogaiwa ni dola 855 na 40 na zilizosalia ambazo bado hazijagaiwa ni dola milioni 1,254,960. hivyo, kati ya hizo zilizogaiwa tukipiga mahesabu hizo dola 855 na 40, basi asilimia 20 yetu itakuja 171 na 8.

Mhe. Mwenyekiti, nasema 20 kwa sababu kwanza zinagaiwa asilmia 50 zinakwenda kwa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu, asilimia 30 zinakwenda Bara na asilimia 20 ndio zetu. Kwa hivyo, ukipiga mahesabu hapo utapata dola 171 na 8 ukifanya na *rate* ya dola hivi sasa ndio utapata hiyo ambayo imo humu Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, unajua haya majibu wakati mwengine hayatuufanya turefushe vikaa bila ya sababu. Kwa kweli kama ningekuwa nasema maneno yangu Ismail Jussa Ladhu ningesema kama nimefanya makosa, kwa sababu majibu ya Mhe. Naibu Waziri ambapo amekusanya hiyo aliyoipata dola 2,000 au dola milioni 2, amekusanya ya mwaka 2009, 2010 na 2011 ndio ameipata ile.

Sasa majibu haya Mhe. Mwenyekiti naomba tena hebu jamani Waheshimiwa Mawaziri tunapokuja hapa tayari na sisi tumeshafanya *research*. Mhe. Mwenyekiti, haya majibu katika *hansard* ni mwaka 2010/2011 na mwaka 2009 humu haimu, yaani mwaka 2010/2011 peke yake ndio ninayosema labda nisome, ili niridhike kama ni *hansard* naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

> *Hansard* ya tarehe 15 Juni, 2010 ya Mhe. Naibu Waziri Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi wa SMT Bungeni (Dodoma) inasema hivi:-

"Mhe. Spika, Uvuvi wa Bahari Kuu uliingizia mapato kutokana na ada za leseni za uvuvi na usajili wa meli zinazovua kwenye eneo husika. Katika mwaka 2010/2011 jumla ya meli 71 za uvuvi zilisajiliwa na kukatiwa leseni za kuvua katika bahari kuu, mapato yaliyopatikana ni jumla ya Dola za Kimarekani milioni 2,074,400."

Mhe. Mwenyekiti, haya ni majibu na wakati tulipofungua Makao Makuu ya Mamlaka ya Bahari Kuu alikuja pale. Sasa asubuhi nilisoma hata hii aliyoiuliza Mhe. Salmin Awadh Salmin wakati ule na hii ilikuwa bila ya shaka mwaka 2009/2010, kwa sababu yeye alihoja katika mwaka wa fedha 2010 na ilikuwa dola laki 6 na mimi hata sijenda huko.

Sasa mimi nataka hizi za Mhe. Waziri ambazo anatujibu hapa ni kwamba ukijumlisha zao za mwaka 2009/2010 fungu la fedha na mwaka 2010/2011 ndio unapata hizo milioni 2. Kwa maelezo hayo inaonekana hatupewi hesabu sahihi na hawa serikali yenyewe imejibu katika bunge kuonesha kwamba haya ndio mapato halisi. Mhe. Mwenyekiti, bado narejea kauli yangu kwamba hapa kuna kuibiwa.

Kwa hivyo, nasema tusiingie hapo kwa ajili ya kulumbana kama tunaibiwa au hatuibiwi na mimi nilichokitaka ilikuwa ingekuwa ni *very simple* na ndio ingeondosha nong'onong'ono ni kwamba Mhe. Waziri afuatilie mapato yetu haya na sio yale aliyopata. Kwa kweli inaonekana hesabu zile alizopewa si sahihi na wala haiwezekani kama Mhe. Naibu Waziri amelidanganya Bunge na hesabu hizi ziko sahihi, hivyo akatafute kama ni 2010/2011 yalikuwa mapato haya.

Sasa akatafute mwaka 2009/2010 yalikuwa ngapi na baadaye akajumlishe na halafu ndio atapata kwa hiyo asilimia 20 anayoisema ya jumla yake basi ndio itatufanya sisi tupate kwa hizo za mwaka mmoja tu tupate shilini milioni 600 na sio shilingi milioni 200. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo zaidi.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, wazo la Mhe. Mjumbe ni kwamba nikafuatilie, basi nitakwenda kufuatilia. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 0401 - Idara ya Uendeshaji na Utumishi 900,000,000/=
Kifungu 0602 - Idara ya Maendeleo ya Mifugo Pemba

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia eneo hili nilizungumzia mapato ya Kisakasaka na Mhe. Waziri alinijibu na

nimefahamu. Lakini nilimueleza kwamba ng'ombe wanaoingia pale si chini ya 200 au 300 kila siku ya Jumamosi na nilimwambia kuwa mapato ya kila ng'ombe yanayokusanywa ni shilingi 5,500/=, vile vile nilimwambia kwamba risiti wanazopewa si risiti za serikali kwa maana ya Wizara ya Fedha.

Kwa hivyo, amejaribu kuniambia kwamba risiti yeye anaamini kwamba ni risiti halali. Mhe. Mwenyekiti, risiti halali ni ile risiti ambayo ina muhuri wa serikali kutoka Wiizara ya Fedha. Sasa mimi nimefanya utafiti na kugundua kwamba kuna wengine wanapewa risiti ambazo si halali za serikali, maana yake ni risiti za madukani za kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri aniambie kwamba labda nilete risiti hizo ambazo nimeziona za wafanyabiashara wan ng'ombe ambapo mtu ameleta ng'ombe 40 analetewa risiti si halali maana analetewa risiti ambayo haingii kwenye kodi.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri anaponiambia kwamba wako makini na kuamini hivyo, kwa sababu kuamini ni jambo moja na ukweli ni jambo jengine. Mhe. Mwenyekiti, naomba ufafanuzi zaidi.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mimi nashukuru kwa maelezo yake na kwa maelekezo yetu sisi ni kwamba wafanyakazi wanaokusanya mapato watumie risiti rasmi, sasa kama hawatumii hizo basi nipe nafasi nifuatilie nikigundua hilo anayehusika naahidi kumuadhibu.
Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Waziri amekuwa muwazi na hilo na ishaalla mimi namuahidi nitamsaidia taarifa hizo ili aweze kufanya ufanisi zaidi.

Kifungu 0602	Idara ya Maendeleo ya Mifugo Pemba	48,000,000
Kifungu 0801	Idara ya Uzalishaji wa Nyama Unguja	60,000,000
Kifungu 0802	Idara ya Uzalishaji wa Nyama Pemba	9,000,000
	Jumla ya Fungu	**1,020,000,000**

FUNGU22 WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

Kifungu 0010	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	37,044,000
Kifungu 0011	Idara ya Uendeshaji na Utumishi Pemba	401,035,000
Kifungu 0012	Idara ya Mazao Baharini	79,135,000
Kifungu 0013	Idara ya Uzalishaji wa Nyama Pemba	33,871,000
Kifungu 0014	Idara ya Huduma za Utibabu wa Mifugo Pemba	51,421,000
Kifungu 0015	Idara ya Maendeleo ya ya uvuvi Pemba	82,374,000

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba hii nilizungumzia suala la ujenzi wa uzio wa vituo vya Minai, lakini katika majibu ya Mhe. Waziri alisema sababu ya kusimamisha ujenzi huo ni kutokana na kutokuwa na fedha kutoka World Bank, mimi nina masuala kidigo katika hili nahitaji ufafanuzi ujenzi wowote nafikiri unakuwa na mkataba, sijui Mhe. Waziri una mkataba wa ujenzi huu. Na kama unao ujenzi mlikubaliana uanze lini na uishie lini na kwa kuahirisha ujenzi huu serikali itakula hasara kiasi gani katika kusubiria, maana yake huu ujenzi ulikuwa umalize 2010 lakini mpaka hii leo haujakamilika. Kwa hivyo nilikuwa nataka ufafanuzi kuhusu hilo.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ni kweli kwamba ujenzi wowote unatakiwa kuwa na mkataba na pesa ya World Bank haiwezi kutumika bila ya kuwa na mkataba wenyewe ni wakali sana, sasa mikataba ipo na ninayo. Mikataba hii imetiwa asini mwaka Septemba, 2010 kwa hivyo siyumkini kama mkataba umetiwa saini mwaka 2010 jengo limalize Oktoba 2010. Lakini la msingi ni kama nilivyosema mimi kwamba ni kweli nilipoingia nikaona huu utaratibu kwamba kifungu kile cha majenzi pesa kimeshamaliza nikauliza watendaji vipi wakanambia wanasubiri pesa, subirini lakini msitumie pesa za watu hivi hiyo ni kuihami serikali, serikali ikitiwa doa na wafadhili kwamba utaratibu wao ni kutumia pesa jambo bay asana. Sasa sisi lazima tumsaidie Rais tumsaidie Makamo wa Kwanza na Makamo wa pili pamoja na nchi kwa jumla baraza hili tunahusika kuona tunakwenda sawa sawa kwa hivyo hakuna jambo ambalo limefanyika baya, mikataba ipo. Kwa sababu ni uzio serikali au nchi haijapata tatizo namwambia mwenyewe kafahamu baada ya pesa zikishapatikana tayari kazi inaendelea.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, bado mimi ninashaka katika hilo kwa sababu mkataba wa ujenzi utakuwa unaonyesha ujenzi utaanza lini na utakamilika lini, sasa kama Mhe. Waziri yeye ameenda kuzuia ujenzi huo usijengwe kwa sababu ya fedha, mimi anieleze ujenzi huo mlikuwa mmekubaliana uanze lini na ukamilike lini. Makubaliano hayo mapya mmeyapanga muanze lini tena ujenzi mwengine.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, ujenzi sio kwamba usimama lakini umezuiwa kwa hivyo umesimama kwa sababu hizo nilizoeleza, nafikiria Mhe. Muwakilishi angelielewa hiyo hali halisi kwa hivyo ukifika pahali maslahi ya nchi lazima tuyaangalie kidogo, hapa tulikuwa tunaangalia jambo ambalo lina maslahi na nchi zaidi kuliko mambo mengine, kwa hivyo uenzi umeshaanza baada ya kupata pesa taarifa niliyokuwa nayo ni kwamba kila kitu tayari, hayo ndio majibu ambayo naweza kuyazungumza.

Mkataba unasema '*The Contract should be completed in too month from the date of this complete in too month'.*

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, nafikiri mkataba unatueleza kwamba mkandarasi baada ya miezi miwili awe amemaliza ujenzi, cha kushangaza ndio mpaka leo ujenzi haujakamilika na pesa za fungu lile zilikuwepo na ndio maana wakafunga mkataba na yule mkandarasi, kwa hivyo mimi nilikuwa nataka kujua sababu za msingi kwa sababu pesa hizi zipo *World Bank* waliotoa hizo pesa na pesa zipo na ndio maana wakafunga mkataba, wakakubaliana miaka miwili tu kwa sababu ya ujenzi wa uzio, lakiini mpaka hii leo haujajengwa umejengwa nusu na nusu haujakamilika.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Majumbe nafikiri Mhe. Waziri hukumfahamu vizuri Mhe. Waziri hebu nyanyuka tena umfahamishe namna ambavyo ulimpa maelekezo.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti sisi Wizara na wenzangu walionitangulia hawana ujenzi wa huu uzio tu lakini wanajenga na Afisi hiyo ambayo tunaizungumza hapo, kuna ujenzi wa Afisi ya Wizara pale na Pemba vile vile yote hayo ilikuwa April, hii iliyopita tumeshakabidhiwa Aprila, Mei, lakini kwa hali halisi iliyojitokeza Mhe. Mwenyekiti mimi nina vifungu hapa, kifungu ambacho kilikuwa na pesa nyingi kuliko vyote ni vya *consultants* mambo yao wenyewe wanayokuja kufanya fanya kazi. Sasa watendaji wakasema tulia tuziache hizi pesa ziingie katika masuala ya majenzi na upereshen na *training* ili tuweze kuzitumia, hizi pesa zitarudi.

Sasa baada ya kupata pesa hapa panakwenda chini hapo panamaliza, pale Maruhubi wanakwenda na Pemba watamaliza, na hivi vyuo mambo madogo Asifi zimeshahamiwa sasa bado uzio mimi nadhani utauzungumzia uzio, Mimko ishahamiwa, Peka imeshahamiwa na Minai imeshahamiwa sasa wanamalizia ujenzi na sisi tuko makini kama hilo hatuwezi kuhakikisha kwamba pesa hiyo ya mfadhili lazima tuisimamie.

Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, fedha za mfadhili na fedha za serikali zina utaratibu wake wa kuzitumia ndio maana tunaita vifungu, wafadhili wanapotoa pesa zao wakisema kwamba kiasi fulani kiende kwenye ujenzi, kiasi fulani kiende katika *consultancy* sisi kama ni serikali inayofuata utawala bora, lazima tufuate hiyo anachosema Mhe. Waziri kwamba katika ujenzi ule kile kifungu ambacho kiliwekwa fedha kwa ajili ya *consultancy* kilikuwa na fedha nyingi, kama tusingelipata *sonsultancsy* zile pesa zingerudi.

Mhe. Waziri anachosema ni sahihi na tulikuja kushauriana kwamba hizi fedha zisitumike mpaka itoke *no objection* wafadhili wanasema sasa mnaweza kuzitumia kwa masuala hayo ambayo mmeyomba sasa hivi, kwa maana huku kwetu tunaita *ree allocation* kwa hivyo ule muda ambao tulikuwa tunasubiri ndio sasa zimekuja hizo pesa na ndio tunaendelea na huo ujenzi. Sasa ili isilete athari ninaamini kwamba Wizara imemuarifu mkandarasi kwamba tunasubiri hizo fedha na yeye kama ni mkandarasi ninaamini ameridhika anasubiri ili fedha ziingie aendelee na kazi huo ndio utaratibu. Tungeliweza kuzitumia zile pesa wangekuja maodita wao ingekuwa kelele, ingelazimika sisi serikali kuzilipa hizi pesa, ndio kwa maana waziri na watendaji wakasema tusubiri mpaka ije *no objection* na sasa imeshakuja na sasa hivi wanaendelea na kufanya kazi.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, hoja yanagu mimi bado iko pale pale kwamba nasema hapa tulifunga mkataba wa kujenga uzio, mimi sizungumzii jengo kwa sababu jengo limeshahamiwa, lakini nazungumzia uzio baina ya zile nyumba mbili ya Kizimkazi na ile ya Uroa. Ujenzi umeanza ukaachwa mkandarasi yule kachukua pesa, mimi nilikuwa nataka kujua kwanza huu mkataba ambao umefungwa walifunga kwa sababu fungu la pesa tayari lilikuwa lipo na ndio maana wakafunga mkataba na kuna makubaliano.

Kama waliahirisha mkataba kuna maandishi yoyote ambayo waliandikiana au wameahirisha tu hivi hivi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru nadhani majibu yametolewa kwa ufasaha sana, tatizo linakuja labda hatufahamu hoja ya Mjumbe kwa sababu mnapokuwa na mkataba suala la kuahirisha kazi ni makubaliano ni suala ambalo mnaweza kukubaliana na mkikubaliana wakati mwengine hata kama sio kwa maandishi, sheria inatambua kitu kinachoitwa *implied up sentence.* Yaani kama mimi kwa mfano nilitakiwa nifanye kazi ndani ya wiki tatu nikafanya ndani ya mwezi mmoja na wewe hukulalamika, sasa hilo suala kimkataba huwezi tena kwenda mahakamani au kokote ukasema mimi baada ya miezi miwili au mitatu huyu mtu alicheleweza na ukamkubalia.

Sasa kama mkandarasi hajalalamika hajasikitika, hajaleta barua ya maandishi kusema kwamba bwana hili sikubali sasa mimi sidhani kama kuna kosa, pengine awe muwazi zaidi huyu mkandarasi kamfuata kwenda kumlalamikia, lakini kisheria hapa hapana tatizo haya ni makubaliano baina ya pande mbili ni wao wenyewe kama mkandarasi ana tatizo uko utaratibu ataandika barua ya kulalamika na yapo Wizara ndio itaingia kwenye makosa. Lakini kama hakujawa na hilo hakujawa na tatizo hapa, sasa labda atwambie awe muwazi

mkadarasi kenda kumlalamikia na kwa nini amlalamikie yeye kaandika barua Wizarani nadhani hilo ndio jambo la msingi.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Mwanasheria Mkuu, mimi nilikuwa nimeuliza hoja yangu ya msingi hapa zile sababu za mwanzo kwa nini ujenzi ule haukukamilika, kwa sababu mkataba unasema tutajenga ndani ya miezi miwili wamekubaliana na pesa zipo, lakini majibu tukaambiwa hapa Mhe. Waziri anasema kwamba pesa ziliisha lakini wao kwenye mkataba ndio waliosema watajenga ndani ya miezi miwili. Leo hii tuna mwezi katibu wa tisa ule uzio haujakamilika.

Hoja yangu ipo hapa ingawa huko *cabinet* inateteana sana mimi ninachosema ujenzi huu mpaka sasa hivi haujajengwa, sasa Mhe. Waziri hapa anieleze ujenzi huu lini utakamilika.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe hebu tusaidie wasi wasi wako ni nini.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, wasi wasi wangu kuwa huu ujenzi utakamilika lini maana yake una muda mrefu haujakamilika, sasa namuomba Mhe. Waziri atwambie sasa wakati umeshapata pesa lini utakamilika.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, mimi Mheshimiwa Mtando ni swahiba wangu mkubwa labda hii lugha tu hajaifahamu. Nilisema tulikuwa hatuna pesa sasa hivi pesa tayari sasa hivi namhakikishia baada ya mwezi mmoja na nusu itakuwa tayari pesa tayari ninazo.
Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri tuendelee.

Kifungu 0016	Idara ya Maendeleo ya Uvuvi Unguja	201,184,000
Kifungu 0201	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	352,085,000
Kifungu 0401	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	306,740,000
Kifungu 0601	Idara ya Maendeleo na Mifugo Unguja	

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu hapa ni kwamba nilihoji shamba la mifugo Donge Mchangani Mhe. Waziri majibu yake alionyesha kwamba shamba hili limekodishwa na akanishawishi kama nikiwa nina uwezo ana mashamba chungu nzima akanikodishe, kwa bahati mbaya sina uwezo. Lakini nasema kwamba shamba hili lilitengwa na serikali kwa ajili ya mifugo, nikasema kwamba hivi sasa shamba hili limelimwa viyazi sio mifugo ambayo serikali ilipanga.

Mhe. Waziri ananambia kwamba hili shamba sasa hivi limerekebishwa na huenda limepewa mtu mwengine muwekezaji, sera ya serikali ni mifugo na muwekezaji yeye ni sera nyengine ya viazi. Labda anisaidie tu kampa nani ambae lengo lake ni kutia viazi pengine kwa ramadhani aniambie kampa nani tu basi.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Muwekezaji anapokuja sisi utaratibu wa serikali tunaangalia karatasi zake tunawasiliana na *ZIPA* tukiona kwamba *ZIPA* na serikali wakiona sawa basi huwa wanakodishwa, sasa katika ukodishwaji kuna mambo mawili, kuna wakati mwengine muwekezaji mambo yake huwa mazuri kama mambo ya mfugo ufugaji ukawa mzuri alhamdullillah kuna wakati mwengine huweka mifugo yote ikafa ikawa mtihani viumbe vile Mhe. Mwenyekiti.

Sasa anapofika hatua hiyo katika kujivuta vuta angalau atafute mifugo mingine basi shamba hulipanda japo viazi angalau apate chochote mbona inatokea, sasa hivi ndio ninavyoelewa kwamba muwekezaji mzalengo mfanyakazi wa serikali enzi hizo miaka hiyo aliomba kwa taratibu na kakodishwa akaweka mifugo mingi pale nilivyoambiwa ng'ombe, mbuzi bahati mbaya wamekufa.

Sasa hajapata uwezo wa kuweka mifugo mingine sasa anahangaika mimi nimemwita nikamuuliza shamba vipi akanambia naomba muda, kwa sababu nikamwambia vyenginevyo huwezi anayeweza apewe. Yeye alivyonambia sawa sawa wapeni hao wengine mpaka wakimaliza kwa sababu sisi tunayo mengi, ndio nikasema mtu yoyote anayetaka aje ikiwa anapenda tutaelekeza sisi tunataka hasa wazalendo. Mawaziri, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi njoni mashamba tunayo sio yasikae vile.

Sasa tunataka aendeleze mifugo ikifika katikati kama mambo yake yakiwa mazuri hatumwambii tupe mwenyewe kwa sababu hivi hivi, hapana lazima tumpe muda Mhe. Mwenyekiti, hivyo ndivyo ilivyotokea kwa hivyo ni kweli alisema sasa hivi analima viazi lakini akipata hali ataendelea.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti niseme kwamba sikubaliani na majibu ya Mhe. Waziri na nikiendelea na hoja yangu hiyo nikuombe tu kwamba ulipotuomba kuongeza muda ilikuwa imebakia dakika mbili na ukatuomba tukaridhia, kwa hivyo tukiamua kuongeza muda maana yake ni kufanya kazi ya watu unapoamua basi ilikuwa utwambie tukapumzike kwa hivyo kusiwe na maneno kwamba tunachelewesha tu. Tumeongeza muda kwa ajili ya maslahi ya umma wa Zanzibar.

Kwa hivyo mimi nasema kwamba muwekezaji huyu mzale mimi nampongeza sana alipita *ZIPA* akajaza mikataba kwa ajili ya ng'ombe na mbuzi sasa hivi

amepanda viasi, sijui sheria zipi mwanasheria anaweza kutwambia zinasema hivyo. Lakini mimi ninachotaka Mhe. Waziri aniambie huyu mzalendo mwenye imani ya kusaidia wenzake ni nani ili Wazanzibari wajue kumbe wazalendo wanawekeza hapa Zanzibar, tena miradi ya viazi sio mbuzi na Ng'ombe.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, ninachokuhakikishia taarifa niliyopewa ya uchunguzi niliofanya aliweka mbuzi na ng'ombe hilo ndio uhakika, niliuliza mpaka watu wa Donge wenyewe wakanambia huyu aliweka lakini hapa kama nilivyokwambia kuna watu hapa wamepewa mashamba ya kuku ukenda utastaajabu Mhe. Mwenyekiti, mashamba yote kuku wamekufa sasa huwezi kumwambia tupe mashamba yetu yule ni binaadam lazima umpe muda ajitume, sasa hiyo ndio hali halisi inavyokwenda. Huwezi kumwambia ondoka namuomba Mhe. Hija Hassan Hija akubali labda tukiona muda umechukua mwingi na hana la kulifanya basi tutashauriana na serikali tutalichukua wenyewe shamba halafu tutasubiri muwekezaji mwengine ndio utaratibu, huo ndio ubinaadamu hasa wazalendo tuwape nafasi.

Kwa sababu wageni tunawapa muda mwingi sasa mzalendo lazima tumtizame sasa namuomba sana Mhe. Muwakilishi aone kwamba tunachofanya ni ile dhana ya serikali kuwa kuwapa wazalendo nao kuwekeza, kwa hivyo akiharibikiwa lazima tumstahamilie katika nchi nyengine mtu kama huyu hupewa mkopo na mabenki ili akaendeleze, lakini hapa kwetu sahibu wangu Mhe.Waziri wa Fedha, Uchumi na Maendeleo hajaanza, lakini alitakiwa hivyo ameanza amekwama anapewa tena anasaidiwa sasa Mhe. Muwakilishi lazima uwelewe hivyo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti namuomba Mhe. Waziri afuate mwenendo wa Mhe. Omar Yussu Mzee yeye anakuwa anatwambia bila ya kificho yeye ana hisa banki hii, shirika hili na kampuni hii hana wasi wasi.

Mimi sizungumzii mtaji nazungumzia mzalendo ambae amejitokeza naomba jina la huyu muwekezaji hilo ndio tatizo langu tu akinambia basi, Wazanzibari watajua kwamba muwekezaji huyu amewekeza shamba hili kwa ajili ya viyazi.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo Mhe. Mjumbe unataka kumjua nani aliyeekeza.

Mhe. Hija Hassan Hija: Ndio hoja yangu, Wazanzibari wanataka kumjua aliyewekeza ambae ni Mzalendo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti kidogo twende kitaalm unapowekeza vitu kama vya kilimo hasa mifugo, lazima ujitayarishe kwa lishe viazi ukitaka ng'ombe

wako watoe maziwa vizuri sana lima muhogo na viyazi uwe navyo kwa wingi sana na unatanua ule wigo wako wa uwekezaji. Sasa hapo Mheshimiwa kasema aliharibikiwa mwanzo sasa na viazi vinakaa muda mrefu, lazima twende kitaalam tufahamiane ile unawekeza pale Mheshimiwa kasema ameharibikiwa kesho kutwa anaongeza mifugo tena chakula kipo, Donge Mchangani kule sijui naamini Mhe. Hija Hassan Hija ameshafika kule ni hali ya kuchanga ukame pale chakula cha ng'ombe hukioni, hakuna kabisa chakula cha ng'ombe sasa viazi vinakaa anakuja anaanza mifugo tena analisha ng'ombe wake kwa hivyo mradi unaendelea.

Kwa hivyo namuomba Mhe. Hija Hassan Hija afahamu yule lengo lake la uwekezaji wa mifugo upo pale pale aliharibikiwa na tatizo kubwa sana ni lishe kwenye mifugo, nafikiri unaona humo njiani magari yanavyochukua majani ya ng'ombe viazi na muhogo ni tatizo kubwa kwa wakulima.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina tatizo na serikali, mimi lengo langu naisisitiza serikali ni furaha yangu pia waziri afanye kwa ufanisi ili tumsifu. Lakini inaelekea jina la mtu huyu hajuulikani na kwa hivyo hakuna uwekezaji. Mhe. Mwenyekiti, kama serikali nzima jina linawashinda alifikaje *ZIPA*, walimpaje kibali cha uwekezaji, mimi nasema nahitaji jina. Mhe. Mwenyekiti, inaelekea kwamba miradi hii ya uwekezaji serikali wanaificha kwa nini? Mimi sioni tatizo kwamba *public issues* zifichwe hata jina, ikiwa mtu wa Mwambe kama mimi nafichwa Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba kwa maslahi ya wa Zanzibar ili tumjue pengine tunataka kuomba ajira huko.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba nimsaidie kidogo ndugu yangu Mhe. Hija Hassan Hija kwa sababu imetajwa taasisi ya ZIPA na mimi ndiye msimamizi wa taasisi hiyo, mimi nampenda sana ndugu yangu Hija kwa masuala yake yako *very constructive*. Nataka nimwambie kwamba hiki chombo kazi yake ni kutunga sheria, na mimi nitakuwa tayari kumpatia jina la mwekezaji wa hilo shamba analolitaka yeye baadae.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mwakilishi wa wananchi 16,000 na kama ningechaguliwa kwa sura na uwezo nisingepita, kama ningechaguliwa uwakilishi kwa unene, kifua na pesa basi nisingepita, lakini waliniamini kwamba ni mtetezi wa watu. Mhe. Mwenyekiti, mimi sina maslahi yoyote kwenye shamba hili sina mgomba, sina kiazi sina hata mchanga ninachoomba mimi ni Mtumbatu wa Zanzibar wanataka ajira, mimi nakaa Pemba ndugu zangu wako Potoa, Kidoti na Nungwi wanataka ajira, mzalendo amejitolea kwa fedha leo serikali inashindwa kumtaja.

Kwa hivyo, ikiwa wenzangu wataona ni busara hiyo nitamwambie Mhe. Waziri aniambie jina lake, sawa lakini mimi binafsi nasema kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kiwani nina kura asilimia 88 ya Jimbo la Kiwani naomba jina ili nimjue fulani, hilo ndio jambo ninalolitaka mimi kama haliwezekani serikali inambie sisi hatuwezi kumtaja, nitakaa kitako.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, nataka nirudie tu kwamba iliyoguswa hapa ni taasisi ya *ZIPA* nataka nimuhakikishie kwamba aridhike nitampigia simu Mkurugenzi Mkuu wa *ZIPA* ili anipe hilo jina la mwekezaji halafu nimpe Mhe. Hija Hassan Hija akubali kwamba nitampa hilo jina. Kwa sababu akilitaka sasa hivi mimi sinalo hilo jina hapa, na iliyoguswa hapa ni taasisi ya *ZIPA* lazima nimtafute Mkurugenzi wa *ZIPA* nitampatia hilo jina.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nina hakika wa Zanzibar wamenisikia, wameniona na wamenifahamu kwamba serikali haiwezi kunitajia jina hadharani kwa hiyo sina haja ya kupoteza muda naomba tuendelee wa Zanzibar wenyewe wanajua hiyo hali.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, alipokuwa Mhe. Waziri akitupa majumuisho hapa nilizungumzia suala la shamba Pangeni na akatujibu kuwa shamba hilo lina plan ya kuwapa mwekezaji atakayekwenda kutaka kuekeza. Lakini mimi mwanzo ushauri wangu nilitaka kuwa shamba lile ilichukue serikali na iweze kutafuta mbegu iliyokuwa nzuri kati ya ng'ombe na mbuzi. Kwa hivyo, hapa nimeshtuka kuwa bado shamba lile wao wanataka kulipeleka, lakini mimi suala langu liko hapa. Kwa nini Mhe. Waziri hivyo anavyotaka kuwapa wawekezaji kwa nini asiwashauri kwanza wananchi wa Jimbo la Kitope halafu baadae ndio akatafuta mwekezaji?

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, sera ya serikali ni kujitoa kabisa katika masuala ya biashara sasa akinambia kwamba mimi nirudi huko itakuwa tabu kidogo. Kwa hivyo, muongozo ni kwamba tutafute wawekezaji wazalendo na wakigeni ili waekeze, wallahi ningefurahi sana Mhe. Mwenyekiti, kama Mwakilishi wa Jimbo la Kitope na Mbunge wake wangekuwa wawekezaji katika shamba lile, ningefurahi sana. Kwa hivyo, kupitia kwa Mhe. Mwakilishi ambaye yupo namuomba kwamba mtu yeyote wa Kitope ambaye yuko tayari kuekeza, basi aje tutazungumza, tutampeleka *ZIPA* na baadae atawekeza. Kwa hivyo, akipata mtu wa Kitope nitafurahi zaidi maana mazingira ya pale anayaelewa. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mshimba ajue hilo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri majibu yake mazuri sana na mimi kama unavyojua huwa sina tabu, lakini nini maana ya kusema kuwa washauriwe wananchi wangu wa Jimbo la Kitope kwa sababu wengi wao ajira iko pale, lakini kwa kuwa ameshato mwongozo kuwa mimi Mwakilishi pamoja na Mbunge kuwa twende tukaekeze Mhe. Mwenyekiti, mimi ndiye wa mwanzo nitakwenda kwake, naomba tuendelee.

Kifungu 0601	Idara ya Maendeleo ya Mifugo Unguja	197,231,000
Kifungu 0701	Idara ya Mazao ya Baharini Unguja	120,632,000
Kifungu 0801	Idara ya Uzalishaji Wanyama Unguja	226,248,000
	Jumla ya Fungu	**2,089,000,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matunizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 22 – WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

Kifungu 0601 Idara ya Maendeleo ya Mifugo Unguja

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru katika mchango wangu niliomba ufafanuzi wa Mhe. Waziri juu ya *figure* halisi za fedha hizi za matumizi kwa upande wa miradi ya maendeleo ambazo zinatolewa na mashirika mbali mbali pamoja na SMZ. *Concern* yangu ilikuwa ni kwamba kuna mchanganyiko fulani wa nambari kati ya fedha ambazo zilitajwa na bila shaka ni mradi wa miaka 5 katika hii ripoti ya Kamati ya Mifugo, Uwezeshaji na Utalii ukurasa wa 83 nikasema pale ukisoma na bila shaka kamati hii walipewa na watendaji wenyewe.

Lakini *figure* zile na *figure* zilizokuwepo huku ni tofauti kwa hiyo nilikuwa nataka maelezo juu ya *figure* hizi kwani katika kitabu ukizisoma ni tofauti kwa sababu nilimpatia Mhe. Waziri *copy* mapema ya ukurasa ili azione hizi hesabu. Alitwambia kwamba pale alitaja hesabu tu akasema kwamba hizo ndio sahihi, sasa nataka kujua katika hizi ipi ni zaidi kwa sababu hizi ambazo zimo katika kitabu hiki ambacho tunakipitisha hivi sasa ni tofauti na zile ambazo kamati ambazo waliambiwa bila shaka na Wakurugenzi. Kwa hivyo, nataka maelezo kuhusu hili ni figure zipi sahihi na kwa nini kulitokezea mkanganyiko huu.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Jussa alionesha *concern* hiyo haki yake sasa mimi majibu niliyoyapata ni haya ambayo nimempa kwamba hizi ambazo zimetiwa katika kitabu hivi sasa ndio sahihi kwake. Kwa hivyo, naomba aichukue hii ya kwenye kitabu ambacho kimetolewa kiambatanisho hiki.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakubali tuendelee nishauri tu na kupendeza kwamba kamati hii inayohusika na sekta hii itakwenda kufuatilia baadae kwa mwaka huu wa fedha ili iweze kulifuatilia kwa kina hili baina ya zile figure ambazo walituletea ndani ya Baraza na hizi ambazo ametupa Mhe. Waziri, lakini kwa sasa hivi naridhika naomba tuendelee.

Kifungu 0601	Idara ya Maendeleo ya Mifugo Unguja	9,539,445,000
	Jumla ya Fungu	**9,539,445,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matunizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako liyakubali makadirio hayo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe wanaokubaliana na hoja hii ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe sina budi kushukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kumaliza mambo yetu na kazi yetu hii nzito kwa salama na amani, sasa kwa mujibu wa kanuni nachukua fursa hii kuliahirisha Baraza hili hadi kesho tarehe 23/07/2011 saa 3:00 asubuhi.

(Saa 3:14 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 23/07/2011 saa 3:00 asubuhi)